

1 JUNI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini - Tarehe 1 Juni, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Moja, Kikao cha Arobaini, na tutaendelea na ratiba kama ilivyoletwa hapa mezani. Kwa hiyo, naomba nimwite Katibu ili aweze kutuongoza.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2013/2014
Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi**

(Majadiliano yanaendelea)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingi ya wafugaji na wakulima imesababishwa na kutokuwepo na maeneo rasmi yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo na kilimo. Serikali ieleze Bunge ni maeneo yapi na kiasi gani yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo kwa Wilaya za Kaliua, Urambo, Uyui – Mkisi Tabora na Mikoa mingine?

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sheria zinazosimamia mifugo na maeneo ya hifadhi hapa nchini. Sheria hizo zimeainisha aina na viwango vya faini zinazotakiwa kutozwa pale mifugo inapoingia eneo la hifadhi.

Naomba Serikali itamke Bungeni kisheria ni fedha kiasi gani kinatozwa kama faini kwa ng'ombe, mbuzi, kondoo, ngamia pale wanapokutwa hifadhini? Wilaya ya Kaliua, viongozi wamepanga faini ya Tshs.180,000/= kwa kichwa cha ng'ombe na pale wafugaji wanaposhindwa kulipa fedha hizo ndani ya siku tatu, mifugo hiyo inapigwa mnada kwa mafungu na pesa yote inachukuliwa na Wilaya na Polisi walioshiriki kukamata mifugo hiyo, wafugaji wanabaki maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais aliahidi ujenzi wa kiwanda kikubwa cha Nyama – Ruvu kwa nia ya kuboresha sekta ya mifugo na kupata soko zuri la mazao ya mifugo. Serikali itoe majibu ya msingi ni kwa nini mpaka leo kiwanda hicho hakijaanza kujengwa kwa sababu za kuchelewa kwa mchoro tu? Kweli Serikali iko *serious* kwenye utekelezaji wa mipango inayopangwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga bandari kubwa pale Mbegani – Bagamoyo. Chuo cha Mbegani cha Uvuvi ni muhimu sana kwa maendeleo ya uvuvi na pia ni eneo pekee ambapo wanazalisha vifaranga vya samaki na kuuzwa kwa bei nafuu. Ni kwa nini Serikali inataka kuhamisha chuo hiki badala ya bandari kujengwa eneo lingine la mwambao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wengi wamekuwa wanahangaika kwa sababu ya malisho. Wakati wa mvua majani yanakuwa mengi tena mazuri na yanakauka yote. Wizara ina wataalam na Maafisa Mifugo kwenye ngazi ya Mkoa na Wilaya, ni lini Serikali itaanza kutoa mafunzo na kusaidia wafugaji kutengeneza *silage* na *hays* (majani ya kukaushwa) kwa ajili ya chakula cha akiba ya mifugo wakati wa kiangazi?

1 JUNI, 2013

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijielekeze upande wa uvuvi hasa upande wa uvuvi wa baharini hasa ukanda wa Bahari kuanzia Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi hawa wanavua kwa taabu sana kwa vile hawana msaada wa mikopo kwa ajili ya kununua nyavu na kama wapo wenye nyavu za mkopo basi ni wachache sana. Mtakumbuka kuwa mwaka ule wa *operation* ya uvuvi haramu uliofanywa ukanda huo wengi waliathirika kwa matatizo ya kunyang'anywa vifaa vyao vya uvuvi, kwani baadhi yao walionekana kuwa walitumia vifaa vya uvuvi haramu kuvulia samaki, kwa hiyo, wakanyang'anywa. Wavuvi hawa sasa hawana vifaa safi na mbadala kwa hiyo Wizara ifanye tathmini ili kuona wavuvi hawa wameathirika kiasi gani na wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya *operation* hiyo kwa kutumia meli ya Jeshi liitwalo Pono, hali ilikuwa shwari, lakini sasa hali ya uvuvi haramu imerudia tena katika ukanda wa Pwani. Serikali iliahidi italeta boti kwa ajili ya ulinzi wa Pwani ya Lindi na Mtwara, naomba Mikoa hiyo iletewe boti ya *patrol* katika ukanda wa Pwani wa Lindi na Mtwara ili kuzuia uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunaomba kiwanda cha minofu ya samaki Lindi.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole-Nangoro (Mb), Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usindikaji wa maziwa Singida. Napenda kupongeza juhudi za uongozi wa Wilaya ya Singida za kujenga kiwanda kidogo cha kusindika maziwa huko katia Tarafa ya Sepuka kijiji cha Msungua.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kusaidia miundombinu kwani ni duni sana na wataalam pia ni wachache. Serikali ikisaidia, nina hakika kiwanda hiki kitakuwa tija na mafanikio makubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Vilevile itawasaidia wafugaji kutokusafiri mwendo mrefu kwenda kuuza maziwa yaani Singida Mjini. Naomba wakati Waziri anajibu hoja za Wabunge atoe majibu Serikali inasaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kidogo cha kuwamba ngozi. Naipongeza sana Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa kujenga kiwanda kidogo cha kuwamba ngozi na kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa kutumia ngozi mfano viatu, mikanda, mikoba na kadhalika. Kwa kuwa bidhaa ambazo zinatengenezwa ni chache na ubora mdogo, ni vema Serikali kuwapa elimu zaidi wataalam kwa kuwapeleka kozi mbalimbali pamoja na kuongeza wataalam zaidi ili kiwanda kiweze kuwa na uwezo wa kutengeneza vitu vyenye ubora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo vya kuwamba ngozi kujengwa Iramba, Manyoni, na Mkalama. Kwa kuwa Wilaya hizo hapo juu ni za ufugaji, je, kwa nini Serikali isijenge vituo au viwanda vidogo ili kuongeza pato na ubora wa ngozi kuliko ilivyo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga maeneo ya kuchungia mifugo. Bado kuna tatizo kuwa vijiji havitengi maeneo ya kuchungia mifugo hivyo ni vizuri Serikali kutenga maeneo ya mifugo, ili kuondoa mizozo ya wafugaji na wakulima, vijiji vipewe maelekezo rasmi, naomba maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinjio ya kisasa Singida. Naiomba Serikali kujenga machinjio ya kisasa kwani Singida ni kati ya Mikoa mitano ya mwanzo inayofuga ng'ombe. Hivyo hakuna sababu ya kukosa machinjio ya kisasa.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii nikiamini kuwa Serikali itazingatia mchango wangu na kutoa majibu.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji na wadau wote wa Wizara hii kwa jitihada wanazozifanya za kuhakikisha sekta hii ya mifugo inakuwa ni miongoni mwa sekta zinazochangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu wa bajeti. Naomba tuiongezee bajeti Wizara hii kwani tunaweza kwa kutumia mifugo na uvuvi kuinua uchumi wa Taifa na kuachana kabisa na kutegemea wafanyabiashara wachache ndio walipe kodi na Serikali ipate mapato ya kuendesha Serikali. Naiomba Serikali iongeze fedha katika sekta hii kama ambavyo Kamati imeshauri shilingi bilioni 40 kwa matumizi yaliyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati ya Kilimo, Maji, Mifugo na Uvuvi.

(ii) Kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji, nashauri kujengwe mabwawa kwa ajili ya kufugia samaki; miundombinu ya mifugo, marambo na majosho, dawa na malisho na kadhalika; kutengwa maeneo ya wakulima na wafugaji na elimu itolewe kwa wananchi.

(iii) Kufufua na kujenga viwanda kwa ajili ya usindikaji wa mazao ya mifugo na samaki. Naishauri Serikali iongeze kasi ya kuwawezesha Watanzania wazalendo kujenga viwanda kwa ajili ya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi.

(iv) Uimarishaji sekta ya uvuvi, naishauri Serikali itafute fedha na kujenga mabwawa ya kufugia samaki na kukabidhi vijana na wanawake kwa ajili ya kujiondolea umaskini na kuchangia pato la Taifa. Pia Serikali ijielekeze katika kupata meli kubwa ya uvuvi ili iende bahari kubwa na kufanya uvuvi ili kukuza pato la Taifa.

1 JUNI, 2013

(v) Kuwawezesha vijana. Mkoa wa Mara, napenda kujua, je, Serikali imejiandaaje kujenga miundombinu ya wafugaji wa Mkoa wa Mara ili nao wasiingie katika tatizo la ufugaji wa kuhamahama kama ilivyo Mikoa ya Mwanza, Simiyu na Geita na kuwasababishia migogoro na wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia kwa njia ya maandhishi. Mimi mchango wangu utakuwa ni maswali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba aniambie ni kwa nini anaonekana kutambua zao litokanalo na ufugaji ni moja tu au mawili kuwa ni nyama na ngozi? Kwa nini hatambui kama maziwa na mafuta ya samli yatokanayo na maziwa kuwa ni mazao yenye tija?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hujazungumzia suala la Kiwanda cha Maziwa cha Musoma ambacho kinasuasua na hali tukijua kuwa kinahitajika kufufuliwa au kusaidiwa ili kiongeze ajira kwa wafugaji wa eneo hilo na Taifa? Ina maana kipaumbele cha Waziri ni kuongeza majosho na chanjo tu wala si kwa kuimarisha na kufufua viwanda vya nyama, ngozi na maziwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Waziri hivi kuku wapo katika Wizara yake au vipi? Nimesoma hotuba hakuna mikakati yoyote hasa kwa Singida, je, atakuwa tayari kusaidia kutoa elimu ya kufuga kisasa katika Mkoa wa Singida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo yote, naomba niunge mkono hoja.

MHE. MOSHI S KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa siungi mkono hoja hii. Siungi mkono hoja hii kwa sababu hakuna fedha za kufanyia kazi hasa za

1 JUNI, 2013

maendeleo. Wizara hii ina eneo pana sana lakini bahati mbaya Serikali haijawekeza vya kutosha. Tunaomba Serikali iongeze bajeti kama Kamati ya Kilimo na Mifugo ilivyopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo ni muhimu sana kama Serikali itawekeza na itainua pato la Taifa. Kwa wakulima na wafugaji, kama tutawekeza miundombinu ya malisho, malambo na majosho, wafugaji hawatahamahama. Ni vyema Serikali ikaangalie jambo hili ili liweze kuwasaidia wananchi wanaoishi katika maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda vya kusindika nyama litasaidia kukuza uchumi na kupunguza mifugo ambayo ni mingi kiasi kwamba inasababisha uhaba wa malisho ya mifugo. Naishauri Serikali iwekeze kwenye viwanda vya kuchakata na kusindika nyama na viwanda vya ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haujawezeshwa kwani kama wakiwezeshwa tutakuwa tumewasaidia sana wavuvi wa Ukanda wa Bahari, Maziwa Makuu na Mito mikubwa iliyopo katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema mkaongeza doria kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu ambao umeshamiri. Mbaya zaidi uvuvi huo umekuwa ukifanywa na mataifa jirani ambayo yananufaika na rasilimali za nchi yetu. Ukienda Ziwa Victoria wanaonufaika na Ziwa hili ni nchi ya Uganda na Kenya na wakati huo wao wanamiliki sehemu ndogo ya Ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa, hakuna uwezeshaji wowote uliofanyika katika maeneo hayo. Ni vyema Serikali ikawa na mpango mkakati wa kuwezesha wafugaji wadogo wa samaki katika maeneo hayo. Tunahitaji kuwe na miradi mikubwa ya uwekezaji kwa kujenga viwanda vya kuchakata samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuitaka Serikali itoe maelezo juu ya meli iliyoshikwa ya Wachina ambayo

1 JUNI, 2013

ilikamatwa ikiiba samaki ukanda wa Bahari ya Hindi. Mpaka sasa hatujui iko wapi wakati wenzetu wa Msumbuji wao wanaitumia kwa shughuli za kudhibiti wavuvi haramu. Naomba nipate maelezo ya kutosheleza kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo ya Waziri juu ya nyongeza ya bajeti ya shilingi bilioni arobaini zilizopendekezwa na Kamati.

MHE. SUSAN L.A.KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo ni nyeti sana katika nchi yetu kwa amani na maendeleo ya nchi yetu lakini Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo za maendeleo kila mwaka, karibuni kila mwaka inashuka kwa takribani shilingi 14 bilioni. Sasa kuna haja gani ya kupitisha bajeti ambayo haitaweza kutatua matatizo ya wafugaji na wavuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa 85, Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilombero inasomekaa kwamba Serikali imepima vijiji 25 na kutengwa kwa ajili ya ufugaji na malisho (Ha) 78,754.30. Sasa nataka majibu ya Serikali ni vijiji gani kwa majina na kila kijiji kuna ng'ombe wangapi? Je, kwa maeneo yaliyotengwa kwa wafugaji, Serikali imepeleka miundombinu ipi kwa wafugaji? Serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha wafugaji ili wafuge kwa faida na Serikali kuwahakikishia soko bora la mazao yatokanayo na mifugo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu ya Serikali ni kwa vipi wameshughulikia kero za wafugaji wa Kilosa kwa kuwapa maeneo ya kufugia ili kukomesha mapigano kati ya wafugaji na wakulima yanayotokea mara kwa mara katika kata ya Msowelo Parakuyo (kijiji) na kwingineko? Je, kwa nini Serikali imeshindwa kuwashirikisha wananchi na wafugaji wa Kilosa katika ugawaji wa Ranchi ya Mkata na kugawa ardhi hiyo kwa wawekezaji wa nje na kuwaacha wafugaji wa Kilosa/Parakuyo wanahangaika na mifugo yao

1 JUNI, 2013

kwa kukosa maeneo ya kuchungia? Kwa vile wamepakana na hifadhi ya Mikumi kwa sasa wana uhaba wa eneo la kuchungia. Wanachi wa Kilosa wanaomba uamuzi wa Serikali kutoa eneo la Mkata kwa wawekezaji wakubwa ubatilishwe na wapewe wafugaji wadogo ambao wana uwezo wa kulipa gharama zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije na majibu ya kuboresha na kuwezesha ujenzi wa mabwawa ya samaki kwa wananchi wa Wilaya ya Kilombero na Ulanga kwa kuwa Mto Kilombero ndio tegemeo la wananchi wa Wilaya hizo. Sasa hivi Serikali inazuia wavuvi kuvua katika Mto huo, ingawa kuna kipindi wanaruhusu lakini inaleta tabu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kupiga marufuku uvuvi wa nyavu zenye matundu madogo, mkumbuke Mwenyezi Mungu na uumbaji, alumba samaki wa aina nyingi wengine ni wa kudumu na wengine ni wa msimu. Mfano katika Mto Kilombero, kwa kipindi cha mavuno mwezi wa Mie, Juni na Julai wapo samaki wanaopatikana kwa wingi kama Njuju (dagaa saizi ya kati), Mlamu Kaliandili yaani dagaa wadogo sana, hivyo wanavuliwa kwa nyavu zenye matundu madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja hadi nipate majibu ya Waziri kuhusu ujenzi wa mabwawa na majosho, ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki, shamba (ranchi) ya Mkata iliyopo Kilosa kugawiwa kwa wafugaji na kuhusu ujenzi wa viwanda vya mazao ya mifugo Mkoani Morogoro.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchungia mifugo, uhibitaji wa magonjwa ya mifugo. Wizara ilibaini virusi vya ugonjwa wa miguu na midomo. Wizara imekiri kutekeleza mkakati wa kuzuia ugonjwa wa miguu na midomo (*RMD*) maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imewatelekeza wananchi wafugaji muda mrefu sana wana Maofisa Mifugo kila Wilaya haohao kilimo, haohao mifugo. Wanafanya kazi

zao, wafugaji wanahangaika huko vijijini kwa magonjwa haya, kupe ndorobo, kupasuka miguu, midomo, ugonjwa mbaya na unauwa sana ugonjwa wa sotoka. Je, Wizara haijui kuwa Wilaya ya Chemba na Kondoa na Mkoa mzima wa Dodoma ni wafugaji kwa nini hawatokomezi hawa mbungo, kupe, kuzuia kero kwa viumbe hawa? Lini Wizara itamaliza kujenga majosho nchi nzima? Takwimu zilizotolewa ni za kubuni si kweli kwani ni muda mrefu sensa ya mifugo haijafanyika kabisa, ni muhimu sasa Serikali iwe makini na kazi zao na si kukaa mezani tu na kuletewa kwani mifugo tuliyo nayo ndiyo dira ya pato la Taifa na ni chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku, ng'ombe, vifugwavyo vyote tukitoa kuku wakipelekwa mnadani kuuzwa hutozwa ushuru na kila mfugo hulipiwa ukiwa majumbani kodi za tozo na kadhalika. Wakati anafuga mwenyewe mfugaji kabanwa hana eneo la machungaji bado na maliasili, hivi kero hii itaisha lini hasa kwenye vijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo hutupa faida ya ngozi, maziwa, mapato, kwa nini Serikali haiangali hili? Punda hubeba mizigo bila huruma hata gari huharibika na kutengenezwa, je, hawa wanyama hawaonewi huruma, Serikali inasemaje kwa hili? Mbona ushuru wake wanachukua, malambo hawajengi, lini watawaokoa wanyama hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uvuvi bahari, tunazo na maeneo makubwa tunayo kwa kuwa wananchi wengi wa maeneo yenye Ziwa, Bahari na Mabwawa yenye samaki hawana amani ya uhuru wa uvunaji na hawapewi eneo au la kuvua na wao wawe wanajipatia riziki wao na vizazi vyao lakini wakienda kuvua tu hukamatwa na kutozwa faini na kunyanganywa nyavu. Serikali haijajipanga kuwasaidia wananchi kwenye sekta nzima ya uvuvi hebu itoe fursa ya muda wa kuvua samaki wananchi wapate riziki, waachiwe kwa uwiano, wananchi wapewe elimu ya faida na hasara ya uvuvi, kuna mito pia ina samaki waachiwe maeneo ya kuvua na kupata chakula na biashara.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja kwani Serikali haiwajali wafugaji inajali maslahi yake kumtoa kodi mwananchi na mifugo yake na kuwadhalilisha wavuvi kutwa kukamatwa na kuitwa wavuvi haramu na kuwaporu nyavu na madukani zinazwa.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam ndio soko kubwa la mifugo yaani nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo kuku na kadhalika lakini kuna tatizo kubwa sana la machinjio ya kisasa. Nataka kufahamu kuna mkakati gani wa Serikali kujenga machinjio ya kisasa katika Jiji la Dar es salaam au kujenga machinjio ya kisasa katika Wilaya ya Kinondoni ambapo eneo liko tayari kwa sababu kuendelea kuwa na machinjio kama ile ya Vingunguti ambayo hairidhishi ni hatari kwa afya za wakazi wa Dar es Salaam. Nafahamu kujenga machinjio moja kubwa ya kutosheleza Jiji la Dar es Salaam ni gharama kubwa sana lakini tuangalie kujenga katika kila Wilaya yaani Kinondoni, Temeke, Ilala zijengwe kama hii iliyojengwa Dodoma ambayo gharama yake si kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya kina kuhusu jambo hili, tumelalamika sana sisi wakazi wa Dar es salaam lakini Wizara inatupuza.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hotuba yangu kwa kumpongeza Waziri na Watendaji wake wote. Bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana ukilinganisha na changamoto kubwa sana walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kwa wafugaji na wakulima bado ipo mingi na mikubwa inajitokeza hata kusababisha umwagaji wa damu. Je, Serikali imeweka mkakati gani utakaosaidia kuleta suluhu kwa migogoro hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa Maafisa Ugani, kama kweli Serikali yetu inataka kuleta tija katika sekta hii ya mifugo, ni vema ingekuwa na mkakati wa makusudi ili kila Halmashauri kuwe na hawa Maafisa Ugani wa kutosha na Maafisa hao wapite katika Kata, Vijiji kwa wafugaji

1 JUNI, 2013

kuwapatia elimu na mara nyingi tumeona hawa Maafisa Ugani maeneo mengine wanatoa huduma hiyo kwa kuwatoza pesa. Hii inasababisha baadhi ya watendaji kutowajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wengi hawana utaalam, wananchi wanafuga kwa kubahatisha tu. Vilevile maeneo yaliyo mengi hakuna maduka ya madawa kwa ajili ya mifugo. Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wafugaji wanakuwa na maduka na vituo kwa ajili ya kutibu mifugo. Kuna magonjwa mengi yanajitokeza katika mifugo lakini hakuna mkakati ulionekana kwa ajili ya kunusuru mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu machinjio ya nyama, sina uhakika kama Wizara hii inaelewa hali ya baadhi ya machinjio yetu yanavyofanya kazi. Naomba nitoe mfano tu hali za machinjio ya Ukonga Dar es Salaam, wanachinja mifugo katika hali ya uchafu sana kiasi kwamba inahatarisha hata afya ya walaji. Nimetoa mfano wa machinjio moja tu lakini ni vema Wizara ingekuwa na utaratibu wa kuwa na kitengo cha ukaguzi ili kuweza kubaini hali halisi za machinjio zetu zinavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia Wizara iwe na mkakati wa kusaidia baadhi ya machinjio yaliyopo katika Halmashauri kama machinjio iliyopo katika Jimbo la Iringa Mjini, machinjio ile imekuwa na ujenzi wa muda mrefu sana usioisha kutokana na bajeti finyu ambayo kila mwaka inapewa ahadi lakini pesa haziletwi. Ni vigezo gani vinawekwa kwa ajili ya kupewa pesa hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SILYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inasimamia maendeleo ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina mifugo mingi kama ilivyoainishwa katika Hotuba ya Waziri, lakini tatizo kubwa ni ubora wa nyama itokanayo na mifugo hii.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi kikubwa cha mifugo iliyoko kwa wafugaji wadogowadogo ina nyama duni isiyo na ubora. Hii imepelekea makampuni mengi yawekezayo katika uchinjaji na usindikaji wa nyama, kushindwa kuwekeza kwa madai kuwa, nyama tuliyonayo haina ubora. Mfano mzuri ni *Farmers Choice* ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imetokana na kutokuwa na mashamba makubwa ya ufugaji kibiashara (*Commercial Ranch*), kwa ajili ya kuwa na mbegu bora, lakini ng'ombe kupewa vyakula vizuri na kutotembea umbali mkubwa na hata kuumizwa kwa kupigwa. Hii huzingatia ubora wa mbegu kwa kuzalisha ndama bora wa nyama na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua sasa Wizara ina mpango gani wa kuzalisha na kusimamia vyema mitambo ya kisasa na mashamba ya mifugo ya kibiashara? Wizara ina mpango gani wa kuwafikia wafugaji wadogowadogo na hususan wale wanaofuga ndani (*Zero Grazing*) ili waweze kuzalisha nyama na maziwa kwa mpango wa ufugaji bora wa kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutegemea bahari na maziwa na mito kwa kupata samaki, linaelekea kuwa gumu na kuwa mipango ya ufugaji wa samaki ni mkombozi wa Wananchi ili kuweza kuzalisha samaki wa kutosha na bei ya kuridhisha. Ufugaji wa samaki kwa mabwawa una ufanisi mkubwa, naiomba Serikali kupitia Wizara hii, itoe mafunzo na kipaumbele katika ufugaji wa samaki na hii italeta mapinduzi ya ulaji vyakula bora na ulaji wenye afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuomba Serikali sasa ijikite katika kuendeleza mashamba makubwa ya mifugo, yaani *Ranch* kubwa za kibiashara, itenge maeneo ya kuanzisha *Ranch* hizi ili uzalishaji wa mazao ya mifugo uwe na tija, yaani kupata nyama bora na nyingi kwa eneo dogo. Kwa kufanya hivi, tutapunguza migogoro ya wakulima na wafugaji ambao kwa hakika unahitaji sana maendeleo makubwa.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali pia ianzishe Programu Maalum ya Elimu ya Ufugaji wa Samaki na iwe sehemu ya elimu ya ujasiriamali katika hatua mbalimbali za elimu wafuzuyo Vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwe mwisho sasa wa migogoro ya malisho ya mifugo na mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida katika mazao yoyote yale hupatikana kwa kuongeza thamani kwa kupitia usindikaji. Ni aibu hata miji yetu mikubwa mazao ya mifugo kuanzia ngozi na nyama, haisindikwi kitaalam na hasa machinjio ya Serikali yako katika hali duni sana, hayakidhi kiwango hata kidogo. Kiwango cha majengo yenyewe, kiwango cha afya katika mfumo mzima wa kuanzia kupokea mifugo hai, namna ya kuiua na hata namna ya kuchuna na kutoa nyama yenyewe. Uhifadhi wa nyama kwa maana ya mafriji, ndiyo kinachopelekea hata ubora kupotea kabisa. Natoa wito kuwa sasa Serikali ioneshe mfano wa viwango vya machinjio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David – Waziri, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro - Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa jitihada wanazofanya kuendeleza Sekta hizi za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba Wizara itusaidie Wakazi wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kuboresha malisho ya mifugo, kwani ardhi tuliyonayo ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya mifugo.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kwa vile maeneo yenye wafugaji wengi kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi ikiwemo Kata za Oldonyosambu, Olkokola, Mwandet, Musa, Kisongo, Mateves, Oljoro na Bwawani, yanapata mvua kidogo sana na hakuna vyanzo vya maji yafaayo kwa matumizi (mfano Oldonyosambu), naomba tusaidiwe kujenga malambo ili mifugo ipate maji ya kutosha na malambo hayo yatumike kufuga samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, naomba Wizara itusaidie kuendesha mafunzo kwa vijana juu ya ufugaji wa samaki na kutusaidia au kushauri juu ya namna ya kupata mitaji kwa ajili ya kuanza na kuendeleza ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kunusuru Ziwa Rukwa lisiweze kukauka kutokana na msongamano wa mifugo mingi kandokando ya Ziwa Rukwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Rukwa ni Ziwa lenye mamba wengi ambao huchangia kwa sehemu kubwa madhara mengi sana kama kumaliza samaki, kuuu wavuvi na kuwala na kujeruhi wavuvi na kuwaacha vilema na wala Serikali hajatoa fidia yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kumpelekea Mheshimiwa Waziri, mapendekezo ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kuwa nini kifanyike katika Ziwa Rukwa; hadi leo hii sijapata majibu au maelekezo yoyote na Mheshimiwa Waziri anipe majibu juu ya Ziwa Rukwa katika kulinusuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri anipe majibu Shamba la Malonge ni la kulima au la kufuga?

Hivi kazi ya Wizara hii ni nini? Wawekezaji wanakiuka mikataba na watu waliopewa dhamana ya kulinda haki hii wapo na hawafanyi hivyo. Kuna sababu ipi ya kuendelea kuwa na watu hawa? Hiki ni kitendawili? Nani afanye?

1 JUNI, 2013

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kuleta maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii kwenye maeneo mawili yafuatayo:-

Kwanza, tatizo la mgogoro wa mpaka kati ya Chuo cha *LITI* Mpwapwa na Kijiji cha Kibodyani katika Jimbo la Mpwapwa. Mgogoro huu sasa (suala zima) liko Mahakamani. Ninayo imani kwamba, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya ya Mpwapwa, mtaingilia kati na kufikia mwafaka mzuri wa mgogoro huu kwa manufaa ya pande zote mbili.

Pili, Chuo cha Utafiti wa Mifugo *LITI* Mpwapwa kuwa Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine – Morogoro, Mheshimiwa Rais alishakubali suala hili. Je, Wizara inasemaje kuhusu hili au inatoa ushauri gani?

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni moja ya kazi kubwa ya Watanzania wengi. Tanzania ina miti mingi, Mabwawa, Maziwa na Bahari. Ni dhahiri kuwa, ingeendelezwa na hasa kilimo cha ufugaji wa samaki, sekta hii ingeweza kudumisha uchumi, kuleta ajira nyingi sana na kuboresha lishe ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa samaki; inasikitisha sana kuona Sekta hii imepuuzwa kabisa kabisa, hata ukiona bajeti yake huwezi kudhani eti ipo kwenye KILIMO KWANZA au tuelewe KILIMO KWANZA hakijumuishi mifugo na uvuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vipi kuwe na bajeti ndogo ya bilioni 38 ambazo katika hizo bilioni tisa vikiwa ni kwenye mapato yake ya mwaka?

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo ni bilioni tatu tu kutoka ndani na bilioni tano toka nje, lakini fedha hizo nyingi kwa ajili ya utafiti tu. Hakuna fedha zozote Maendeleo ya Uvuvi, hakuna fedha kwa ajili ya uboreshaji wa malisho ambazo ni kazi nyeti kwa maendeleo ya jamii ya wavuvi na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza vijana hawana ajira, lakini hizi si ndiyo zingeweza kuwasaidia vijana kujiajiri. Mimi nilienda kule Kisiju, nimekuta vijana wamejikusanya wanachimba mabwawa, lakini ni Mbunge wao tu Mheshimiwa Adam Malima ndiye alikuwa anawapa msaada kidogo na kuwawezesha kupata kama milioni moja na nusu tu kwa mwezi kwa vijana zaidi ya ishirini. Jinsi vijana hao wanavyojituma katika mazingira magumu hayo, mapato ya mwezi yingeweza kuwa ya siku.

Ukichukua ukanda wote wa Pwani toka Mkoa wa Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara, unaona jinsi gani Sekta hii ingeweza kutoa ajira. Hapo hujaweka Mito na Maziwa Makuu. Mheshimiwa Waziri atueleze ni mkakati gani umeandaliwa na Wizara kuwawezesha vijana wote kuweza kujiendeleza kwenye fani hii na wapi itatoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unenepeshaji wa mifugo; bajeti kama inavyoonyesha haina fedha zozote kwa ajili ya *Pastoral System Development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna uhaba wa malisho na ndiyo maana wafugaji wamekuwa wakipeleka mifugo mbali na hata kuvamia mabonde ya hifadhi. Wafugaji hawa wanatafuta malisho ya mifugo yao. Serikali imekuwa ikiwaasa wapunguze mifugo, lakini hili lingeenda sambamba na Mradi wa Kunenepesha Mifugo ili ufugaji utoe tija, ingekuwa ni rahisi kuwaelekeza na wangeelewa kwa urahisi kwa sababu na wao wangeona tija kwamba ingawa mifugo ni michache, lakini mapato ni makubwa kuliko wakati wakiwa na mifugo mingi.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wengi ni wafugaji wa kuku wa kisasa kwa ajili ya nyama na mayai, lakini hivi sasa ufugaji wa kuku wa kienyeji umekuwa maarufu kwa akinamama hao. Ufugaji wa kuku huleta kipato na ajira siyo tu kwa wafugaji bali hata kwa Wananchi wanaojishughulisha na biashara ya chakula. Bajeti nzima ya Maendeleo, hakuna bajeti yoyote inayohusu ufugaji wa kuku! Hivi sasa hii bajeti tunapitisha nini mishahara tu ya watumishi?

Mimi nitoe ombi, kama Serikali inaona Wizara hii siyo muhimu, basi si wairudishe kwenye Wizara ya Kilimo ili tupunguze gharama na iwe Idara tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja hadi hapo nitakapopata ufafanuzi wa kina.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa Mungu, kwa kunipa nafasi ya kutoa ushauri, kero, maoni na maelekezo kwa Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana tukatambua ni fedha kiasi gani tunaokoa kwa kutoagiza nyama nje ya nchi, kwa kuwa wafugaji wetu wanatosheleza mahitaji ya nyama humu ndani na ziada kusafirishwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na uokoaji wa fedha zote hizo, bado wafugaji wanalilia maeneo ya malisho na kuleta migogoro ya wakulima na wafugaji, hadi kupelekea vifo na uvunjifu wa amani. Kwa nini Serikali ishindwe kumega eneo la hifadhi kwa kuwapa wafugaji ili kupunguza mitafaruku isiyo ya lazima na kupunguza kasi ya mapigano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe maeneo ya hifadhi yetu ni makubwa mara mbili ya Nchi ya Rwanda na Burundi na bado Serikali imekuwa ikiyaongeza kila mara. Napenda kusikia majibu ya Serikali kuhusiana na kuwapa maeneo ya malisho wafugaji wetu na kuongeza pato la mfugaji mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo mwanzo, pia napenda kupata majibu ya Serikali ni kiasi gani tunapata faida au tunaokoa fedha kiasi gani baada ya nyama kutoagizwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa sana wa Samaki katika Ziwa Victoria na hii inatokana na uvuvi haramu unaoendelea katika Ziwa Victoria. Pamoja na juhudi za Serikali kuzuia uvuvi haramu, bado ipo haja ya kutengeneza *syllabus* kuanzia shule za msingi, kufundisha athari za uvuvi haramu na uharibifu wa mazalia ya samaki, sambamba na kufundisha jinsi ya kufuga samaki na kuchukua uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wafanyabiashara wenye viwanda vya samaki hapa nchini ndiyo wenye viwanda vya samaki Nchi jirani ya Kenya. Ninayaandika haya kwa uhakika kabisa, bado Serikali haijawa na nia ya dhati ya kupigania na kusimamia bei ya samaki kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wavuvi wa Tanzania wamekuwa wakipewa bei kandamizi na wenye viwanda na kupelekea hasara kwa wavuvi wetu kuuza samaki katika viwanda vya Tanzania na wenye viwanda hao hao wanatoa bei nzuri sana kwenye viwanda wanavyomiliki Kenya na kupelekea wavuvi wetu waliopo Visiwa vya Tanzania kama vile Kweru, Goziba, Malelema, Irugwa, Ghana, Kome kwa Juma, Ukara, Siza na maeneo mengine, kwenda kuuza samaki Homa bay na Kisumu – Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na Serikali ya Kenya kulinda ajira za watu wao kwenye viwanda vya Kenya na huku ajira za viwanda vya samaki vilivyopo Tanzania kufungwa kwa kukosa samaki kwa makusudi kwa hujuma za wenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la samaki nje ya nchi ni moja; inakuwaje bei ya manunuzi kwa viwanda vya samaki kuwa tofauti kati ya Kenya na Tanzania?

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya Wizara kuitakafari jambo hili kwa kina na kuamua kama Taifa ni namna ipi ya kuwasaidia Wavuvi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali ya samaki kuwa mbaya kwa maana ya kuwa samaki wamepungua sana, ni vigumu sana kuwazuia wavuvi kuvua maana Ziwa ni kubwa sana na mipaka yake inaweza kuwa ngumu kui-*manage*. Jambo jepesi linalowezezana ni Wizara kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuweka Azimio la Kununua Samaki wa Biashara kwa msimu wa kuanzia Mei hadi Disemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia sana kutoa nafasi ya samaki kuzaliana na kuwapa wavuvi matayarisho ya zana zao. Ni vizuri zaidi kuweka Azimio kwa Mabunge yetu kwa nchi zenye Ziwa Victoria. Pia Bunge la Afrika Mashariki liweze kusimamia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusikia kutoka kwa Serikali kupitia Wizara kama jambo hili litachukuliwa kwa uzito wake au litapuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nitapata nafasi ya kuchangia kwa mdomo, basi nitaweza kuongea na kutoa maoni zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kuwa, mimi pia ni mfugaji na Mjumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono Hotuba ya Waziri husika, naelekeza mchango wangu katika dawa za kinga, ambazo Serikali inagharamia kwa gharama kubwa ila mara nyingi huwa hazifiki kwa wakati mwafaka. Kufanya hivyo ndiyo chanzo cha wafugaji kuanza kuwalalamikia Viongozi wao wa Wilaya husika au Serikali ya CCM.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu, pamoja na kuwa na mifugo zaidi ya milioni 22, bado wafugaji hawafaidiki na mapato yenye faida nzuri katika kuuza mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba Serikali iweze kusambaza mizani ya kupimia mifugo katika minada yote nchini ili waweze kuwasaidia wafugaji wanufaike na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza jambo hili kwa sababu walanguzi wa mifugo wanawalalia bei wafugaji kwa kununua mifugo bila kupimwa. Mlanguzi anapanga bei ya ng'ombe, mbuzi au kondoo kwa kuangalia tu; kwa kweli wanaumizwa sana wafugaji. Walanguzi hao wengi hawana huruma na pia hawamwogopi Mwenyezi Mungu.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhifadhi mazingira, kuondoa mgongano wa masilahi baina ya wafugaji na wakulima na pia katika kupata ubora wa mifugo, Serikali iliwasilisha Miswada miwili katika Bunge la Tisa, Mkutano wa Afrika mwaka 2010 inayohusiana na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada hiyo ambayo baadaye ilipitishwa kuwa sheria na ilikuwa ni Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo (*The Livestock Identification, Registration and Traceability of 2010*) na Sheria ya Malisho na Chakula cha Mifugo ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hizo mbili kama zingelitekelezwa, basi hii migogoro ya kugombania ardhi baina ya wafugaji na wakulima, ingelipungua kiasi kikubwa. Ninaitaka Serikali inieleze sheria hizi muhimu kwa Sekta ya Mifugo kwa nini mpaka leo hazijatekelezwa na utekelezaji wake utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni ya tatu kuwa na mifugo mingi Barani Afrika, lakini mchango wake katika Uchumi wa Taifa wa Sekta hii, haulingani na wingi wa mifugo hiyo. Wizara wanafikiria nini kuhusu kukuza mapato ya Sekta hii ili Taifa letu lifaidike zaidi na mapato hayo?

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inakabiliwa na uchache wa mapato licha ya kuwa na samaki wengi katika Bahari na Maziwa. Bado wingi wa samaki hawa haujasaidia ukuaji wa mapato na uchumi kwa jumla. Lipo eneo kubwa la Bahari ambalo kama litavuliwa ipasavyo, basi uchumi wa nchi pamoja na mapato ya wavuvi yataongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha, mpaka leo hali za wavuvi wetu kimaisha ni ngumu sana na mapato yao ni madogo, hayaendi sambamba na ukuaji wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga vipi ili Sekta hii ya Uvuvi ichangie ipasavyo uchumi wa nchi kama ilivyo Namibia wakati nchi hiyo eneo lake la uvuvi ni dogo ukilinganisha na nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa asili unakabiliwa na changamoto kuu zifuatazo:-

(1) Upungufu wa maeneo ya malisho.

(2) Upungufu wa mabwawa na malambo/ majosho, mahali pengi (mfano katika Kata nyingi Bukombe) hayapo kabisa.

(3) Wakati wa kiangazi (au ukame) ufugaji wa asili unakabiliwa na ukosefu wa nyasi karibu nchi nzima kwa kuwa nyasi hukauka na mahali pengi huchomwa. Pia mabwawa mengi hukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye nini ili kupunguza makali ya changamoto hizi?

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa maeneo ya malisho, Serikali haiwezi kuendelea kujificha nyuma ya pendekezo kwamba wafugaji wa asili wafuge kisasa kwa kupunguza ng'ombe wao taratibu kwa kuwauza. Wafugaji wa asili wana imani yao kuhusu mifugo. Pendekezo ni zuri, lakini haliwezi kutekelezeka katika kipindi cha muda mfupi. Inabidi Serikali iendeshe elimu kuhusu ufugaji wa kisasa, lakini wakati huo huo ikiwa imeongeza juhudi katika kuwapimia na kuwatengea maeneo ya malisho kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza tatizo la malisho wakati wa kiangazi, Serikali lazima iandae mpango kabambe wa malisho mbadala (badala ya nyasi ambazo wakati wa kiangazi huwa zinanyauka au kuchomwa). Kadhalika, Serikali iwezeshe uanzishwaji wa viwanda vya kutengeneza chakula cha wanyama, pamoja na viwanda vya kutengeneza mabunda ya nyasi. Hatua hii itaweka sokoni bidhaa muhimu ambayo baadhi ya wafugaji watainunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la upungufu au ukosefu wa mabwawa na malambo/majosho. Serikali ifanye tathmini ione kuna upungufu/ukosefu kiasi gani ili iandae mpango wa kutatua kabisa tatizo hili. Sambamba na hatua hizi, Serikali ifanye yafuatayo:-

(1) Serikali iharakishe mchakato wa kuwatafutia masoko mazuri wafugaji wa asili.

(2) Serikali iwezeshe uanzishwaji wa viwanda vya kutosha vya maziwa katika maeneo yote yenye mifugo. Hakuna sababu kwa nini Kenya ituzidi katika uzalishaji wa maziwa wakati sisi tunawazidi idadi ya ng'ombe.

(3) Serikali iharakishe mchakato wa uanzishwaji wa viwanda vya nyama.

(4) Machinjio ya kisasa yaanzishwe katika kila Wilaya yenye mifugo wengi.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo hatua hizo zitatekelezwa kwa makini na mpangilio, sekta ndogo ya ufugaji wa asili itastawi na kuwaletea neema wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nitakaloongelea ni ufugaji wa samaki vijijini kwa kutumia mabwawa. Hivi sasa Serikali haina mpango kabambe wa Kitaifa wa ufugaji wa samaki kwa mabwawa. Kuna miradi michache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika, Serikali iandae mpango wa kitaifa wa kuanzisha ufugaji wa samaki wa mabwawa, hasa vijijini. Mpango huu utaongeza ajira na kupunguza/kuondoa umaskini kwa vijana wengi watakaoungana katika makundi. Mpango huu ujumuishe uchimbaji wa mabwawa madogo madogo na mabwawa makubwa.

Mabwawa madogo madogo yawe kwa ajili ya kaya na mabwawa makubwa yawe ni kwa miradi mikubwa ambayo inaweza kuendeshwa na makundi ya vijana au wawekezaji wazawa. Mchango wa Serikali hapa uwe ni pamoja na mafunzo ya ufugaji wa samaki, jinsi ya kuchimba mabwawa madogo na makubwa, kutoa mbegu ya samaki na kusaidia katika kutafuta soko la samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, kwanza kuhusu ufugaji wa asili, Serikali iendelee na hatua chanya inazochukua. Hata hivyo, iepuke matendo yoyote hasi yanayojenga uhasama na wafugaji wa asili na badala yake iwashirikishe katika kutatua matatizo mbalimbali.

Pili, kuhusu ufugaji wa samaki vijijini, Serikali ichukue hatua ili ufugaji wa samaki vijijini uweze kuwa shughuli muhimu ya kiuchumi vijijini. Ni shughuli isiyo na changamoto nyingi kama ufugaji wa wanyama kama ng'ombe, mbuzi, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

1 JUNI, 2013

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina changamoto nyingi Kitaifa. Pamoja na nchi yetu kufahamika katika Afrika kwamba kuna mifugo mingi, mchango wake katika pato la Taifa ni mdogo sana. Lakini pia sekta yetu ndogo ya ngozi inakuwa kidogo sana. Zipo fursa nyingi sana katika eneo hili. Nchi ya Ethiopia ni mahali pazuri pa kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya maziwa, naomba msaada ya Wizara kuendeleza zao hili Wilaya ya Mbinga. Nipo tayari kukutana nanyi ili tuwe na mpango kazi juu ya suala hili. Nataka kuinua sekta hii Wilayani Mbinga. Wafugaji wapo na wako tayari kutengeneza mtandao wao. Wanahitaji kuwa na soko la pamoja, wanahitaji kuongeza thamani na kutoa mazao mbalimbali. Nataka tuwe na kiwanda cha kusindika mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ombi hili lifikiriwe na litekelezwe. Ni ombi maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuhakikisha mazingira sawa kwa wakulima na wafugaji hasa kwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya Sekta ya Uvuvi inakwamishwa sana na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa ya Mtwara na Lindi mwambao wa bahari ya Hindi, lipo tatizo kubwa la uvuvi haramu. Katika maeneo mengi ya Mtwara, Lindi na Kilwa, Uvuvi haramu umekithiri. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali kwa ngazi ya Mikoa na Halmashauri husika, bado tatizo hilo linaendeleo kukua.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaofanya uvuvi haramu ni dhahiri pia watakuwa na mbinu nyingi za kupambana na wanaopinga uvuvi haramu. Ninashauri Wizara kuwa na operesheni kabambe za kupambana na uvuvi haramu wa mabomu katika bahari ya Hindi Mkoani Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha, wakati mwingine hata tunapokuwa katika mikusanyiko ya Kitaifa au ugeni wa Viongozi Wakuu wa Kitaifa nyakati za jioni mabomu ya baruti ya uvuvi haramu yanasikika waziwazi katika Mji wa Lindi. Ni vyema Wizara kwa makusudi ingepanga kuwa na (*speed boat*) kwa ajili ya kufanya doria katika bahari ya Hindi (Lindi na Kilwa) ambako hawana kabisa vyombo vya kuwezesha Polisi kufanya doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa rasilimali za uvuvi ni suala mtambuka kama inavyoonekana ukurasa 55, kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, na kadhalika ndizo zinazoendelea kusimamia rasilimali za uvuvi, hususan udhibiti wa uvuvi haramu. Bado kunahitajika mpango maalum wa udhibiti wa uvuvi haramu, kupangiwa mtekelezaji husika na kwa wakati maalum kuliko ilivyo sasa ambapo pengine kila aliyetajwa kuhusika na ulinzi huo anatarajia kupangwa na kundi lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendea kazi vya kuwezesha udhibiti wa uvuvi haramu katika Mkoa wa Lindi hakuna kabisa. Naishauri Serikali kuharakisha kuanzishwa kwa Kambi ndogo za ulinzi wa bahari katika Mkoa wa Lindi ambako uvuvi haramu umekithiri. Hatua hiyo iendane na kuwapatia vitendea kazi ili kuweza kupambana na hali mbaya iliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Waziri na wake katika kuendesha Wizara hii kwa ufanisi, licha ya changamoto ya *budget* ndogo.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii. Naomba kuikumbusha tena Wizara hii kwa ombi letu ndani ya Jimbo la Manyovu/Buhigwe, kufungua mnada uliopo Tarafa ya Muyama ambao wananchi wanautaka ili kuvuna mifugo waliyonayo. Mnada uliojengwa Buhigwe hautaweza kufanya kazi kama mnada uliokuwepo Muyama bila kufunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nimelifikisha ndani ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri. Naomba Wizara itoe maagizo mahususi kwa wahusika ili mnada huu uanze mara moja. La sivyo, tutashauri wananchi waanze mnada huu hata bila ridhaa maalum, kwani tunauza ng'ombe, mbuzi bila Halmashauri kupata kodi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge naomba tena na tena.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa Tanzania ina ukanda mrefu wa bahari na imejaaliwa vilevile kuwa na ushirika katika maziwa makuu matatu yaliyomo kwenye Bara la Afrika. Lakini pia kuna maziwa mengine madogo madogo mengi na mito kadhaa mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yote haya yana utajiri mkubwa wa samaki na bidhaa nyingine za majini. Kwakweli sekta ya uvuvi pekee ingeliweza kuchangia kiasi kikubwa katika pato la Taifa na pia kupunguza kwa kiasi kikubwa kabisa umaskini unaoikabili jamii ya wavuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo hapa kwetu ni kwamba Sekta ya Uvuvi haijapata msukumo wa kutosha ili iondokane na ukale na kujiingiza katika uvuvi wa kisasa wenye tija na uhifadhi wa mazingira. Kwa ujumla, uvuvi haujafanyiwa kazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika, sasa hivi kumekuwa na ongezeko kubwa sana la uhitaji wa samaki siyo Tanzania tu, bali duniani kote kunakotokana na sababu

1 JUNI, 2013

kuu mbili. Watu wengi wameanza kukimbia kula nyama nyekundu kwa vile zina kiwango kikubwa cha *cholesterol* inayosababisha magonjwa ya moyo pale inapozidi kiwango kinachohitajika mwilini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kupungua kwa samaki kwenye vyanzo vya asili vinavyozalisha samaki kama mito, maziwa, mabwawa na bahari kunakotokana na uvuvi haramu huku idadi ya watu ikiongezeka kila siku. Pia takwimu zinaonyesha kuwa sekta ya samaki inachangia kiasi kidogo sana cha 1.5% kwenye pato la Taifa kwa mwaka, wakati Uganda ni 2% na nchi nyingi za Afrika Magharibi ni 5%. Kwa kweli hicho ni kiasi kidogo sana ukilinganisha na rasilimali ya maji iliyopo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Serikali ianzishe mfuko rasmi wa kudumu wa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi zana bora na za kisasa za kuvulia, kwani itawaongezea kipato, pia mazingira yatakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali iimarisha shughuli za doria ambazo ni muhimu sana kwa ajili ya uvuvi endelevu, kwani uharibifu wa mazingira majini ni mkubwa sana. Serikali ifanye jitihada ya kutafuta wawekezaji wa viwanda vya kusindika minofu ya samaki ili kukuza ajira na kupata soko la uhakika kwa wavuvi wadogo na wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mifugo: Mnamo tarehe 30 Machi, 2011 Mheshimiwa Rais alitembelea Wizara hii na kuzungumza na viongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zake, na alisema kuwa, "anzisheni mashamba ya kunenepesha ng'ombe, tafuteni ardhi ya kutosha katika kila Mkoa kuanzia kiasi cha hekta 100 kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kuanzisha mashamba hayo." Mheshimiwa Rais alisisitiza sana uanzishwaji wa mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka mitatu sasa tangu Mheshimiwa Rais atoe agizo hili. Mpaka sasa ni lipi limefanyika? Mimi kwa maoni yangu, kama kweli

1 JUNI, 2013

yangetekelezwa aliyosema Mheshimiwa Rais, yangechochea uwekezaji katika Sekta ya Mifugo, kwa upande wa viwanda vya nyama. Watu watawekeza kukiwa na uhakika wa kupata ng'ombe wa kuchinja wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie Botswana imepata mafanikio makubwa katika mashamba ya kunenepesha ng'ombe. Botswana ina ng'ombe kiasi cha milioni 1.8 tu, na uzaji wa nyama nje ya nchi unawaingizia nchi hiyo zaidi ya Dola za Marekani milioni 20, wakati sisi Tanzania tunao ng'ombe kiasi cha milioni 20. Lakini tujiulize, tunapata pesa za kigeni kiasi gani? Inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu sasa ni wakati muafaka wa kuachana na maneno tu, twende kwenye vitendo zaidi, kwani mnasikia matatizo yaliyopo kati ya wakulima na wafugaji, migogoro inaongezeka siku hadi siku, na hii ni hatari sana! Ilianzia Bara, sasa hivi imefika mpaka Pwani. Leo Pangani – Tanga imefikia wakulima na wafugaji wanapigana! Hii siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali ifanye jitihada za haraka kuweza kuainisha maeneo ya wafugaji na wakulima kwa ajili ya kuleta amani na utulivu na shughuli za kiuchumi ziendelee vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. NASSIB S. OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi hutoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu, pia husaidia kutoa lishe bora na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa kutumia baruti, nyavu za kukokota na nyavu za macho madogo husababisha uharibifu mkubwa katika bahari zetu. Uvuvi wa aina hii

husababisha uharibifu wa matumbawe (nyumba za samaki) na kuu samaki wadogo. Lazima hatua za kudhibiti uvuvi wa aina hii udhibitiwe haraka ili kuongeza idadi ya samaki baharini. Hatua zinazofaa ni kuongeza doria ili kuwakamata wale wenye kuvua kwa kutumia mabomu, nyavu za kukokota na nyavu zenye macho madogo. Kadhalika adhabu ziongezwe, yaani ziwe kali zaidi ili kudhibiti uhalifu huu. Kama siyo hivyo, samaki watapungua sana na baadhi yao kutoweka kabisa katika miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali haijachukua hatua madhubuti kudhibiti uvuvi haramu katika bahari kuu. Bado uporaji wa samaki unafanyika katika bahari kuu. Serikali haina vyombo na zana zinazosaidia kuziona meli hizo.

Pia Serikali haina vyombo vya kuzifikia meli hizo kwa haraka kwa azma ya kuzikamata. Hivyo, uporaji huu umekuwa ukiendelea kwa kiwango kikubwa. Serikali inunue helikopta ambazo zitaweza kufanya doria katika bahari kuu. Pia inunue boti zitakazoweza kufika maeneo ya bahari kuu kwa haraka. Adhabu pia ziongezwe kwa watakaokamatwa.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya uvuvi haijapewa uzito unaofaa. Bado wavuvi wadogo wadogo hatujaliwi. Wanachomewa nyavu zao.

Pili, bajeti ni ndogo sana, huwezi kusaidia wavuvi wadogo wadogo. Je, pale wanapochomewa nyavu zao zisizofaa, kwanini hawapatiwi njia nyingine mbadala, tunawaacha wanakuwa hawana pa kushika?

Tatu, misamaha ya kodi mbalimbali ingeweza sana kusaidia kuboresha maisha yao. Kwa mfano, misamaha itolewe kwa nyavu na siyo nyuzi; na *engine* za boti ni ghali sana. Wizara ifikirie namna ya kupendekeza msamaha wa *engine* na vifaa vingine, vijana wasaidiwe kama wanavyosaidiwa wakulima kwa kupatiwa ruzuku ya pembejeo. Kuhusu tiba ya Mifugo, sisi wafugaji wadogo wadogo tunapata taabu sana pale mifugo yetu inapougua. *Private doctors* wa wanyama, gharam zao ni ghali na dawa

1 JUNI, 2013

zake pia ni ghali mno. Je, ni mkakati gani wa haraka unaoweza kutoa *solution* ya tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa makusudi isaidie wafugaji wadogo wadogo majosho ili kuinga mifugo yao. Hii ni kutokana na kuwa wafugaji hao uwezo wao ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa wananchi juu ya ufugaji wa samaki kwenye mabwawa, iko haja ya kulipa uzito suala hili, kwani litasaidia sana lishe kwa watu wetu na kunyanyua hali ya maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo yenye mifugo mingi, tuhamasishe wafugaji kutengeneza majiko ya *biogas* na mitambo yake ili ipunguze ukataji miti na kumpunguzia mama kazi kubwa ya kutafuta kuni.

MHE. DKT. KEBWE STEPHEN KEBWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu malambo/mabwawa ya maji machache. Ni vizuri Serikali iendelee na kuongeza kwa kiwango kikubwa uwepo wa malambo kwa kuchimba au kukarabati malambo yaliyokuwepo. Hii itasaidia sana kuimarisha afya ya mifugo pia itazuia kuhamahama kwa wafugaji na kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vituo vichache vya utafiti (*VTC/VIC*): Ni vizuri vituo hivi viimarishwe na ugatuaji ufanyike ili kila Kata kama ilivyo Kenya. Hii itasaidia sana uimarishaji wa afya ya mifugo katika nchi, na ufuatiliaji wa magonjwa ya mifugo katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri majosho yaongezwe kwa kujengwa ama kukarabatiwa. Hii itasaidia sana kuboresha afya ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa ugani wapatiwe nyenzo. Shukrani kwa Serikali na Wizara kwa jumla kwa kuongeza ajira ya watumishi wa ugani. Ni vyema wapewe nyenzo za usafiri, zana za kazi, mazingira ya Ofisi na makazi viimarishwe.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi ndogo ya mifugo/mazao ya mifugo (Shilingi 10,000/=) inayosafirishwa nje ya nchi, hii inapoteza fedha nyingi ambazo zingeweza kuongeza pato la Taifa. Hivyo ni vizuri kodi hiyo itazamwe upya. Kutokana na ulinzi duni wa bahari, maziwa na mito, hii imeendelea kusababisha kuwepo uvuvi haramu na umri wa samaki bila udhibiti. Ni vizuri Serikali iongeze bidii na uwezo wa kudhibiti hali hii kwa makusudi kabisa. Ni vyema kununua boti za kisasa na zenye nguvu, kuwa na mell za kisasa za doria (mfano, nyangumi), ndege za doria zikiwemo helikopta za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali kwanini haikujumuisha mifugo/uvuvi katika *“Presidential delivery Bureau”*, kwa sababu ni eneo linalogusa Watanzania wengi? Pia itasaidia sana kuboresha maisha ya Watanzania na pia kuongeza pato la Taifa? Kuhusu dhana ya Kilimo Kwanza, haijajumuisha kikamilifu mifugo/uvuvi. Ni kwanini mifugo/uvuvi havina msukumo mkubwa katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo ijitenge ili kuwa Wizara inayojitegemea. Kwa ajili ya unyeti wa mifugo na upana wake ni vyema Wizara hii ijitegemee kuliko kuchanganywa na maeneo mengine. Kutokana na kuwekwa na maeneo mengine kwa miaka mingi imedidimiza kuongeza pato la Taifa na kuboresha mifugo kwa kasi (mfano huko nyuma ilikuwa Kilimo na Mifugo, Maji na Mifugo na ikaja Mifugo na Uvuvi). Hivyo ni kudidimiza uboreshaji wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha masoko ya mifugo, masoko yaimarishwe ili kutoa ajira na kuwezesha kuinua kipato kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu juu ya matumizi bora ya ardhi iongezwe na kuimarishwa pamoja na uwezo wa malisho (*carrying capacity*) hiyo itasaidia wafugaji kuelewa nini cha kufanya kuhusu mifugo.

1 JUNI, 2013

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wengi wa vijiji hawatengi maeneo ya wafugaji, wameuza maeneo yao, naomba Waziri afanye ziara kwenye Mkoa wa Manyara ambao kwenye randama inaoneshwa Babati zimetengwa hekta 20602.10. Hii taarifa ni uwongo naomba wamwambie kwa kila Kijiji kilichopo Babati, nipatiwe kwa maandishi vinginevyo hii randama imedanganya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kuhusu Sheria ya Mipango Miji kwa zile Wilaya ambazo zimeingia kwenye Halmashauri za Miji toka Halmashauri za Vijiji, Sheria inasemaje? Wanatakiwa watenge hekta ngapi kwa kilimo Mijini na ufugaji maana hawa wataalam wa Mipango Miji wanatumia vibaya Sheria hii kwa kutokuacha hata kidogo maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara mwaka jana ilipandisha bei ya uchinjaji machinjioni, ambayo yapo chini ya Halmashauri maeneo yale ya akiba ya machinjio badala ya kulaza ng'ombe, mbuzi, wakuchinjwa kesho, yale maeneo siku hizi yamekuwa yanalimwa na wataalam wa Halmashauri, wachinjaji wameshindwa kulaza mifugo yao na hakuna maji safi ya bomba machinjioni, jambo ambalo linasababisha migogoro na migomo na wachinjaji mfano, Machinjio ya Babati Mjini, naomba hili mlifuatilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa mwongozo kutokuua mbwa kwa risasi miaka miwili sasa, ikiahidi itapeleka sumu ya kuua mbwa hawa, lakini hamjapeleka, mzigo wote mmewaachia Wizara ya Afya. Naomba majibu, hii sumu mnapeleka lini? Wananchi wengi wanaathirika na mbwa wanaozurura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya kuuzia maziwa katika Halmashauri vipo katika hali chafu, hakuna umeme wala usafiri wa kupeleka maziwa hayo sokoni, eg. Kituo cha maziwa Halla – Babati. Mheshimwa Waziri, naomba kipatiwe vitendea kazi.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wadogo wadogo kuonewa kwa maziwa kufungiwa muda mrefu, Mheshimiwa Waziri angalieni hili suala japo nia ni zuri, lakini udhibiti wake umekuwa hafifu, rushwa imetawala sana zoezi hili, watu wachache wanavua kinyemela na hawachukuliwi hatua.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya bajeti. Aidha, nimpongeze pia Naibu Waziri Ole-Nangoro kwa kazi nzuri na ngumu anayofanya. Aidha, nimpe pole Katibu Mkuu kwa kazi kubwa na ngumu, ambayo haina bajeti, ukichanganya na wataalam waliobobea ambao kwa sababu moja au nyingine, wamekata tamaa kabisa. Suala kubwa nadhani ungebuni mkakati wa kuwajengea uwezo mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo naomba kuchangia ni kuwa, katika Vyuo vya *LITI*, ada imepanda sana kutoka elfu arobaini hadi milioni moja na laki mbili. Kwa mwananchi wa kawaida hili ni ongezeko kubwa mno, naomba mwangalie uwezekano wa kupunguza ada hiyo. Kilindi ina wafugaji zaidi ya 48%, wanaomba angalau Waziri au Naibu Waziri wawatembelee, waone changamoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja na bajeti hii iongezwe.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana katika kuchangia pato la Taifa na hivyo kusaidia katika kufanikisha vita dhidi ya umaskini uliopo nchini na hasa katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie Sera za Mifugo na Uvuvi zinasemaje na hivyo kuendeleza shughuli za uzalishaji bora kibiashara ili kufanikiwa katika kuondoa umaskini kati ya Watanzania na hasa wafugaji na wavuvi husika.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta hizo, Mifugo na Uvuvi, kuna uhaba mkubwa wa Maafisa Ugani. Elimu inahitajika ya matumizi sahihi ya teknolojia ya kisasa kwa wafugaji na wavuvi katika uzalishaji wa kisasa. Vyombo vya habari na hasa redio zitumike kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa Vijijini kuboresha na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya ufugaji yanakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa majosho. Aidha, kuna baadhi ya majosho ambayo yamefungwa hayatumiki kwa ukosefu wa dawa za kuondoa/kuua kupe. Zinahitaji juhudi za makusudi kujenga majosho mapya na kufufua yale ambayo hayatumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kichaa cha mbwa, bado ni tatizo kubwa katika maeneo mengi ya nchi yetu. Siku za nyuma mbwa wenye kichaa walikuwa wakipigwa risasi na kuuawa. Kwa nini sasa mbwa wenye kichaa hawauawi na badala yake wanadungwa sindano. Ufuatiliaji uboreshwe kwani endapo kutakuwepo kutowajibika kwa kuwadunga mbwa sindano basi itakuwa ni hatari na mbwa wenye kichaa wataweza kuleta maafa kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi iangaliwe vizuri na iendelezwe. Vijana wengi waishio katika maeneo yenye kujihusisha na uvuvi wanaweza kujiajiri na kujiondoa katika makundi hatarishi yanayoweza kusababisha uvutaji wa bangi na mambo mengine kama hayo yanayoweza kuleta athari kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wawekewe utaratibu mzuri ili waweze kukopesheka kwa kujiunga katika vikundi vya uvuvi. Hivyo watafanya uvuvi wa chakula na kibiashara, wavuvi wapatiwe elimu ya madhara ya uvuvi wa mabomu na waelimishwe umuhimu wa uvuvi usiotumia mabomu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

MHE. MAGALLE J. SHIBUDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi ili nipate ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali itatoa fidia kwa wafugaji wa ng'ombe waliopokonywa na watumishi wa Wilaya za Mkoa wa Rukwa ambao sasa wapo Mkoa mmoja na Katavi.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa pametokea maovu na dhuluma nyingi za mauaji kwa mifugo katika Mikoa mbalimbali kwa kupigwa risasi na kuitwa wafugaji haramu na wahamiaji haramu ndani ya nchi yao je, Serikali inafidia gani kama ilivyoona fidia kwa wafugaji wa Kimasai.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ipo tayari kuunda Kamati shirikishi wafugaji, Wabunge na Serikali pachunguzwe uwazi na ukweli wa dhuluma na maovu yaliyotendeka?

(4) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Chama Tawala katika mkutano Mkuu wa CCM mwaka 2012, paliazimiwa kwamba hoja ya mifugo itapewa uzito maalum. Je, Serikali kupitia Wizara wana mchakato wa faida zipi za kuondoa makovu ya dhuluma ambazo ni hasira dhidi ya CCM?

(5) Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara hii baada ya kupokea maombi ya huduma za pesa kwa mahitaji ya majosho, mabwawa, sasa Serikali inanipa maelezo yapi?

(6) Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara hii ipo tayari kupitia Waziri wake tuungane twende kusikiliza vilio vya wafugaji Kanda ya Ziwa, Mikoa ya Rukwa, Katavi, Pwani na Mbeya ambako mimi ni mlezi wa hao wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu.

1 JUNI, 2013

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi kwa kuwasilisha hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara na yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya gharama kubwa ya Wizara hii ni pamoja na uagizaji wa madawa na chanjo kwa ajili ya mifugo yetu. Kwa bahati nzuri baadhi ya Watanzania wameanza kutengeneza dawa muhimu za chanjo hapa hapa nchini. Tatizo wanalolipata watengeneze madawa na chanjo, ni kodi kubwa wanayotozwa kwa kuagiza malighafi (*raw materials*) ili kutengeneza madawa hayo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba, madawa na malighafi kwa madawa ya binadamu hayatozwi kodi hizo yaani *zero rated* isitishie madawa ya mifugo yanayoingizwa kutoka nje hayatozwi kodi kubwa kama inavyofanyika kwa malighafi ya madawa ya mifugo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba malighafi za kutengeneza madawa na chanjo za mifugo zisitizwe kodi yaani (*zero rated*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi, ni sekta changa kwa pato la Taifa, lakini pia chanzo kimojawapo kikuu cha ajira nchini kama kikitazamwa kwa macho endelevu na ya ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ilivyo kwa kilimo ambapo wakulima wanapewa pembejeo pamoja na kukopeshwa pesa pamoja na kuwa na Benki ya wakulima. Ni kwa nini sasa tusiwe na Benki ya Wavuvi ambayo italenga kuwainua wavuvi kwa kuwawezesha pamoja na kuwakopesha fedha kwa ajili ya kuendeleza uvuvi nchini.

MHE. SALEH A. PAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kazi nzuri wote Wizarani, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wafanyakazi wote. Poleni kwa kufanya kazi katika mazingira magumu ya kutokuwa na Bajeti ya kutosha. Ninayo maoni yafuatayo:-

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu; simamieni uvuvi katika Bahari Kuu msisimamie utoaji wa leseni tu. Kamateni meli za Majangiri Baharini *DSFA* wajengewe uwezo. *Rub shoulders wite Japanese* wawasaidie Meli ya Doria.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ufugaji Samaki; tuwekeze katika ufugaji wa samaki wa kisasa. Tupo nyuma sana katika *aquaculture Development*. Nusu ya samaki duniani wanatoka katika ufugaji wa samaki.

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitendea kazi kwa Wavuvi Wadogo; anzisheni mfuko maalum wa kuwakopesha wavuvi wadogowadogo. Utaratibu huu uko Wizarani ya kilimo. Anzisheni *Fisheries inputs Revolving Fund*.

(4) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Mitamba Pangani; mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliahidi kutupatia kituo cha uzalishaji mitambo. Je, mpango huo umefikia wapi? Huu sasa ni mwaka wa pili, je, ahadi hiyo itatekelezwa kweli?

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuwapongeza na kuwaonea huruma kubwa sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mathayo pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wanaofanya kazi katika mazingira magumu yenye ufinyu mkubwa sana wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inataka kweli kuongeza ukuaji wa uchumi katika nchi yetu, ni vyema ikawekeza kwa dhati katika Wizarani hii.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Serikali sasa hivi kutengeneza miundombinu ya uhakika ili kusaidia katika maeneo ya wafugaji na uvuvi, ni kuwadhalilisha wafugaji, kuwaacha wafugaji wanahamama kutoka eneo moja hadi lingine badala ya kuwatengenezea miundombinu kutokana na hili la kuhamama na kusababisha migogoro isiyo na tija ambayo imesababisha vifo vya Watanzania wengi wasio na hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la ufugaji linaweza kutengeneza ajira kubwa sana hapa nchini kama itawekeza kwa kiasi kikubwa katika maeneo yafuatayo:-

(1) Kujenga Viwanda vya Kusindika Nyama; hapa ajira ya kutosha ingepatikana, pia Serikali ingepata mapato ambayo ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

(2) Viwanda vya Kusindika Ngozi; eneo hili kama litatumika vizuri litatengeneza ajira kubwa sana hapa nchini kama wenzetu wa Ethiopia walivyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikawaangalia pia wavunaji/wakulima wadogo wa ngozi kwa kuwajengea Viwanda vya Kusindika Ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la uvuvi; Serikali inatakiwa kufanya yafuatayo:-

(1) Kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwa pamoja na kuimarisha ulinzi katika maeneo ya uvuvi kusudi kusiweko na wazamiaji haramu kutoka nje.

(2) Kuanzisha Viwanda vya Kusindika Samaki ili kuongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili tungeweza kuongeza ajira na kipato kwa Serikali pamoja na wananchi walio wengi.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikaongeza bajeti katika Wizara hii ili ilete tija katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania.

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze mchango wangu wa maandishi kwa kujielekeza kwenye sekta ya uvuvi na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi hapa Tanzania imetoa nafasi kubwa kwa vijana wetu wa Tanzania kujijiri wenyewe. Hii inajionesha dhahiri umuhimu wa sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 25% ya Watanzania walio ukanda wa Pwani za Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Mafia, Kilwa, pamoja na sehemu zote za Kanda ya Ziwa Victoria wanaendesha maisha yao katika shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwa vile Serikali ina upungufu mkubwa wa ajira kwa vijana ifanye mambo yafuatayo katika sekta ya uvuvi:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, iandae Mfuko rasmi (dawati la mikopo) kwa vijana ili waweze kuendeleza maisha yao kwa kujipatia riziki ili kupunguza ukali(ugumu) wa maisha.

1 JUNI, 2013

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijiandae kupitia Wizara hii mafunzo ya uvuvi wa kisasa ili kukuza kipato katika sekta ya uvuvi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iwaandae wavuvi kiutalaam ili kuepusha uharibifu wa mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti ya Wizara; Bajeti ya Wizara haitoshi, ni ndogo, inahitaji iongezwe kwa njia yoyote, shilingi bilioni nane ni fedha ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni sekta mama kwa Watanzania kama walivyochangia Wabunge wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima fedha ziongezwe. Serikali itafute fedha kwa njia yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dira na dhamira ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ni kuhakikisha kuwa rasilimali za Mifugo na za Uvuvi zinaendelezwa na kutunzwa katika mazingira bora na endelevu kwa ajili ya matokeo bora ya ukuaji wa uchumi na kwa ajili ya uboreshaji wa maisha ya wananchi.

Sambamba na hilo ni kwa ajili ya kuhamasisha, kuwezesha na kusimamia kwa kukua kwa ufugaji wa kisasa na uvuvi endelevu, uzalishaji bora kwa wadau wa sekta ya Mifugo ili kuwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi na ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; ili dira na dhamira hii iliyowekwa isiendeleo kuonekana ghiliba kwa wadau wa sekta hii nyeti ya Mifugo. Serikali ikubali kuchukua maamuzi magumu kwa kuyapunguza baadhi ya mbuga zake

1 JUNI, 2013

za hifadhi za misitu na wanyama ili mifugo zaidi ya 85% inayotawaliwa na wafugaji wa asili waweze kupatiwa maeneo maalum ya kuendeleza mifugo yao kwa kuwapatia ardhi ya kutosha kulishia mifugo yao.

Hifadhi za Mbuga za Misitu na Mbuga za Wanyama na mapori ya akiba katika nchi yetu yana ukubwa unaozidi ukubwa wa nchi ya Uganda, hivyo Serikali ikiamua kupunguza mbuga zake za hifadhi zipatazo nne wafugaji wanaotangatanga kuhamahama hata kuuliwa ovyo kutakoma na hivyo wafugaji hawa nao wataweza kulifikia daraja la kwanza la binadamu kama lilivyo daraja la jamii nyingine ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu ukitekelezwa nchi yetu itarejesha amani inayotoroka hivi sasa siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kusema naunga mkono hoja hii. Pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na wasaidizi wao Wizarani kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Pamoja na kuunga mkono hoja, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa kisasa uhimizwe hadi sasa sehemu kubwa ya sekta hii ya mifugo inaendeshwa kijadi (*traditional livestock keeping*). Kwa hiyo, ipo changamoto ya kuibadili kutoka ufugaji wa jadi kwenda ufugaji wa kisasa wenye tija, Serikali inashauriwa kufanya uwezeshaji ufundi ili kutimiza azima hii.

(i) Watumishi wa Ugani (Maafisa Mifugo) wasambazwe kila kijiji na wapewe nyenzo za kuwafikia wafugaji na kuwapa elimu kwa vitendo wafugaji;

1 JUNI, 2013

(ii) Ng'ombe wa kienyeji wawekewe mpango wa kuwageuza kuwa chotara na baadaye wa kisasa, hivi sasa kupata mbegu wa ng'ombe wa kisasa, hivyo vijijini ni shida kubwa; na

(iii) Huduma za madawa ya mifugo ziboreshwe kwa kuwa ni bei nafuu na zipatikane kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipango ya kuboresha malisho na maji; utaratibu mbaya wa ufugaji wa kuhama hama utakomeshwa tu pale ambapo, Serikali itawawezesha wafugaji kupata maeneo ya uhakika wa malisho na mabwawa madogo madogo ya kunywesha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulazima wa huduma za majosho; hivi sasa kazi ya ujenzi wa majosho imeachiwa wananchi wenyewe na Halmashauri zao, Serikali inashauriwa iwe na mpango wa kusaidia Halmashauri katika ujenzi wa mabwawa.

Kilio cha Wabunge kuhusu udogo wa bajeti wa Wizara hii unalenga kupata ongezeko la fedha ili kazi ya majosho ifanyike, pia uchimbaji wa malambo kwa ajili ya maji ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji mdogo mdogo wa samaki hili ni eneo ambalo tupo nyuma sana, lakini likifanyiwa kazi linaweza kuinua kipato cha wananchi. Naishauri Wizara kutoa elimu ya kutosha kuhusu ufugaji wa samaki, wataalam wa kuelekeza waje vijijini na vifaranga vya samaki iwe rahisi kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema naunga mkono hoja hii.

1 JUNI, 2013

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tu niwarejeshe kwenye *Order Papers* zetu za leo, lakini hasa hasa niwarejeshe kwenye maagizo ya Mheshimiwa Naibu Spika jana, wakati akitoa Mwongozo na Utaratibu wa kuendesha shughuli za Bunge leo ndani ya Bunge. Hoja hii iliyoko hapa mbele yetu ya Mifugo na Uvuvi, inatulazimu tuimalize saa Tano, na tutakapomaliza hoja hiyo saa Tano tutaendelea na ile hoja nyingine ambayo tulikuwa tumeiahirisha. Sasa baada ya kupata Mwongozo wa Katibu, ninaomba sasa niite Serikali ianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu tutamalizia na Waziri na tutaendelea na utaratibu wa Kikanuni kama ulivyoainishwa kwenye Kanuni.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia hoja kwa iliyopo mbele yetu. Ninaomba tu uniruhusu nitamke mwanzoni kwamba, naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, imeeleza kwa undani kabisa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/2013, na kubainisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Pamoja na Mikakati tuliyoandaa kama Wizara na Mipango ya Serikali katika kutekeleza Bajeti inayoombwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea na kwa maandishi, wote kwa pamoja wametoa mawazo mazuri na muhimu sana katika kuleta mapinduzi katika sekta ya Mifugo na sekta ya Uvuvi, michango ya Waheshimiwa Wabunge imebainisha umuhimu wa sekta hizi mbili muhimu, kwa maana ya sekta ya Mifugo na ya Uvuvi. Mifugo na Uvuvi ni sekta mbili muhimu sana, katika ajira ya watu wetu mijini na vijijini, uhakika wa chakula la lishe bora, ustawi wa watu wetu ambao ni wafugaji, wavuvi, na wadau wa sekta hizi mbili za ufugaji na ya uvuvi.

1 JUNI, 2013

Fursa zilizopo katika sekta hizi mbili zinafunikwa zaidi na migogoro hasa ile ya uvuvi haramu, uharamia ulikuwepo katika Bahari ya Hindi na wizi wa rasilimali za uvuvi katika Bahari kuu na katika maji ya Kitaifa. Kwa upande wa Mifugo, fursa zilizopo katika hii muhimu, mara nyingine zinafunikwa na migogoro hasa ile kati ya wafugaji na wakulima. Si rahisi kunufaika na fursa hizi hadi tutakapowezekeza kikamilifu katika sekta hizi zote mbili Mifugo na Uvuvi.

Hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwa muda tulio nao si rahisi kuzijibu zote, lakini tumepokea michango mingi, mizuri, na kwa sababu ya muda, hoja ambazo hatuwezi kuzijibu hapa, tutazijibu kwa maandishi.

Wabunge waliochangia hoja iliyoko mbele yetu, jumla ni Wabunge 86, maana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu walichangia Waheshimiwa 23. Hoja za Wizara nyingine mbalimbali, hasa Ardhi, Maji na Kilimo, kuna Wabunge 13 waliochangia na katika siku ya jana, kuna Wabunge 19 waliochangia kwa kuongea na Wabunge 31 wamechangia kwa maandishi. Hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge ni hoja 74, maana Kamati ya kisekta imeibua hoja tisa za msingi, Kambi ya Upinzani hoja 16 na Wabunge hoja 28 na zile zilizoibuliwa katika hotuba ya Waziri Mkuu na Wizara mbalimbali jumla ni 21. Kwa hiyo, jumla ya hoja zote zinakuja kuwa ni hoja kama nilivyosema 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nianze kwa kujibu hoja zilizochangiwa na Wabunge pamoja na Kamati ya kisekta na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Nitaanza na suala zima la migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji, hili limechangiwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Kamati ya kisekta imeeleza umuhimu wa kushughulikia suala hili, na Wabunge wengine wengi, akiwemo Mheshimiwa Lekule Laizer, Opolukwa, Sakaya, Kilufi, Makilagi, Kakoso. Hawa na wengine wengi ambao kwa sababu ya muda sitataja majina ya wote, lakini kwa kweli wameongelea suala hili na wakaongelea kwa uchungu mkubwa. *(Makofi)*

1 JUNI, 2013

Niseme ni ukweli usiofichika kwamba migogoro hii itaisha tu pale tutakapomudu kupima maeneo yote, kuyatenga maeneo haya ya malisho, kilimo, makazi, maeneo ya huduma na ya hifadhi. Lakini pia baada ya kuyatenga yanahitaji kubainishwa, uhakiki wa maeneo haya uweze kufanyika, lakini kama Wabunge wengi walivyochangia, haitoshi kubaisha. Maeneo haya yanapaswa kuendelezwa kwa kuwekwa Miundombinu hasa ya maji, majosho, lakini huduma nyingize za jamii, zikiwemo Shule, Zahanati na huduma nyingine muhimu.

Maana wafugaji ni watu, na tunapaswa kutazama katika mkakati huu, si mahitaji ya mifugo tu kama mifugo, bali pia watu wanaofuga hii mifugo. Maana kusipokuwepo na huduma hizi muhimu katika maeneo haya, watafanya kama inavyofanyika sasa, watarudi katika vituo vyenye huduma na hapo migogoro inayoanza. Serikali imefanya jitihada nyingi kama tulivyosikia mara nyingi, kwamba katika Halmashauri 69, kwenye Mikoa 21 taratibu hizi zimefanyika na Wizara ya Ardhi, kwa kutumia pia Tume ya Mipango bora ya Ardhi, imefanya jitihada nyingi, na hata kuna takwimu kwamba ni maeneo mangapi yamebainishwa, kwa maana ya *hectors*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki unaendelea na unapaswa kuimarishwa zaidi, uendelezaji wa maeneo haya kama nilivyosema, lakini pia kuna haja ya kuwa na mkakati na wa haraka zaidi, na hii Wizara imeandaa kwamba na sheria ndogo ndogo zitatungwa ili kuhakikisha kwamba maeneo haya yatatumika kwa makusudi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayokuwepo, ni kwamba hili ni eneo linalowahusiha wadau wengi na hata tukitazama *mandate*, kama Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, sisi ni watumiaji wa ardhi, lakini inapokuja katika kupima, kupanga, hii imo kwenye Wizara ya Ardhi, lakini likija kwenye usimamizi, hili linakwenda TAMISEMI zaidi, kwa maana ya muundo tulio nao katika vijiji vyetu na katika Halmashauri na mwishoni hata katika ngazi ya kitaifa.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Wabunge kadhaa wametoa pendekezo tuliloanza na sisi kujadili kama Wizara, kwamba huenda kwa sababu ya ukubwa wa tatizo hili na umuhimu wa shughuli hii kufanyika, huenda kuna haja ya kuwa na wakala ambao muundo wake utafanana na ule wa *TANROADS*, uanze ku-*operate* kusimamia shughuli hizi kotoka ngazi ya Taifa kuteremka katika ngazi ya ya Halmashauri, kwenda kwenye Kata na kwenye Vijiji, kusudi nguvu na jitihada zinazofanyika na Halmashauri zetu hizi ziweze kuongezewa nguvu, kwa maana ya kuwa na watu wengine wataokuwa wanasimamia shughuli hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liginine lililoongelewa na Waheshimiwa Wabunge ni haja ya kuwa na mashamba ya kuzalisha mifugo bora, ikiwemo kuwa na vituo maalum vya mitamba, vituo vitakavyokuwa vinazalisha na kukuza na kuwapatia wafugaji na wakulima mitamba bora kwa ajili ya maziwa.

Mheshimiwa Silvestry F. Koka ameongelea hili, Ignas Malocha, Mheshimiwa Saleh A. Pamba na Wabunge wengine, hasa katika Kamati pia ya Kisekta na Kambi ya Upinzani, pamoja na Wabunge wengine wengi.

Niseme tayari vituo vingi vipo na Wizara imekuwwa na hivi vituo, lakini kuna jitihada pia ya kupeleka katika Kanda na kuhakikisha kwamba vituo hivi vitasaidia pia kufika hata katika ngazi ya maeneo waliko wafugaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari katika Mkoa wa Tanga, kuna umoja wa Tanga *Dairy Corporative Union*, na huu umejipanga vizuri, kuna mwingine wa Shilda na Asasi nyingine pamoja na *Health Project Tanzania*, hawa wamekuwa nao wakizalisha mitamba na Taasisi hizi zimezalisha jumla ya mitamba 9,741 ambazo zimeuzwa na kusambazwa kwa wafugaji wengi katika maeneo mengi.

Mashamba yanayosimamiwa na Wizara pia yamezalisha na kusambaza mitamba 1,303, lakini kwa uhakika tunaona haja ya hii sekta hasa ya maziwa kuwekewa

1 JUNI, 2013

mkazo zaidi na rasilimali zikipatikana, mikakati iliyopo itaendelezwa ikiwemo pamoja na ile iliyoongelewa na Waheshimiwa kama Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Diana Chilolo, lakini pia Gaudence Kayambo, Martha Mlata, Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha hawa, hawa wameongelea sana kwa maana ya viwanda vya kusindika maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya maziwa, Serikali imeondoa kodi zote kwa sasa ipo *zero rating*, na hii ni sababu ya kuhakikisha kwamba vifaa vile hasa vifungashio na vyombo vingine vya kubebea maziwa pamoja na mitambo yake, hii iweze kupatikana kwa urahisi zaidi bila kodi, ili moja kuleta na kuunda mazingira ya ushindani, lakini pia kuhakikisha kwamba ubora wa bidhaa utazingatiwa katika kuendeleza sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Waheshimiwa wengine hasa Rose Kamili, akiongea kwa niaba ya kambi ya upinzani, pamoja na Wabunge wengine, wameongelea sana suala la kuimarisha na kuboresha zaidi Bodi yetu ya maziwa. Niseme tu kwa sasa mafunzo yametolewa kwa watumishi tisa, na tayari kama Wizara, Bodi imepata idhini ya kuajiri watumishi wengine tisa, ili kuhakikisha kwamba Bodi itakuwa na uwezo. Moja ya kufanya kazi yake ya kuratibu, lakini pia ile ya *Regulation*, kusimamia sheria na sera na kuhakikisha kwamba viwango vinavyohitajika vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine, Wabunge wengine akiwepo Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, wameongelea muundo wa Wizara na kueleza kinagaubaga haja na hitaji la sekta ya mifugo kama Wizara, kusimama ikajitegemea bila kuwa na sekta nyingine.

Niseme tu kwamba Serikali itatazama haya, lakini tayari tuna Wizara nyingi na hatuna uhakika kama ni rahisi

1 JUNI, 2013

kwa mara moja kuongeza Wizara maana kila unapoongeza Wizara, gharama hasa zile za *overhead costs* zinaongezeka, na kumbe tungependa zaidi rasilimali nyingi ziende kwa walengwa zaidi kuliko kutumika katika ngazi ya juu, ngazi ya Wizara na ngazi ya usimamizi.

Wabunge wameongelea katika sekta ya uvuvi suala zima la Bandari ya Uvuvi, na hii wote tunaona haja, kama Wizara tumekuwa tunaongea na tuna mipango, *Concept note* na *Proposals* zimeandikwa, lakini rasilimali kutoka katika sekta ya binafsi hazijapatikana na katika upande wa Serikali bado jitihada zinafanyika kutafuta namna ya kuwa na kujenga Bandari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba Bandari inapojengwa, tunakubaliana na Wabunge waliochangia, kwamba usimamizi utaboreka, udhibiti utaboreka, na tukitazama tu hali halisi sasa, asilimia 71 ya mazao ya uvuvi inatoka wa kweli katika Ziwa Victoria, na sababu si kwamba Victoria ina Samaki zaidi kuliko Bahari kuu, bali ni kwa sababu ya Miundombinu iliyowekwa pale, Mialo 28 iliyojengwa kwa msaada wa fedha kutoka *European Union* hasa baada ya kuwa Sangara wamepatikana pale.

Tulipowekeza tunaona matunda kwamba ni wazi kwamba uzalishaji umeongezeka kwa kiasi kikubwa sana, na tunakazania kama mipango inavyosema, kuona jinsi ya kujenga Bandari hii, ili kuhakikisha kwamba Meli za kigeni zinapokuja kuna mahala zinafikia kupata leseni, waende wavue, wanaporudi pia uhakiki ufanyike na kuhakikisha kwamba walichopewa leseni, ndiyo hicho hicho walichovua, hawakuzidisha kama huenda inavyofanyika sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wameongelea pia tena kwa uchungu mkubwa suala zima la kuhakikisha kwamba vyuo vyetu vya mifugo na vile vya uvuvi vinapanuliwa, viwe na uwezo zaidi, ili kusudi kuwaandaa watalam wengi zaidi na kuhakikisha kwamba Wagani katika sekta ya uvuvi na katika sekta ya mifugo wanakuwepo wa kutosheleza vijijini.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni hitaji lisilofichika, lakini tayari udahili umeongezeka, japo si kwa kiasi tunachohitaji, udahili umeongezeka katika sekta ya mifugo, lakini pia katika sekta ya uvuvi, lakini jitihada zinafanyika ili tupanue zaidi na pengo kubwa lililopo la wagani katika sekta hizi mbili liweze kujibiwa.

Mheshimiwa Gregory G. Teu, Mbunge wa Mpwapwa, alikuja na hoja ama ombi la kuomba kwamba *LIT* ya Mpwapwa ipandishwe ama iunganishwe na *Sokoine University of Agriculture*. Angalau kwa sasa Wizara haina mpango wa kufanya hivyo, tunachojibidisha kufanya ni kuona kama rasilimali zitapatikana za kupanua kwanza Chuo hiki, kubaresha kwa maana ya miundombinu, lakini pia na taaluma, wawe na walimu wa kutosha na baadaye itakapofikia hadhi ya kuonekana kwamba kuna haja ya kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha *SUA*, hatutakuwa na ubishi wa kufanya hilo, lakini angalau hii itachukua muda zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengine wengi wameongelea suala zima akiwemo Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, ameongelea suala la malisho. Maeneo yaliyogeuzwa na kuwa *WMAs*, na mfano wa eneo la Monduli, la Lokisale, Makuyuni, Naiti na Mswakini pia. Kwamba hatma ya wafugaji ni nini, baada ya eneo hili kutangazwa kuwa ni *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuna changamoto. Changamoto yenyewe ni dhana inayotumika katika kuhifadhi. Kwa sababu eneo hili *WMA*, zilianzishwa ili kuhakikisha kwamba Mamlaka yanatoka zaidi katika Idara ya Wanyamapori na kwenda katika ngazi ya vijiji kwa usimamizi na Matunzo ya Wanyama wanaokuwa katika Ardhi ya Vijiji. Sheria haina mgogoro. Nionavyo mimi tatizo linakuja katika dhana ya Uhifadhi.

1 JUNI, 2013

Kwa sababu dhana hii zaidi ni ile ya kizamani ya kuwa na picha ya *Wild Waist* na kwamba Hifadhi lazima isiwe na matumizi mengine, isiwe na watu wengine. Lakini nadhani dhana hii imeanza kubadilika na mkazo siku hizi kwenye *new thinking* kwenye Uhifadhi, zaidi inatazama suala moja la mkamilishano kati ya Watumiaji kadha wa rasilimali hizo, na kwa uhakika mifugo na wanyama pori, hawa wanakamilishana, kuna ko-*complementarit* kati ya Wanyama na Mifungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niseme pia taaluma za Ki-Ecolojia siku hizi zinasema mkamilishano huu kuna jani na mimea mwitu ambayo wanyama porini hawatumii mifugo inatumia. Kuna mimea ambayo mifugo inatumia, wanyama pori hawatumii. Kwa hiyo nadhani ni budi tuanze kutazama dhana hizi na kuhakikisha kwamba mawazo haya pamoja na wanachogundua watalaam wa Ecolojia kwamba tunazingatia lakini kubwa tuende kwa muelekeo wa sasa ambao badala ya kutotumia kuwa dhana ya Uhifadhi ni kutumia Rasilimali kwa busara, na nadhani hapa hakuna tishio kwa Wanyama pori na hakutakuwepo na tishio kwa upande pia wa Wakazi karibu na maeneo haya, hasa wale wanaofuga.

Nimseme tu hatima nadhani ni taratibu zifanyike, ili wenye maeneo haya ambavyo ni vijiji ulivyotaja Mheshimi Rose Kamili Sukum, kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wahakikishe kwamba sheria ile inafuatwa, tartibu zifuatwe. Na kuhakikisha kwamba Rasilimali hizi zitakuwa *managed* kwa taratibu ambazo hazikinzi na kimsingi hazikinzi kama zitatazamwa kwa ukaribu wake.

Umeongelea suala la Loliondo. Ambalo pia ni sehemu ya hii migogoro na migongano. Kwa hili niseme tu tayari ujumbe wa watu wengi kutoka Loliondo, walikuja walimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa hili liko kwenye mikono ya Mtendaji Mkuu wa Serikali, tuliache na tuvute subira nina uhakika kwamba Serikali itatoa maelekezo ambayo yatazingatia haya yaliyo ibuliwa na yale ambayo wenyeji wa Loliondo na wao wamekuwa wakiongelea.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya Uvuvi, kuna Wajumbe kuna waliohoji suala zima la Meli ile ya Tairikwana ambayo imeshikwa, ama Meli ya Mheshimiwa Dr. Magufuli, samaki wa Magufuli, na kwamba nini imeachwa. Hukumu ilitolewa, lakini baada ya hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu, Rufaa ilikatwa na wale waliopatikana na hatia na kwa sababu hiyo suala hili halijaisha Mahakamani, Meili haikukabidhiwa katika Wizara yetu, na hivyo bado ilibaki kwa sababu ilikuwa ni sehemu ya ushahidi wa kesi hii.

Kwa hili huenda tutajifunza kutokana na mfano huo. Lakini niseme tu kwamba imebidi ibaki kwenye mikono ya vyombo husika kwa sababu ilikuwa ni sehemu ya *exhibit* katika uendeshaji wa kesi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoongelewa na Waheshimiwa Wabunge ni Elimu kwa Wafugaji. Na hii niseme tu tayari vyuo vyetu, mbali ya kuwa na hizi kozi za shahda na stashahda. Vimekuwa pia vinatoa mafunzo ya muda mfupi, na mafunzo haya yameandaliwa zaidi kulenga mazingira ya wafugaji wetu, wavuvi wetu ili kuhakikisha kwamba wanauelewa mpana wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninashukuru. Nitamke tena kwamba ninaunga mkono hoja. Waziri ataendelea na hoja zilizozobakia, lakini pia tutatoa majibu yetu kwa maandishi kwa sababu hatukuweza *cover* yote kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Naibu Waziri katika kutoa utangulizi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge. Ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Waziri ambaye ni mtoa hoja ili na yeye atumie dakika zilizobaki kujibu hoja za Wabunge.

1 JUNI, 2013

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii, kukushukuru wewe binafsi kunipa nafasi hii. Pili ni Mshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana wa Wataalah*, Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele yenu Waheshimiwa Wabunge kujibu hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Makamu Mwenyekiti, Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati wa Sekta ya Kilimo Mifugo na Maji, kwa mara nyingine kwa michango yao yenye lengo la kuboresha Sekta ya Mifugo na Uvuvi ili hatimaye iweze kuongeza kipato cha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ninaomba kumshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii kwa michango yake mizuri. Yale mazuri tutayachukua na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa pekee napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika Wizara yangu hii, kwa kuzungumza na kwa maandishi. Vile vile wapo waliochangia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge ni mizuri na ni mingi, ambayo nina imani kabisa kuwa itatusaidia katika kuboresha utendaji kazi katika Wizara yetu.

Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye amemaliza kuchangia hivi karibuni. Kwa michango yake mizuri na ufafanuzi alioutoa kwa baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya waliochangia wameshatajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, nisingelipenda kupoteza muda. Lakini niseme tu kwamba wale ambao hoja zao hazitajibiwa tutatoa majibu hayo kwa maandishi.

1 JUNI, 2013

Baada yamaelezo hayo mafupi, sasa napenda kuanza kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza katika Bajeti hii. (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze kwamba sisi Wizara yetu fedha ambazo tulikuwa tumeomba tangu awali kwamba zingelitotosha zilikuwa ni Shilingi Bilioni 163. Shilingi Bilioni 163.

Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti, tumepatiwa Shilingi Bilioni 47.18. Hata hivyo katika suala hili la ufinyu wa Bajeti. Napenda kusema kwamba hoja ya Waheshimiwa Wabunge ni ya msingi na Serikali imeielewa.

Serikali tunawaomba waipe muda kidogo na jibu lake litakuja kabla ya kupitisha Bajeti yote ya Serikali, kwa sababu *Appropriary Bill* inakuja kwa hiyo masuala hayo tutayazunguma. Lakini Serikali imeona kuna msingi huo, imesikia na imeona. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ninawaomba kwamba tupitisha Bajeti hii, lakini tuvute subira kusudi kabla ya Bajeti kuu ya Serikali haijapitishwa basi tutakuwa tumeishajua kwamba tunafika katika hatua gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zingine ambazo zilisababisha Bajeti hii kupungua, kuonekana kwamba imepungua, kulinganisha na mwaka 2012. Ni kwamba kuna *component* moja ya *ASDP Program* ya kuendeleza Sekta ya Kilimo. *Program* hii imekwisha. *Program* hii wakati ipo mwaka 2012 tulifikisha Shilingi Bilioni 53. Lakini *program* hii imekwisha. Kwa hiyo, ndiyo maana hata fedha zake zile zimepungua kwenye Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna *programme* ya MASEM. *Program* ya MASEM nayo imeisha mwezi Februari, 2013. Nayo ilikuwa inaongezea fedha kwenye Bajeti ya Wizara hii. Hizi *program* mbili kubwa kwisha kwake kumepunguza kwa kiasi kikubwa fedha za Bajeti hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nipende pia kusema kwamba kama mnavyoelewa Waheshimiwa Wabunge, miundombinu ya Mifugo kwa maana ya Majosho, Malambo, Minada midogo, yote hii inasimamiwa na Halmashauri za Wilaya. Wao ndiyo wenye jukumu la kusimamia maeneo haya na hata fedha zinapotengwa zinakwenda moja kwa moja kwenye Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu 2013/2014 TAMISEMI, imetengewa Shilingi Billioni 5.3, ambazo zote zinaenda kwenye sekta ya Mifugo na Uvuvi. Fedha hizi haziko kwenye Wizara yangu lakini zinaongezea huduma katika sekta hii ya Mifugo na Uvuvi baada ya kutengwa kwenye TAMISEMI.

Vile vile zipo Shilingi Milioni 350 ambazo zimetengwa Wizara ya Ardhi, kwa ajili ya Kamisheni ya Matumizi Bora ya Ardhi, kwa ajili ya kuendeleza zoezi letu la kupima maeneo kwa ajili ya wafujgaji na kwa ajili ya watumiaji wengine wa ardhi. Ninakiri kwamba kasi ya upimaji ni ndogo. Kasi ya upimaji wa maeneo haya ni ndogo, lakini utengaji na uwainishaji wa maeneo haya utatokana hasa na upatikanaji wa fedha kwenye Bajeti za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni ile ya kwamba Mifugo inapo hama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine inasababisha kusambaa kwa magonjwa. Ni kweli hilo tunalielewa lakini Serikali nayo ina *program* zake, kuhama kwa mifugo ni kitu ambacho hakizuiliki. Kwa sababu zipo taratibu za kuhamisha mifugo kihalali tu. Kwa hiyo ni kitu ambacho hakizuiliki.

Lakini Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali inazo *programme* za kukabiliiana na magonjwa hayo, zikiwemo *programme* ya kutoa chanjo kwa magonjwa kama vile homa za mapafu yaani (CBPP). Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, *foot and mouth disease*. Yaani ugonjwa wa midogo na miguu. Hasa na *program* hii pia inatekelezwa katika nchi za SADAC.

1 JUNI, 2013

Vile vile, chanjo inatolewa kwa ajili ya ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo na vile vile kuna *program* ya kuzuia ugonjwa wa kichaa cha mbwa ambayo inaratibiwa na Shirika la Afya Ulimwenguni, ikiwemo Taasisi ya *Bill and Melinda Gates Foundation*, kwenye Halmashauri 16 za Tanzania Bara pamoja na eneo la Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutopatkana kwa mikopo ya kutosha na yenye mashariti nafuu kwa shughuli za ufugaji na uvuvi na gharama za pembejeo na zana za ufugaji na uvuvi. Katika Kanda ya Ziwa, kwanza Serikali imefuta kodi ya ongezeko la dhamani yaani VAT. Kwa nyavu, imefuta VAT kwenye *engine* za boti. Imefutwa VAT kwenye nyuzi za kushonea nyavu. Vile vile imefuta VAT katika vifungashio kuanzia mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na makubaliano ya Soko la Pamoja la Afrika Mashiriki, ushuru wa malighafi, zana za uvuvi na viambata vyake, zimefunguzwa au kufutiwa kodi la ongezeko la dhamani. Serikali imekuwa ikiwezesha Wavuvi wadogo kupitia *program* mbali mbali hususa *MASEMP*, iliyokuwa inatekelezwa na wavuvi waliweza kupata kwa ujumla Shilingi Bilioni 1,303,950,355/= zilizotolewa kama Ruzuku kwa ajili ya kuwezesha wavuvi. Ambapo jumla ya Miradi 125 ya uzalishaji ilitekelezwa kuanzia mwaka 2006 mpaka mwaka 2013 yaani mpaka mwaka huu mwezi Februari, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhaba wa Maofisa Ugani, kwa maana ya mifugo na uvuvi. Mahitaji ya Wagani, wale ambao ndio wanaotegemewa na Wavuvi pamoja na Wafugaji wetu. Mahitaji yake ni 17,325 kwa maana ya Wagani wa Mifugo. Wagani wa Uvuvi ni 16,000 nchi nzima kwenye ngazi za vijiji, ngazi za Kata, ngazi za Tarafa.

Katika mwaka 2013/2014, Serikali itaajiri wataalam 2,500 kwa sekta hizi za sekta ya Mifugo na Uvuvi, na vijana hawa wako tayari kwa sababu tumeishawasomewa na wataajiriwa mwaka huu.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukosefu wa Mbegu Bora za Mifugo na Samaki. Pembejeo na Huduma Hafifu za Uhamilishaji: Kutokana na watumiaji wa huduma za Uhamilishaji kulalamikia huduma hiyo inayotolewa Wizara ilifanya tathmini na kufikia maamuzi yautayo:-

(i) Kituo cha Uhamilishaji kifanyiwe ukarabati na kupatiwa vifaa vipya vya kisasa ili kiweze kuongeza ufanisi katika kuzalisha mbegu bora na za kutosha.

(ii) Kusambaza huduma za uhamilishaji kupitia vituo vya Kanda vya Uhamilishaji na vituo vidogo, ili viwe karibu na watumiaji kwa lengo la kupunguza gharama za kuboresha uhifadhi na kulinda ubora wa mbegu hizo. Jumla ya vituo vya Kanda vya uhamilishaji vipo vitano na vituo vingine vidogo viwili vimeanzishwa ili kukidhi huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaranga vya Samaki huzalishwa kwenye Vituo vya Ufugaji wa Samaki, kule Kingolwira Morogoro. Ruhira kule Ruvuma. Vituo hivi ni vichache kulingana na ukubwa wa nchi na ongezeko la mahitaji. Wizara kwa kuliona hili imeanzisha vituo vya Mwamampuli, Kituo cha Chato na Kigoma na kuimarisha vilivyopo kwa lengo kuongeza uzalishaji. Aidha Sekta binafsi zimehamasishwa na zimeanza kuonyesha mwelekeo wa kuzalisha vifaranga vya samaki, aina ya perege na Kambale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukosefu wa Soko la Uhakika la Mazao ya Mifugo na Uvuvi na hasa katika maeneo ya vijijini. Minada ya Upili, *Secondary Market* na ya Mipakani inaendelea kuimarishwa. Minada ya Upili iko 12 nchini na Minada ile ya Mipakani ya Mifugo iko 10. Machinjio za kuchinja na kuchakata na kusindika nyama ziko 11 kwa maana ya ng'ombe, mbuzi na nguruwe. Lakini zipo nyingine ndogo ambazo zinashughulikia kuku.

Machinjio hizi zimejengwa katika Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Morogoro, Pwani Arusha, Rukwa Iringa na Mbeya. Minada ya awali 369 inaendeshwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika maeneo ya vijiji kuna maeneo

maalum. Yaani Mialo, au Bandari kwa ajili ya kupokelea na kuuzia samaki, ambapo wafanya biashara na wachuuzi hukusanya kwa ajili ya ununuzi wa samaki. Serikali inashauri Serikali za vijiji zibainishe maeneo maalum kwa ajili ya kupokelea samaki, ili kuwarahisishia wafanyabiashara na wachuuzi mbali mbali kujua wapi soko la samaki lilipo. Serikali inaendelea kuboresha mialo, bandari ili kuongeza ubora na usalama wa mazao ya uvuvi wakati huo huo, kuwa na soko la uhakika na kwa bidhaa za uvuvi na mazao yake vijijini. Mfano imejenga mialo katika maeneo ya Masoko Pwani Kilindoni pamoja na Nyamisati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni ushiriki mdogo wa wadau katika kudhibiti uvuvi haramu na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi. Wizara kwa kushirikianana Halmashauri imewezesha kuanzishwa kwa vikundi shirikishi wa rasilimali, yaani *Beach Management Units* 20 na kuvifanya *BMUs*. Hivi vikundi hivi sasa hivi vimeishafikia 739. Aidha *BMUs* zimesajiwa na nane kuwezesha kutunga sheria ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu duni ya ufugaji bora na ufugaji usio wa kibiashara na matumizi duni ya teknolojia za kisasa kwa wafugaji. Wizara imeandaa miongozo ya wafugaji na uvuvi ambayo inatumiwa na Halmashauri kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi kupitia mipango ya kuendeleza kilimo kwenye Wilaya yaani *DADPs*. Elimu hiyo inatolewa kupitia Sabasaba na Nanenane, siku ya uvuvi duniani, wiki ya Maziwa, siku ya Vetinari duniani, siku ya Maziwa shuleni na duniani, siku ya chakula duniani, mashamba darasa na kupitia vyombo vya habari. Elimu pia hutolewa juu ya ufugaji bora na wa kibiashara na matumizi ya teknolojia za kisasa kwa wafugaji kila mwaka kufuatia vyo vyetu vya wafugaji yaani *NFTCs* na vyo vya mafunzo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imeshazungumzwa vizuri na Mheshimiwa Naibu Waziri nisingependa kurudia tena.

1 JUNI, 2013

Lakini maeneo ambayo yanapimwa kwa ajili ya matumizi ya mifugo na matumizi ya watumiaji wengine wa ardhi yanapimwa na Wizara, kiongozi wetu wa kupima maeneo haya ni Wizara ya Ardhi na hata takwimu tunazozisoma hapa zimethibishwa na Wizara ya Ardhi ambao ndiyo wapimaji.

Sisi ni wadau huwajulisha kwamba eneo hili linafaa kwa mifugo na eneo hili halifai kwa mifugo lakini wao hasa ndiyo wanaopima maeneo yale, tunachowaomba ni kwamba waongeze kasi ili wafugaji wetu maana sisi ndiyo watumiaji wa maeneo hayo, basi waongeze kasi ili tuwe na maeneo ya kutosha wafugaji wetu wasipate shida ya kuhamahama.

Lakini vilevile, tunawaambia Halmashauri waongeze kasi pia ya kuweka miundombinu ya mifugo katika maeneo ambayo yametengwa ili wafugaji wasihamame kwenda kutafuta malisho na maji kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapori na maeneo ya hifadhi yatengwe kwa wafugaji. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Kasulumbayi, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Shibuda, wote wamelizungumza hili. Lakini niseme tu kwamba hoja hii kwanza mimi nilishaanza kuzungumza na Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Waziri wa Ardhi.

Ili tuweze kweli kuliangalia hili suala vizuri panapokuwa na uwezekano, kama kuna mapori ambayo tunaweza tukasema yanabadilishwa matumizi kidogo kwa maeneo ambayo yamezidiwa sana kwa kweli hili lingesaidia sana wafugaji wetu maana maeneo Wilaya nyingi ambazo zimepakana na mapori yaliyohifadhiwa pamoja na hifadhi za Taifa, Wilaya nyingi ambazo zipo katika mazingira hayo zimebanwa sana kwa sababu unakuta hifadhi hizi ni zamani hata kabla hatujapata uhuru na wakati tunapata uhuru tulikuwa Watanzania milioni tisa lakini sasa hivi tupo milioni 45.

Ni dhahiri kwamba mahitaji ya ardhi yameongezeka. Sasa ni lazima tuangalie vilevile kwamba pamojana kuacha maeneo haya kwa ajili ya vizazi vijavyo kama tulivyokuwa tunasema wakati tunapata uhuru nadhani vizazi vijavyo vimeshakuja tayari kwa hiyo baadhi ya maeneo tunaweza tukaongea kimsingi kabisa kwamba jamani hebu tujali kidogo mifugo yetu hii inayoitwa Ng'ombe, Mbuzi, Kondoo na kadhalika, wakati mwingine labda tuipunguzie Pundamilia kidogo maeneo yaani tupunguze kidogo pale kwenye Pundamilia ili na mifugo yetu pia iweze kupata, ni suala ambalo tumeshaanza kuzungumza sasa tutajua kwamba linaishia wapi. Lakini ni vema kuliangalia hilo ili Watanzani wafugaji na hata wakulima waweze kupata maeneo kwa sababu maeneo yamekuwa madogo, Watanzania wamekuwa wengi na mifugo nayo imekuwa mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itamke viwango vya faini zinazotakiwa kutozwa kisheria kwa Ng'ombe, Mbuzi au Kondoo wanapoingia kwenye hifadhi. Viwango vinavyototzwa hutegemea sheria inayotumika na aina ya hifadhi iliyoingiliwa. Kwa mfano, sheria ya misitu namba 14 ya mwaka 2002 imeweka kiwango cha chilingi 30,000/= kwa siku. Aidha, sheria namba saba ya mwaka 2007 inazipa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutunga sheria ndogondogo kwa mifugo inapoingia katika hifadhi na Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua yenyewe imeweka kiwango cha shilingi 20,000/=, hii ni mifano. Kwa hiyo, viwango vinatofautiana.

Lakini kuingia tu Ofisa wa Hifadhi anaingia anakuta Ng'ombe halafu anasema kwamba toa shilingi milioni 10 au 15 huo ni wizi, ni wizi ama unakuta Ng'ombe wapo ndani ya Hifadhi ama kwenye mapori ya asili halafu unawapiga risasi kwanza huo siyo ubinadamu na ni kosa kubwa ambalo kwa kweli tunalifanyia kazi na baadhi ya majina tunayo, wanachunguzwa na watakapobainika watachukuliwa hatua kali na tutahakikisha hayo majina tuliyonayo ya Maafisa Wanyamapori ambao wanapiga risasi mifugo wakati sheria zipo wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria tena hatua kali. Kwanza ni dhambi na unavunja Sheria ya Ustawi wa Mifugo Namba 19 ya Mwaka 2010. (*Makofi*)

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi katika Bahari Kuu kuwezesha wazawa. Kusema kweli tunachokifanya ni kuhamasisha wenye viwanda kutengeneza boti zinazoweza kufika kwenye maji mengi. Lakini vilevile Wizara yangu inaweza vitu vinavyoitwa *FADs* yaani *Fish Aggregating Devices*, hivi ni vitu ambavyo unaviweka baharini halafu Samaki wanajikusanya kwenye vyombo hivyo kwa hiyo inakuwa ni rahisi kuvua Samaki kwa sababu wamejikusanya sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa pia inafanya doria za anga na kwenye maji, niseme doria hizi zinafanywa mchana na hazifanywi usiku. Kuna Mheshimiwa mmoja alizungumza kwamba zinafanywa usiku, hazifanywi usiku bali zinafanywa mchana na hasa zinafanywa asubuhi na jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeweka chombo kinachoita *Versal Monitoring Device au System* ambayo ni rahisi kuona meli inayovua kwenye maji yetu ndiyo maana mnasikia wakati mwingine meli fulani imeripotwa, imeonekana au inachunguzwa, hii ni kutokana na vitu hivi ambavyo tumeviweka.

Kujenga uwezo wa wavuvi katika bahari kuu walete mazao yanayovuliwa nchini badala ya kupelekwa moja kwa moja nje. Ni kweli kwamba hili litawezekana vizuri kiurahisi na tumeshaanza taratibu za kujenga bandari ya uvuvi, tunapokuwa na bandari ya uvuvi ambayo ina *facillities* basi ni rahisi meli kuja na kushusha Samaki na wale Samaki ambao walikamatwa ambao hawana soko nje basi wanatumika humuhumu ndani ya nchi na wanasaidia watu wetu na watu wengi wangepata ajira. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ni kuwa na bandari ya uvuvi na taratibu hizo tumezianza.

Kuhusu uvuvi haramu na wavuvi haramu ni wangapi wamehukumiwa wangapi? Mwaka 2012/2013 kulikuwa na kesi za uvuvi 23, kati ya kesi hizo nane zimetolewa hukumu na wahalifu wanatumikia kifungo, jela na kesi 15 kwa sasa zinaendelea Mahakamani.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuteketeza zana haramu, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamesema kwa nini tunawanyang'anya halafu tunaziteketeza halafu hatuwapi *replacement*. Wavuvi wanajua kipi kizuri na kipi kibaya, wanajua nyavu zipi nzuri na zipi mbaya, sisi wenyewe tumekwenda huko tumeangalia tumekuta wavuvi wameficha zile nzuri wameziweka kwenye maboti yao hawazitumii halafu zile nyingine ambazo ni mbovu zenye matundu madogo au macho madogo wamezificha porini kwa sababu wanajua kwamba tunakuja kukagua.

Kwa maana hiyo, wanajua nyavu nzuri na wanajua nyavu ambazo si nzuri haziruhusiwi na uteketezaji wa zana haramu za uvuvi ni kutokana na maamuzi ya Mahakama kuzichoma moto nyavu zote na kuziangamiza na hii inatokana na sheria Namba 22 ya uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 ambapo mtu haruhusiwi kuhodhi wala kumiliki ama kuvua kwa kutumia nyavu hizi ambazo haziruhusiwi.

Si dhamira ya Serikali kufidia mtu yeyote anayevunja sheria, huwezi kuwa nyavu mbovu halafu ukategemea kwamba ufidiwe maana wakati mwingine wanazo nyavu nzuri halafu wanapitisha uzi katikati ili kupunguza matundu, sasa mtu kama huyo ukimkuta umpe nyavu nyingine nzuri kwanza ataiharibu tena kwa kupunguza matundu lakini pia atakuwa anajua anachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Maafisa Ugani nilishalizingumza. Vyuvo vya mafunzo viongeze udahili, ni kweli kwamba ili tuweze kupata maafisa ugani wa kutosha ni lazima tuongeze udahili. Katika kukabiliana na upungufu wa Maafisa Ugani Wizara imeongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya Uvuvi hadi kufikia 943 toka mia tatuna ushee. Sasa hivi wako 943 kwa mwaka, ikilinganishwa na mwaka jana walikuwa 700 na mwaka juzi walikuwa chini ya 400. Katika vyuo vya mifugo kutoka wanafunzi 300 mpaka sasa hivi ni 1,720 kwa mwaka, ikiwa ni pamoja na kuongeza vyuo vya Umma na Binafsi.

1 JUNI, 2013

Pia wanafunzi hawa wanafundishwa elimu ya kujajiri kwamba hata ambao hawatapata ajira basi wanaweza wakajajiri yaani ajira ya Serikali basi wanaweza wakajajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu kwa wafugaji na wavuvi. Wizara imeandaa miongozo ya ufugaji na uvuvi bora ambayo kwa kweli inatumwa na Halmashauri kutoa elimu kwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo yaani *DADPs* kwenye Halmashauri zetu. Elimu hizo pia zinatolewa katika maadhimisho ya Nanenane, siku ya uvuvi duniani, wiki ya Maziwa, siku ya Vetinari duniani, siku ya Maziwa mashuleni duniani na siku ya chakula duniani pamoja na mashamba darasa kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

Malisho na miundombinu ya mifugo, idadi ya mashamba yaliyopo ya kuzalisha mbegu. Hili ni eneo muhimu sana, Wizara ina mashamba nane ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Vikuge Kibaha, Langwira Mbeya, Kizota Dodoma, Mabuki Mwanza, *Sao Hill* Iringa, Mivumoni Tanga, Talili Tanga na Tariri Kongwa.

Mashamba haya ni muhimu kuzalisha mbegu na sasa hivi tunataka tuhakikishe kwamba yanazalisha mbegu zaidi kusudi tuweze kuanzisha mashamba makubwa ya *pasture* kwenye maeneo ya wafugaji na kwenye Halmashauri ili kusudi wafugaji waweze kupata lishe ya mifugo yao ili waweze kupunguza kuhamahama sambamba na kujenga miundombinu mingine. Mashamba haya nane niliyoyataja yana uwezo wa kuzalisha tani za mbegu 300 kwa mwaka ambazo ni mbegu nyingi sana tu ambazo zinaweza zikatusaidia kwa kiasi kikubwa. Lakini sekta binafsi huzalisha wastani wa marobota 513,000 ya hey kwa mwaka. (*Makoff*)

Suala la ujenzi wa malambo nimeshalizungumzia lakini lambo zuri kubwa ambalo linafaa kwa mifugo ni kati ya kuanzia shilingi milioni 100 ndiyo unaweza ukapata lambo zuri kabisa la kuweza kusaidia mifugo.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na ukarabati wa minada, malambo na majosho nchini. Kama nilivyosema hapo awali ujenzi na ukarabati wa Majosho na malambo unatekelezwa kupitia *DADPS* au *SACP* pamoja na sekta binafsi, kutokana na dhana ya ugatujaji wa madaraka.

Wizara haijengi malambo moja kwa moja bali wanaojenga malambo moja kwa moja ni Halmashauri kupitia *DACP* au *DADPs* lakini sisi tunachokifanya ni kukagua kama malambo yale yanajengwa kwa viwango, kama malambo yanajengwa kwa viwango na kama maeneo wanayojenga yanastahili kujengwa malambo yaani tunaangalia ubora wa miundombinu ile.

Lakini Wilaya ndizo ambazo kulekule tunakotoka kwenye Halmashauri ndiyo maeneo ambayo tunatakiwa tuulize fedha zilizokuja kwa ajili ya ujenzi wa malambo ni ngapi na mwaka huu nimesema bilioni tano zimekwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013 minada ya upili miwili, malambo 25 na majosho 14 mapya yamejengwa na minada ya upili saba pamoja na malambo tisa na majosho 20 yamekarabatiwa kupitia fedha za *DADPs* yaani fedha hizo ambazo zinapitia Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo Wizara inashughulikia moja kwa moja ni *ASDP Livestock Component*, ni fedha ambazo zinatolewa na Serikali ya Ubelgiji na zinasaidia katika Wilaya nne tu yaani Wilaya ya Chamwino, Wilaya ya Kiteto, Wilaya ya Bahi na Wilaya ya Kondoa na fedha zake ni shilingi billioni 8.5 na kwa sababu hivi zimebaki shilingi bilioni 2.9 na ndiyo ambazo kwenye Bajeti ya Maendeleo mtaziona zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ambayo Wizara inatekeleza ni pamoja na mpango wa kuendeleza tija na uzalishaji ya Afrika Mashariki yaani *East Africa Agricultural Productivity Program*.

1 JUNI, 2013

Hii inasimamiwa na Wizara moja kwa moja. Lakini vilevile kuna magonjwa ya mlipuko ambayo yanasambaa kwenye nchi za *SADC* yaani *SADC parts*, magonjwa haya pia yanasimamiwa na Wizara moja kwa moja. *Program* ya kudhibiti kichaa cha Mbwa ambayo nimesema kwamba ipo kwenye Halmashauri 16 Bara na Pemba na yenyewe inasimamiwa na Wizara moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Albert Obama amezungumzia ufunguzi wa mnada ulipo Tarafa ya Muyama. Wizara inaendelea kuwasiliana na Halmashauri kuona uwezekano wa kutumia mnada wa Buhigwe kwa sababu minada hii ipo karibu. Kama tutaona hakuna uwezekano huo basi tutaruhusu ufunguzi na tutaruhusu Halmashauri ifungue mnada katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rebecca Mngodo amezungumzia suala la kutoua mbwa kwa kutumia risasi. Ni kweli siku hizi kuna nyingine za kuuu Mbwa wale ambao wanaonekana wana magonjwa kwa maana ya magonjwa ya kuambukiza kwa binadamu kwa mfano, *Rabies* au kichaa cha Mbwa wanatumia njia nyingine ya kuuu badala ya kutumia risasi kwa sababu risasi ni hatari pia kwa usalama wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ruzuku ya madawa ya mifugo. Serikali inatoa ruzuku ya dawa hususani kwa magonjwa ya mlipuko na kwa magonjwa yasiyokuwa na mipaka. Magonjwa ya mlipuko na magonjwa yasiyokuwa na mipaka Serikali inachangia 40% na wafugaji wanachangia 60% ya gharama za kuogesha mifugo, madawa haya yanatolewa kama ruzuku 40% na mfugaji anachangia 60%.

Lakini ugonjwa wa mapafu ya Ng'ombe, homa ya mapafu ya Ng'ombe Serikali inagharamia kwa 100% na hadi sasa shilingi bilioni 16.8 zimetolewa kununulia lita milioni 1.1 na kusambazwa kwa wafugaji.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dawa za mifugo kuwa ghali; kwa sasa Serikali imeacha kutoza kodi nyingi katika dawa za kutibu mifugo. Hata hivyo, ughali wa dawa hizo unatokana na ghalama halisi za utengenezaji wa dawa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuchelewa kwa Machinjo ya kisasa ya Ruvu; ujenzi ulitakiwa ukamilike mwaka 2011, lakini ulisimama kwa muda kutokana na kuchelewa kukamilika kwa michoro na hivyo kulazimu *NARCO* kuvunja mkataba na mkandarasi ambaye alikuwa ni SUMA JKT. Kampuni hiyo kwa sasa imetangaza zabuni na kumpata mshauri mwelekezi wa kusimamia ujenzi na hatimaye kupata mkandarasi mpya, ambapo Benki ya Rasilimali (*TIB*), imekubali kugharamia Mradi huo kwa kutoa Dola za Marekani milioni tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tuna machinjio yafuatayo: Kwanza tuna machinjio ya hapa Dodoma, *Tanzania Meat Company*, ambayo ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 200, mbuzi na kondoo 200, ambayo inamilikiwa na *NICO* pamoja na *NARCO*. Kule Arusha tuna machinjio inaitwa Sakina, ambayo ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 300, kondoo na mbuzi 400, inamilikiwa na Manispaa ya Arusha.

Tanzania Pride ambayo iko Morogoro, ilikuwa iko kwenye mufilisi, lakini sasa hivi tuna kampuni inaitwa TENDAJI, wanakarabati ili waweze kuanza uchinjaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SAAFI* kule Sumbawanga ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 150 na wanyama wadogo, kwa maana ya kondoo na mbuzi 150. Kwa sasa hivi inachinja kwa oda na uzalishaji wake kidogo umepungua.

ORPU ambayo kwa sasa imefungwa iko Simanjiro ilikuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 40 na kondoo na mbuzi 40. Kwa sasa hivi imefungwa kutokana na ushindani pamoja na gharama za uendeshaji.

Manyara Ranchi haijakamilika, bado wanatafuta

mwekezaji ili aweze kusaidia. Ruvu ambayo nimesema tuko kwenye *process* ya kupata mshauri mwelekezi wa kutoa michoro ili ujenzi uanze, fedha zimeshapatikana dola milioni tisa kutoka Benki ya Rasilimali.

Triple S kule Shinyanga wanaendelea na ukarabati. Mbeya na Mbalizi kule *CHC* imeshatangaza kwa mwekezaji ambaye ana uwezo wa kufanya hivyo na majina matatu yamepatikana wanayapitia. Kama watakuwa wame- *qualify* watapewa kazi, kama watakuwa hawaja- *qualify* mwaka kesho tutaomba fedha ili Wizara ianze kushughulikia machinjio haya ya Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Iringa na Mbeya, Halmashauri kwa kushirikiana na *UNIDO*, wanajenga machinjio ambayo yatakuwa tayari hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna machinjio kubwa kule Shinyanga inajengwa na Wachina, ambayo kwa sasa hivi ujenzi wake umefikia asilimia 50.

Pia kuna *Mkuza Chicks* ambao wanachinja kuku 8,000 kwa siku, *Interchicks* wanachinja kuku 3,000 na kule Mkuranga kuna machinjio inaitwa *Tande N Farms*, wao wanachinja nguruwe 1,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na programu ya kuanzisha mashamba ya kunenepesha. Ranchi za *NARCO* kule Kagera, tunapima upya na tutaanza na Ranchi ya Kaboma, baadhi ya vitalu tuhakikishe kwamba, tukimaliza hiyo tunaenda ranchi nyingine yenye matatizo zaidi, kama ni Misenyi au wapi, ilimradi tuhakikishe kwamba mambo yanakwenda vizuri, kusiwe na migogoro ya ardhi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo zitolewe kwa ajili ya ufugaji wa samaki. Hilo litatokana na upatikanaji wa fedha, lakini shilingi milioni 50 zilitolewa kwa ajili ya kuimarisha vituo vyetu vya uzalishaji wa vifaranga vya samaki hususan kule Kingolwira, Luhira, Karanga, Musoma,

1 JUNI, 2013

Nyamirembe, Bukoba, Mwampuli kule Igunga pamoja na Mtama kule Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufugaji wa samaki hutolewa kwa Wananchi kwa njia ya ugani na kupitia Halmashauri zetu. Taasisi zisizo za kiserikali pia zinafanya kazi hiyo na *TAFIRI* nayo inatusaidia katika kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wasaidiwe kuuza samaki kwa bei nzuri. Mimi nadhani suala kubwa hapa ni kuwa na ushirika. Tulishawahamasisha na wameshaanza taratibu zao hasa katika Ziwa Victoria kuwa na ushirika wenye nguvu ili waweze ku-*negotiate* vizuri na wawe na mikataba ambayo inapitiwa pia na Serikali ili kuona kwamba, wavuvi wanauza samaki wao moja kwa moja viwandani badala ya kupitia kwa mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu na sensa za mifugo zinafanyika namna gani? Zinafanyika kwa njia tatu; kwanza, sensa kamili kwa maana ya kuhesabu mifugo; pili, kuna *routine administration data system* ambayo hukusanywa na maafisa wa mifugo katika ngazi za vijiji, wilaya na mikoa; na tatu, kuna sensa au *surveys* ambazo hufanyika kila baada ya miaka mitano au mwaka mmoja wakati tunafanya kampeni ya chanjo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wametaka kujua ni fedha kiasi gani ambazo tunaokoa kwa kutoagiza mazao ya uvuvi na mifugo kutoka nje. Napenda kusema kwamba, kwa kutoagiza mazao ya samaki tuna-*save* zaidi ya shilingi trilioni tatu na kwa kutoagiza mazao ambayo yanatokana na mifugo tuna- *save* zaidi ya shilingi trilioni 15. Hapo ndipo tuone kwamba, mifugo na uvuvi inachangia sana kwa kiasi kikubwa katika ku-*save* fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi, kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa wawekezaji wa kati na wakubwa. Serikali imeondoa kodi, nimeshazungumza kuhusiana na kodi mbalimbali ambazo zimeondolewa

1 JUNI, 2013

kwenye zana za kuvulia na tutaendelea kuangalia mengine ambayo yatawezekana hususan kuondoa *road toll* kwenye mafuta ambayo yanakwenda kuvulia samaki, kwa sababu kule hakuna barabara, ili waweze kupata faida na wahamasike kwenda kuvua samaki kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba, yapo yaliyobaki ambayo tutayaandikia vizuri. Kwa sababu muda umeisha na kengele ya kwanza imeshapigwa, nisingependa nipigiwe ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Naomba sasa nimwite Katibu kwa hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 99 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

Kif 1001 - *Administration and HR*

Management Sh. 3,489,772,000

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Waziri Mathayo, Mshahara unakamatwa!

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taratibu na Kanuni zetu za Bunge, nimepokea wachangiaji wafuatao kutoka katika vyama mbalimbali kupitia kwa *Whips* wao; Chama cha *CUF* atapewa ruhusa Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, CHADEMA Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, CCM Mheshimiwa Mtutura Adallah Mtutura, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda na Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda. Kama muda utaruhusu nimeona sura nyingine, basi

1 JUNI, 2013

ninaweza kuzipa nafasi, lakini kwa mujibu wa kanuni hao ndiyo watakaopata nafasi ya kuzungumza kwenye mshahara huu wa Waziri.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi kwa ufupi tu ninasema, dhamira yangu bado iko palepale, iwapo sitapata ufafanuzi wa kutosha utakaoniridhisha mimi pamoja na Bunge hili, nitaondoa shilingi.

Katika mchango wangu wa jana nilizungumzia kuhusu kasoro ya bajeti hii kwamba ni ndogo ukilinganisha na sekta mbili pamoja, yaani mifugo na uvuvi. Nilizungumzia pia matatizo ya mifugo kuanzia majosho, ukosefu wa maji, *research centers*, *vaccination* na mambo mengi tu ambayo Wabunge wengi wameyaelezea hapa. Nikaelezea pia upande wa Sekta ya Uvuvi kwamba, hatujawa *serious* kwani kuna vifaa ambavyo vinahitajika ili kudhibiti uvuvi haramu katika Bahari Kuu. Vifaa kama vile ndege angalau moja, *speed boat*, *fishing ports* na kuwawezesha hata vijana kuwa na boti wakaweza kuvua katika Ukanda wa Pwani kuanzia Tanga, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai Mheshimiwa Waziri kutoa kauli hapa kwamba, kuna mchakato na ndiyo maneno ambayo tunayatumia mara nyingi, bajeti itakapokuja kusomwa kutaongezwa fedha fulani. Hata hivyo, kauli hii nisingependa itolewe na Waziri kwa sababu yeye anaomba hizi fedha kuendesha Wizara yake, hiyo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kwamba, tulipitisha Bajeti ya Wizara ya Maji hapa na Kamati ya Bajeti ikaenda ikakaa na ikaleta *amendments*. Sasa ninachotaka kukielezea ni kwamba, hatutaki mali kauli, tunataka *written documents* kwamba, *amendments* zipo atapata hizi fedha. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tujali muda. Haileti picha nzuri sana Mheshimiwa Mbunge unakatizwa unapoongea kwa sababu ya kukiuka kanuni za uongaji ndani ya Bunge.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Hivi karibuni tumeanzisha, hatuwezi kuita ni sera, lakini ni kaulimbiu kwamba, tutakuwa na KILIMO KWANZA na hiki kinatumia ardhi. Hawa wenzetu wa mifugo nao pia wanatumia ardhi. Vilevile Serikali iliamua kwa makusudi kabisa kwamba, mifugo ambayo imetoka Ihefu, imetoka Kilombero, ipelekwe Mkoa wa Lindi. Sisi kwa kuelewa kwamba, mifugo ni jambo muhimu, tulipoombwa katika Wilaya mbalimbali za nchi yetu, tulikubali kutenga baadhi ya maeneo. Natoa tu mfano, Jimbo la Tunduru, tulitoa Kata tatu ambazo ni Masonya, Muwesi na Ngapu.

Kitu cha kushangaza ni kwamba, hawa ndugu zetu wanapofika Tunduru wanatawanyika karibu Wilaya nzima. Jambo hili linatoa simanzi sana kwa wakulima kwa sababu mara nyingine hata ukienda katika maeneo mengine ya nchi yetu, hawa wenzetu wakishalisha mashamba ya wakulima na wakifikishwa kwenye Vyombo vya Dola, wakitozwa faini, kesho mifugo ile yote inakwenda kwenye shamba lile wakiwa wanadai wameshalipia. Jambo hili linaleta mapigano katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Je, Serikali inatoa tamko gani ili kuepusha mapigano katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kwa kutenga maeneo na kusisitiza, yale maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wafugaji yaendeleo kuwa hivyo ili wafugaji ambao wanakwenda maeneo ambayo hayajatengwa waweze kuondolewa kwa nguvu za Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba ufafanuzi wa Serikali juu ya jambo hili.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba na mimi pia niseme kwamba, nitashika shilingi kwenye mshahara wa Waziri, pamoja na kwamba, jana nilisema nitakutoa moja kwa moja tutatoka wote.

Mheshimiwa Waziri, amejibu swali kuhusu suala la kutenga ardhi kwamba, wanaohusika ni Wizara ya Ardhi na mimi nakubaliana naye, lakini hakushirikiana na Wizara ya

Ardhi, kwa sababu zile fedha zilizotengwa shilingi milioni 350, zinahusiana na Wilaya nne ambazo ni Newala, Tarime, Rorya na Maswa. Wilaya ambayo ina migogoro sugu ya ufugaji haikutengewa fedha na ninamlaumu Mheshimiwa Waziri kwamba, hakushirikiana na hiyo Wizara. Nataka Waziri akijibu aniambie je, atashirikiana na Wizara ya Ardhi kutatua migogoro iliyopo Kilombero, Rufiji, Chunya, Handeni na katika Wilaya zote ambazo zina migogoro ya ardhi kwa ajili ya wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atujibu hilo na kama hataweza mimi nitashika shilingi, kwa sababu wafugaji wa asili hawana maeneo kabisa hata kwenye bajeti yake hawakutengewa chochote. Naomba majibu.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, wanaozungumzia sera wananifurahisha, kwa sababu hawarudii rudii hoja. Kwa hiyo, atakayerudia rudia hataruhusiwa kuendelea na hoja yake. Mheshimiwa Mponda!

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sera ya Taifa ya Mifugo ya 2006 na Mpango Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo 2011, nimeiangalia kwa undani sana, lakini sijaona kabisa ni namna gani inaelekeza kutatua tatizo la ughali wa bei ya dawa na chanjo za mifugo. Imewaachia moja kwa moja wafugaji, bila hata huruma, wao kivyao vyao ndiyo wagharamie mifugo hiyo. Wakati katika upande wa pili wa kilimo, Serikali wametoa ruzuku ya pembejeo na mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ni namna gani Wizara inaweza ikachukua mkakati huo wa ruzuku ya pembejeo na mbolea kwa wakulima. Vilevile mtoe ruzuku ya dawa na chanjo za mifugo kwa wafugaji ili baadaye iende sambamba na kile ambacho wamekieleza katika mikakati ya Sekta ya Mifugo wanayosema wanalenga kwamba, ifikapo 2016 mnataka Sekta hii ikue kufikia asilimia 4.5 kutoka asilimia 3.1 ya mwaka 2011. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Waziri majibu, aah, bado Mheshimiwa Mtanda, samahani Mheshimiwa Waziri.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunikumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijielekeza kupambana sana na wavuvi haramu, lakini pia wakati ikiendesha zoezi hili na kuwasumbua kwa kiasi kikubwa sana wavuvi wa maeneo mbalimbali wa Kanda hizi za Pwani hasa kutoka kule Kilwa, Mchinga mpaka Mtwara, ilikuwa ikiwaahidi wavuvi wa maeneo hayo kuacha uvuvi haramu na badala yake wawezeshwe kufanya shughuli mbadala ambazo zitawaingizia kipato, jambo ambalo halijafanywa hadi leo hii.

Nilikuwa nataka kupata majibu kutoka kwa Serikali ni lini sasa wavuvi wa maeneo hayo watapata fursa ya kujiwezesha na kupata vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuendeleza zoezi hili la uvuvi? Pia nyavu hizi haramu ambazo Serikali imekuwa ikipambana na wavuvi hawa ndugu zetu zinatengenezwa na viwanda mbalimbali ndani na nje ya nchi ni hatua zipi sasa Serikali inachukua, hatuoni mapambano dhidi ya viwanda hivyo badala yake tunaona mapambano dhidi ya wavuvi. Tulitaka kufahamu kutoka Serikalini ni namna gani sasa wavuvi hawa watawezesha ili kuachana na suala hili la uvuvi haramu?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, kama anaanza Naibu Waziri ama unajibu yote wewe mwenyewe.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika suala alilouliza Mheshimiwa Sanya kwamba, dhamira yake ipo palepale kuondoa shilingi na anachosema ni hoja ambayo imezungumzwa sana na Wabunge wengi kwamba, bajeti inastahili kuongezwa. Nadhani harakati zimeanza za kujaribu kuzungumza namna ya kuongeza bajeti. Wavuvi kama alivyosema, ametoa ushauri mzuri kwa upande wa kutafuta ndege tena yenye vifaa vya kisasa na boti ili uvuvi haramu

1 JUNI, 2013

uweze kudhibitiwa na kuhakikisha kwamba, mazao yetu yanavunwa na wale ambao wamepewa leseni na watakachovuna ni kiasi kilekile walichopewa leseni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa anachokizungumza Mheshimiwa Sanya, uzito wa *commitment* ya Serikali katika kuona haja ya kuongeza bajeti hii siyo kuendelea na masuala ya kutafakari. *Commitment* hasa ya Serikali kwenye jambo hili ni nini; ndiyo hoja ya msingi hapa?

Nakushukuru sana Kaimu Kiongozi wa Serikali Bungeni, kwa niaba ya Waziri Mkuu, tunaomba *commitment* ya Serikali katika jambo hili na si haya tu ya kutafakari, kushauriana. Kaimu Kiongozi wa Serikali Bungeni, Mheshimiwa Sitta!

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI – KAIMU KIONGOZI WA SERIKALI BUNGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwa kusema kwamba, Bunge lako Tukufu litambue Serikali inathamini sana michango na ushauri mzito unapotolewa na Bunge hili. Kwenye hii Sekta ya Mifugo, jana tumepata darasa, maelezo yamekuwa mazuri, watu wamezungumza kwa dhati hata leo Mheshimiwa Sanya alivyosema, anawakilisha vizuri mawazo ya wafugaji na wavuvi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu na mimi jimboni kwangu kuna wafugaji na pia tuna mabwawa ya wavuvi. Sasa nataka niwachukue ili mjue Serikali inavyofanya kazi, niwachukue nyuma ya pazia kuwaelezeni nini kilitokea jana baada ya maelekezo ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais yuko Tokyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko Marrakesh Morocco. Hata hivyo, jana tulimwagiza Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya, afanye kazi ya awali usiku ule kuangalia maeneo ambayo yanaweza kujengewa hoja kupunguzwa ili kukidhi lile ambalo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu wanahitaji.

Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, kazi hiyo amelifanya, nadhani nusu ya kukesha. Alivyojitahidi amefikia fikia kama kiasi cha bilioni 20, lakini hii haikidhi haja ya wanachokisema Wabunge. Kwa hiyo, nimewasiliana na Viongozi Wakuu na jibu ni kwamba, sasa hivi kuanzia tarehe 7, Ijumaa ijayo, kutakuwa na zile siku sita za Serikali kujadiliana na Kamati ya Bajeti. Kufikia tarehe hiyo, ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nadhani aliyapata kutoka Tokyo na niwafahamishe tu, Marrakesh Morocco ni saa tatu nyuma ya Tanzania, Tokyo ni saa sita mbele ya *time* ya Tanzania, lakini bado usiku huo tumeifanya hii kazi mpaka kufikia haya ninayoyaeleza kwamba, hoja imekubalika. Kiwango tulichojitahidi kukipata sisi ambao tunashikilia hizi nafasi, mimi na Mheshimiwa Mkuya, kilipofikia ishirini bado hakijatoshia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa na niseme tu kuanzia mwanzo, tuliweza kupata fedha kwa ajili ya ziada ya Wizara ya Maji, kwa sababu katika hatua hiyo, bado ilikuwa inawezekana kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Kwa hiyo, tumekwenda na tumeongeza katika Wizara nyingine pia. Sasa hapa tulipofika, tunakaribia kwenye mfupa, ile minofu yote imekwisha. Kwa hiyo, maamuzi yanapokufikisha kwenye mfupa maana yake ni hivi; inabidi Wizara fulani shughuli zake zipunguzwe kabisa, hakuna tena hii ya kusema labda upunguze chai; hapana, hayo yamekwisha. Sasa ni kupunguza kwenye baadhi ya sekta, uamuzi kama huo unamhitaji Mheshimiwa Rais mwenyewe na kwa hakika itabidi kwa uzoefu wangu, kutakuwa na Baraza la Mawaziri, kabla ya ile *Budget Committee*. Kwa hiyo, nimewachukua myaone yote hayo yaliyofanyika jana katika kujaribu kufikia lengo la kile ambacho tumeshauriwa na Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokuomba sasa na nawaomba Wabunge wenzangu, mtuachie taratibu hizi zifanyike zikamilike, kwa vyovyote vile kile kitakachoongezeka na natumaini itawezekana kifike hapo ambapo Waheshimiwa Wabunge wanatushauri, basi kitaonekana kwenye *Appropriation Bill* na kwa hiyo, tunapopitisha

1 JUNI, 2013

makadirio ya mwaka huu, eneo hili la mifugo litakuwa limepata kile ambacho linahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nadhani nichukue nafasi hii, kumshukuru sana Kaimu Kiongozi wa Serikali ndani ya Bunge, kwa maelekezo na mwongozo huo alioutoa. Sasa naomba turudi kwa Mheshimiwa Waziri, aendelee kwanza kujibu maswali yaliyopita ili niweze kupata nafasi ya kuhoji katika haya mafungu na hoja za kisera zilizotolewa. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Sitta, kwa kuniondolea gunia la chumvi kichwani.

Mheshimiwa Mtutura ameulizia maeneo yaliyokuwa yametengwa kwa mifugo yaendelee kuwa maeneo ya mifugo; ndivyo ninavyosema mimi kwamba, maadamu maeneo yametengwa na Halmashauri na yakaainishwa kwamba haya ni ya mifugo, yabaki na yaendelee kuwa maeneo ya mifugo. Kama kuna wakulima wanaingilia maeneo hayo na wao wanafanya makosa. Maeneo hayo ambayo yameshatengwa na kuainishwa na vyombo hivyo vilivyowekwa kisheria, yaendelee kubaki ya mifugo na vilevile yale ya wakulima yaliyoainishwa kwa ajili ya kilimo yasiingiliwe yabaki kuendelea ya kilimo ili kuepusha matatizo na mapigano ya hapa na pale.

Naziomba Halmashauri nchini ziendelee pamoja na kwamba, Wizara ya Ardhi inasaidia kupima maeneo, lakini Halmashauri nazo zisaidie katika kutenga fedha za kupima maeneo ili tuweze kuhakikisha kwamba, wafugaji wetu na wao wanapata maeneo sambamba na wakulima walivyo na maeneo. *Otherwise*, wasipofanyiwa hivyo ni lazima matatizo yataendelea na migogoro itaendelea. Lazima tuone kwamba hili ni tatizo kwa sisi sote.

Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, ushirikishwaji huu upo

siku zote na utaendelea kuwepo, lakini kwa sababu umeniambia niseme, basi nasema nitashirikiana nao. Siyo kwamba, nilikuwa sishirikiani nao ila nimesema kwa sababu umeniambia niseme nisisitize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mponda, amezungumzia suala la gharama ya madawa ya mifugo kwamba, kule kwenye kilimo kuna ruzuku, kwa nini huku kwenye mifugo hakuna ruzuku. Kwenye mifugo kwanza kuna magonjwa haya ambayo yanasababishwa na virusi, magonjwa ambayo yanakuja kwa milipuko kwa mfano Homa ya Bonde la Ufa, Serikali inatoa ruzuku kwa ajili ya chanjo, tena siyo ruzuku ni kwamba, inachanja moja kwa moja kwa asilimia mia moja, pamoja na Ugonjwa wa Mapafu wa Ng'ombe (*CDPP*). Serikali inatoa asilimia mia moja kuchanja mifugo. Sotoka ya Mbuzi na Kondoo, Serikali inatoa asilimia mia moja ya kuchanja. Kichaa cha Mbwa, Serikali inatoa asilimia mia moja ya kuchanja.

Vilevile nimesema kwamba, kuna Halmashauri 16 pamoja na Pemba, ambazo sasa hivi programu hiyo inaendelea kwa ajili ya kuchanja kichaa cha mbwa. Ugonjwa wa miguu na midomo, Serikali inatoa asilimia mia moja ya chanjo.

Serikali mwaka huu ambao tunaamalizia hivi sasa, ilitoa shilingi bilioni moja na nusu, kwa ajili ya madawa ya kuogesha mifugo kuzuia magonjwa kama ndigana kali na kadhalika.

Mheshimiwa Mtanda, amezungumzia ahadi ya Serikali ya kuhakikisha kwamba, wavuvi wale wanawezeshwa kufanya shughuli nyingine badala ya kuji-*involve* kwenye uvuvi haramu. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mtanda na umekuwa unalifuatilia hili suala kwa ukaribu kabisa. Ninachokuahidi, baada ya bajeti hii tutakutana ili tuweze kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukawasaidia wale vijana wako na Wananchi wako katika Jimbo lako.

1 JUNI, 2013

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naona mna wasiwasi. Namheshimu sana Mzee wangu, ndugu yangu, Kiongozi wangu na ndiyo Mtendaji kwa sasa hivi ndani ya Bunge, Mheshimiwa Sitta, kwa kauli yake nzuri aliyoitoa na iwe kauli na ahadi ya kweli, kwa sababu amechukua ahadi mbele ya Bunge na kama ni Mhimili muhimu wa kuboresha haya maendeleo. Zaidi, amenikuna pale aliposema kwamba, zitazidi zaidi ya shilingi bilioni 20, tunazisubiri kwa hamu na tuko pamoja na Wizara hii na sasa hivi Mheshimiwa Waziri anaweza akarudi kwa bodaboda.

MWENYEKITI: Kwa hiyo umerudisha shilingi? Mheshimiwa Rose Kamili Sukum!

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana Mheshimiwa Waziri kunijibu kama kitu laini sana. Suala la wafugaji wa asili nimekuomba kwamba, unaposhirikiana na hao na umejibu kwamba utashirikiana na Wizara ya Ardhi, lakini hujatamka kwamba utaonesha maeneo yapi ili waweze kutengewa hawa wafugaji. Wewe mwenyewe ulitamka kwenye hotuba yako kwamba, kazi yenu ni kuonesha Wizara ya Ardhi maeneo ya malisho. Sasa ni maeneo yapi ambayo unayaonesha kwa ajili ya malisho na Mheshimiwa Waziri uelewe kwamba hizi fedha zikitengwa pia zitaelekea kwa hao wenzetu wafugaji wa asili? Hujajibu hilo.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri anayekaimu Serikali kwamba, fedha zimepatikana shilingi bilioni 20. Ungetamka kwamba ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kamili, hoja hiyo haikuwa ya kwako. Sasa ukianza kurekebisha hoja ya mtu mwingine, unaingilia tena mamlaka ya kiti kukuruhusu katika jambo ambalo halikuhusu. Wewe umesharudi kwenye hoja yako ya msingi, sasa sijui kama mipango hiyo ya Halmashauri tutaifanya hapa ndani, lakini Mheshimiwa Waziri wewe ujibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga maeneo hakufanywi na Wizara moja, ni suala mtambuka. Lazima kule kwenye Halmashauri ndiyo wanaoelewa kwamba, maeneo haya tumeya-*project* kwa ajili ya kilimo na maeneo haya ni kwa ajili ya mifugo na maeneo haya ni kwa ajili ya kujenga nyumba za Serikali, maeneo haya ni ya makazi. Kwa hiyo, ni kwamba, tutashirikiana na Halmashauri pamoja na Wizara ya Ardhi na Wizara ya Kilimo ili tuweze kutambua maeneo hayo na kuyatenga, wala hakuna neno.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* Sh. 1,108,293,000

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh. 1,043,005,000

Kif. 1004 – *Livestock Research and Training Inst.* Sh. 8,800,312,000

Kif. 1005 – *Government Communication Unit* Sh. 200,497,000

Kif. 1006 – *National Livestock Institute Mpwapwa* Sh. 2,457,473,000

Kif. 1007 – *Internal Audit Unit* Sh. 223,955,000

Kif. 1008 – *Procurement Management Unit* Sh. 442,015,000

Kif. 1009 – *Legal Services Unit* Sh. 153,549,000

Kif. 1010 – *Information Communication and Technology* Sh. 292,380,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7001 - *Veterinary Services* Sh. 8,372,810,000

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 220400, kinaonesha kwamba, zimetengwa shilingi 823,000,000. Nataka kufahamu fedha hizi zitatoshleza kwa sababu hapa fedha za chanjo zipo, lakini mara nyingi imekuwa baada ya chanjo hizi kupelekwa katika vituo na Wilaya zetu, inalazimika wafugaji wawe wanachangia gharama za uchanjaji. Je, fedha hizi zitatoshleza?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kifungu hiki kwanza zimeongezwa kidogo; mwaka jana ilikuwa shilingi 747,000,000, sasa hivi shilingi 823,000,000. Sasa kutokana na ufinyu wa bajeti ulivyo na kiasi kilichoongezwa, tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuzitumia hizi zilizopo.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nihoji kifungu kidogo cha 220400. Hizo shilingi 823,000,000 Mheshimiwa Waziri ulisema ni za nini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pauline Gekul, kifungu hicho kimeshahojiwa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Kifungu hicho ni kingine.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7005 – *Veterinary Council of Tanzania*Sh. 250,331,000

Kif. 8001 – *Animal Production* Sh. 3,523,563,000

Kif. 9001 – *Fisheries Development Division* Sh. 6,809,801,000

Kif. 9002 - *Aquaculture Development Division* Sh. 1,039,253,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

1 JUNI, 2013

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 99 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba niwarejeshe kwenye utaratibu, fungu moja halihojiwi na Wabunge wawili, huo ndiyo utaratibu ambao tumekuwa tukiendelea nao kila siku. Kwa hiyo, ukishaona tu mtu ameshahoji fungu hilo, naomba tusipoteze muda tuendeleo kwenye kifungu kingine.

Kif. 1003 – *Policy and Planning Sh. 2,424,427,400*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu cha 4486 - *Agriculture Sector Development Programme, Livestock Component* zimetengwa fedha za ndani shilingi 100,000,000, lakini fedha za nje shilingi 2,300,000,000.

Naomba nimhoji Mheshimiwa Waziri; katika maelezo yake alisema fedha za malambo zimetengwa katika Halmashauri na jumla ya shilingi bilioni tano zimepelekwa huko, lakini naona sasa kupitia fungu hili kuna kauli mbili. Ukisoma kwenye randama zimetengwa shilingi 355,000,000 za malambo, lakini shilingi 184,000,000 za gharama za mafuta na ujenzi wa malambo.

Naomba nipate kauli kwa nini hizi fedha sasa zisipelekwe kwenye Halmashauri kwa sababu huku unasema zipo Halmashauri wakati umekaa nazo zaidi ya shilingi 400,000,000?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana dada yangu. Nilizungumzia, nikasema kuna *ASDP Livestock Component*, fedha zinazotoka Ubelgiji, hizi fedha zinahudumia Wilaya nne tu, Wilaya ya Bahi, Chamwino, Kiteto pamoja na Kondo. Hizi fedha ni kwa ajili ya Miundombinu ya maji kwa ajili ya binadamu pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwa ajili ya hizi Wilaya na zimefungwa, sehemu kubwa inatolewa na Ubelgiji, ndiyo maana unaona *local component* ni milioni mia moja. Kwa sababu zipo na zimekuwepo, zinatunika hapa na zimefungwa, haziendi sehemu nyingine yeyote katika Halmashauri nyingine yeyote isipokuwa hizi Halmashauri Nne.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 - *Livestock Research and Training Inst...* Sh. 2,216,332,500/=

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye kifungu kidogo 4486, *Agriculture Sector Development Programme*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba, hiki ni kitengo cha *research* kwa ajili ya mifugo pamoja na Vyu, ni wazi kwamba, mifugo yetu mara nyingi inakumbwa na maradhi mbalimbali, lakini cha msingi nilichotaka kuuliza, ukiangalia utaona kwamba hakuna hata shilingi moja ya fedha za ndani, fedha zote katika kifungu hiki ni za nje. Naomba ufafanuzi, ni kwa nini hatujatenga hata hela kidogo.

MWENYEKITI: Ufafanuzi, Waziri!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema kwamba, *program* ya *ASDP* imekwisha, sasa hivi tunaandaa nyingine. Kwa maana hiyo ndiyo maana unaona hapo hakuna kitu. Zile fedha

unazoziona kwenye kifungu hiki kinachofuata ni kwa ajili ya *East Africa Agriculture Productivity Project* ambayo yenyewe ipo na inaongozwa na *East Africa*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 - *National Livestock Institute –Mpwapwa...* Sh. 614,704,800/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7001 *Veterinary Services...* Sh. 2,632,574,300/=

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufahamu, katika fungu lililotengwa hapa, linahusisha na chanjo ile ya kichaa cha mbwa? Kwa sababu bado katika maeneo ya ukanda wa Pwani usumbufu mkubwa upo kwa mbwa hawa vichaa. Nataka kufahamu fungu hili linahusika na hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mangungu unatakiwa useme kifungu kidogo kipi?

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Kifungu kidogo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mangungu sijamaliza maelekezo yangu, unaposimama ni lazima uwe umejiandaa na unasema kifungu kidogo namba fulani kinahusika na hicho kitu? Sasa tunaendelea.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 7002 - *Livestock Identif Regist. and Traceable Unit...* Sh. 0/=

Kif. 7003 – *Pastoral System Development...* Sh. 0/=

1 JUNI, 2013

Kif. 7004 – *Central Veterinary Laboratories*Sh. 0/=
Kif. 7005 – *Veterinary Council of Tanzania*... ..Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 8001 - *Animal Production*... .. Sh. 1,085,277,000/=

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 8001, Kifungu kidogo cha 4495, hapa fedha za ndani ni milioni 914 na za fedha za nje milioni 171, ukisoma kwenye randama, kwanza napenda kufahamu kama hii *project* ni ya *agriculture* kwa nini ipo chini ya Wizara yake, nilitegemea kwamba ingekuwa Wizara ya Kilimo, lakini pia kwenye hizo fedha ametenga milioni 60 kwa ajili ya ununuzi wa trekta. Naomba nifahamu hili trekta wanalipeleka wapi?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimweleweshe dada yangu kwamba, *livestock* kama ulisoma *agriculture* zamani ni moja ya *branch* za *agriculture*. *Agriculture* ni *broad*, lakini kuna *forestry* na kadhalika. Kwa hiyo, tunaposema *agriculture*, *ASDP* maana yake ni kama *umbrella*, lakini kuna *component* nyingi ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha ni kwa ajili ya ule mradi niliousema wa *East Africa Agricultural productivity program* ambazo zilikuwa zinapitia mwanzoni *ASDP*, lakini sasa hivi zinakuja moja kwa moja kupitia kwenye *program* hii.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 9001 – *Fisheries Development*
Division... .. Sh. 614,704,800/=

Kif. 9002 – *Aquaculture Development*
Division... ..Sh. 614,704,800/=

1 JUNI, 2013

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa!

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha na mabadiliko yatakayofuata. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo
ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2013/2014
yalipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwanza Kaimu wa shughuli za Serikali Bungeni kwa ufafanuzi mzuri leo. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu ya Watalaam wote kutoka Wizarani.

Kitu cha msingi tunachokiomba kutoka kwenu, haya tuliyoyapitisha leo na kama kutakuwa na mabadiliko mengine, basi Waziri mtusaidie sana kuzingatia hoja za

1 JUNI, 2013

Wabunge angalau kuifanya Sekta hii ya Mifugo na Uvuvi iweze kubadilika na kuchangia pato la Taifa letu kwa kiasi kikubwa na kiasi cha kutosha.

Hatuna shaka na utendaji wenu, tunawataкия kila la kheri katika utimizaji wa majukumu kwa bajeti hii ya mwaka mmoja na *Inshallah* tutakutana tena kwenye bajeti ya mwakani, lakini tukitegemea kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa kwenye sekta hii.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa ushirikiano, tumemaliza hoja hii sasa nitamwita Katibu atusaidie kuona ratiba yetu inatuambia nini ili tuendelee na kazi inayofuata. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutokea mtafaruku wa hapa na pale, Bunge kwa kutumia Kamati zake mbalimbali, liliridhia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, iendelee na bajeti yake kwa siku hii ya leo. Kama mnakumbuka mara ya mwisho tuliishia kwenye hoja hii wakati mzungumzaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwenye hoja hii akiwa anasoma hotuba yake.

Kwa kuzingatia makubaliano yaliyofanyika ndani ya Kamati zetu ndani ya Bunge, lakini na Kambi za Upinzani zilizokinzana katika hoja hii, sasa nitamwita Mheshimiwa Wenje aendelee kusoma hotuba yake lakini akiwa amezingatia maagizo yote ambayo yalipitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Wenje nadhani tunaanza ukurasa wa kumi, unaweza ukaendelea, nakupa ruhusa, utaanza pale ambapo tumekubaliana uanze, tunaendela, hatuna haja ya kuanza mwanzo tena.

MHE. EZEKIA D. WENJE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri naanzia pale nilipoachia halafu kurasa za mbele nitaruka.

MWENYEKITI: Sawasawa. Utawapa mwongozo Wabunge utaanza ukurasa gani?

MHE. EZEKIA D. WENJE-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na ukurasa wa pili ndiyo niliachia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliishia ukurasa ambao nilikuwa najaribu kueleza ni shughuli gani kama Kambi Rasmi ya Upinzani tuliielekeza Serikali kutekeleza katika mwaka wa fedha uliopita.

(5) Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali kujenga kitega uchumi katika kiwanja cha Tanzania kilichopo Dubai na kukiendeleza kiwanja namba 19 tulichopewa bure na Serikali ya Uingereza kilichopo Uingereza (*Central London*) ambavyo vimekuwa maficho ya wezi kwa kutoendelezwa kwa muda mrefu na kusababisha Serikali za nchi hizo kutaka kutaifisha viwanja hivyo.

(6) Tuliitaka Serikali kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma za Balozi zetu nchini China na Uingereza kutoa hati za kusafiria kwa Mataifa mengine hasa ya Afrika Magharibi ili kubaini ukweli na kuliondolea Taifa aibu kutokana na tuhuma hizi.

(7) Tuliitaka Serikali kukarabati jengo la Ubalizi wetu nchini China ambalo lilikuwa na nyufa na kuvuja nyakati za mvua na kununua samani na vifaa vya ofisi kama mashine za nukushi na za kurudufu ambazo zilikuwa hazipo.

(8) Tuliitaka Serikali kununua magari mapya ya Ofisi ya Ubalozi wetu nchini China kwa kuwa magari matatu yaliyokuwepo yalikuwa yameshapitiliza muda wa miaka 10 ambao kwa mujibu wa Sheria za China hayapaswi kutumika tena.

(9) Tuliitaka Serikali kupeleka Mwambata wa Kiuchumi (*Economic Attaché*) nchini China, ili kufuatilia fursa mbalimbali za kiuchumi katika kutekeleza diplomasia ya uchumi kutokana na mahusiano makubwa ya kibiashara kati ya nchi yetu na China.

(10) Tuliitaka Serikali kuwawekea zuio wahusika wa kashfa ya rada kuwa viongozi wa shughuli za Kiserikali ili angalau kuonesha uwajibikaji wa kimaadili (*moral accountability*) baada ya kushindwa kuwawajibisha kisheria, ili kuondoa dhana iliyojengeka miongoni mwa jamii kwamba dola imetekwa na mafisadi.

(11) Tuliitaka Serikali kuchunguza na kuwachukulia hatua Watanzania (Wafanyabiashara na Wanasiasa) waliotorosha kiasi kikubwa cha fedha za nchi yetu (zaidi ya shilingi bilioni 315) na kuzificha katika mabanki ya Uswisi.

(12) Tuliitaka Serikali kutoa mchanganuo wa jinsi fedha za rushwa ya rada (chenji ya rada) zilivyotumika.

(13) Tunaitaka Serikali kueleza bayana faida za kiuchumi tunazopata kama Taifa kwa kushirikiana na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa ili kuthibitisha kwamba, mashirikiano hayo hayatumiki kupora rasilimali za nchi yetu kwa hila ya "uwekezaji."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza kwenye mambo mahsusi kwa kipindi hiki cha bajeti ya 2013/2014, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, kuitaka Serikali kutoa majibu mbele ya Bunge hili Tukufu, kwamba,

imetekeleza kwa kiwango gani masuala yaliyoorodheshwa hapo juu, tuliyoitaka iyatekeleze (moja baada ya lingine) kwa mwaka wa fedha unaomalizika wa 2012/2013?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu wa fedha za safari za Rais, shilingi bilioni 3.5; katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013 nilihoji kuhusu Serikali kuchunguza na kuchukua hatua kwa waliohusika na upotevu wa shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya safari "hewa" za Rais nje ya nchi, ili waweze kubainika na kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni nyingi sana na hasa ikikumbukwa kuwa mwaka jana 2012, wapo Mawaziri ambao walichukuliwa hatua na Bunge hili kutokana na upotevu ama udhaifu uliofanyika kwenye Wizara zao, wapo ambao walihukumikiwa kutokana na kupotea kwa Twiga kwenye Wizara zao, wapo waliohukumikiwa kutokana na udhaifu katika kusimamia Wizara zao na taasisi zilizoko chini yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, iweje leo Waziri aliyeshindwa kusimamia Wizara yake na kusababisha upotevu wa fedha hizi mpaka leo bado yupo, wakati wapo Mawaziri wengine waliohughulikiwa kutokana na udhaifu walioonesha kwenye kusimamia Wizara zao, au ndio kusema kuwa Serikali hii ya CCM inafanya upendeleo na kuonea baadhi ya Mawaziri na kuwaacha wengine? *"This clearly indicates the double standard nature of this Government in the performance of its functions"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Ubalozi Mdogo Guangzhou –China; mwaka jana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kuwa Serikali ianzishe Ubalozi Mdogo katika Jiji la Guangzhou kwa ajili ya kurahisisha biashara kati ya wafanyabiashara wa Tanzania na wale wa China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inatambua kuwa Serikali imelifanyia kazi wazo hili

1 JUNI, 2013

na imeamua kuanzisha Ubalazi Mdogo katika mji huo, ila tunataka kujua ni lini Ubalazi huu utazinduliwa rasmi, kupata watendaji na vitendea kazi ili uweze kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Diplomasia ya Uchumi; Moja ya matarajio ya ushirikiano wa Kimataifa ni kuweza kutafuta na kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi zinazoweza kupatikana katika mashirikiano hayo ili kama Taifa, tuweze kujikwamua kiuchumi na kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume na matarajio hayo mazuri, sasa nchi yetu imegeuzwa kuwa kitega uchumi cha nchi zilizoendelea kwa kisingizio cha “ushirikiano wa Kimataifa” chini ya mwavuli wa “uwekezaji”. Matokeo ya ushirikiano huu wa kinyonyaji (*exploitative relationship*) ni kwamba, kiwango cha umaskini katika nchi yetu kimeongezeka na hivyo kuifanya nchi yetu kuwa tegemezi zaidi kuliko ilivyokuwa hapo kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikerwa na unyonyaji na unyanyasaji uliokuwa ukifanywa na Wakoloni, hali iliyompelekea kusema maneno yafuatayo:

“Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, tumepuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndiyo uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka kufanya mapinduzi”

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada uhuru, Mwalimu akaanzisha Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Ujamaa ulilenga kujenga umoja wa Kitaifa na umoja wa Bara la Afrika dhidi ya unyonyaji wa kibeberu, wakati kujitegemea kulimaanisha kujenga uchumi endelevu ili kulijengea Taifa heshima na nguvu ya maamuzi mbele ya Mataifa mengine na kuliepusha Taifa na fedheha ya kuombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imesikitishwa sana na kitendo cha Serikali kulidanganya Taifa, kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 kwamba:-

"Katika kipindi cha miaka mitano 2010 -2015, Serikali ya Chama cha Mapinduzi itatekeleza Sera ya Diplomasia ya Uchumi" wakati Ibara ya 98(i) ya Ilani hiyo hiyo ya CCM inasema kwamba, Serikali ya CCM itaendelea kushinikiza nchi tajiri kutekeleza ahadi yao ya kutenga asilimia 0.7 ya pato la Taifa la nchi zao kwa ajili ya misaada kwa nchi maskini".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba ahadi hii ya asilimia 0.7 ya pato la Taifa la nchi tajiri ambayo Serikali ya CCM inakodolea macho ni fedha za walipa kodi wa nchi hizo kama ambavyo wananchi wetu wanavyolipa kodi. Aidha ni aibu kwa Serikali hii ya CCM kuchukua ahadi za wahisani na kuziweka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM kama ahadi kwa wananchi ili kubembelezea kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uvivu wa kufikiri na kubuni mbinu za kuikwamua nchi hii na umaskini, Serikali hii ya CCM sasa hivi imeachana kabisa na sera ya kujitegemea, ambayo Mwalimu kupitia Azimio la Arusha alisema kwamba "...Hakika ni ujinga na upumbavu zaidi kwetu sisi, kufikiri kwamba tutaondokana na umaskini wetu kwa misaada ya fedha kutoka nje kuliko rasilimali zetu wenyewe."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, kama inatekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kutegemea ahadi ya misaada ya fedha kutoka kwa wahisani na kama hilo ndio suluhisho la matatizo yanayokumba uchumi wetu kama Taifa kwamba, tutaweza kuendelea kwa kutegemea hisani na fadhila za wafadhili, huku tukishindwa kuzitumia rasilimali zetu kwa ajili ya kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani imejiridhisha kwamba kauli mbiu ya Diplomasia ya Uchumi imeendelea kubakia kama ilivyo kauli mbiu ya *Kilimo Kwanza* ambayo imebakia kutamkwa na viongozi bila kuwa na mkakati wa utekelezaji wala vigezo vya kupima kiwango cha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kujitathimini Kiutawala Bora (*APRM*), itakumbukwa kuwa mnamo mwezi Januari, 2013, ulifanyika mkutano wa 20 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, Mjini Addis Ababa, Ethiopia na ni katika mkutano huo Mheshimiwa Rais Kikwete aliwasilisha taarifa ya nchi yetu kuhusu kujitathimini katika utawala bora kwenye mpango wa nchi zinazojitathimini katika utawala bora (*APRM*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa hiyo (randama ukurasa wa 15) nchi yetu ilitakiwa kutafutia ufumbuzi changamoto zifuatazo:-

- (i) Migogoro baina ya wakulima na wafugaji;
- (ii) Imani za kishirikiana (uchawi);
- (iii) Kuhakikisha kuwa manufaa ya kukua kwa uchumi yanawafikia wananchi; na
- (iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu mipango na sera za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi ambazo nyingine zinatia aibu Taifa letu mbele ya Mataifa mengine kama vile sisi kuonekana ni wachawi na hivyo kutakiwa kuchukua hatua dhidi ya uchawi, ni fedheha na aibu kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua Serikali na Wizara imechukua hatua gani mpaka sasa katika kukabiliana na changamoto hizi na hasa tatizo la wakulima na wafugaji na kuhakikisha kuwa manufaa ya kukua kwa uchumi wetu yanawanufaisha wananchi na sio kuwanufaisha baadhi ya viongozi na mafisadi wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlipuko wa bomu Arusha na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa; mwaka huu tarehe 5 Mei, Kanisa Katoliki, Parokia ya Olasiti huko Arusha lililipuliwa

kwa bomu. Tukio hili lilitokea wakati akiwepo Balozi wa Vatican Nchini na ambaye ndio alikuwa mgeni wa heshima kwenye tukio la kuzindua Parokia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya tukio hilo, Balozi wa Vatican nchini aliwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na kuonesha kuwa Tanzania sio nchi salama sana kutembelewa na wageni na kama wakitembelea, basi wanapaswa kuchukua tahadhari kubwa kwa kipindi chote watakapokuwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua nini kauli ya Serikali kuhusiana na tukio hili na hasa kuhusiana na taarifa za hali ya usalama wa nchi yetu na wageni zilizowasilishwa kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari za viongozi nje na misafara mikubwa; tangu mwaka 2011/2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikihoji suala la misafara ya Viongozi wa Kitaifa kuwa mikubwa kutokana na kuambatana na watu wengi ambao wengine wanakuwa hawana hata majukumu ya msingi ya kufanya wakati wa ziara hizo huku wakiliongezea Taifa gharama kubwa ya kuwasafirisha na kulipia malazi yao na starehe zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tumekuwa tukipendekeza na kushauri kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Rais wa nchi kuamua kutuma wasaidizi wake kwenye baadhi ya ziara za nje kama wanavyofanya viongozi wengine wa nchi jirani, kama Rais Kagame wa Rwanda na hata Mwai Kibaki, Rais mstaafu wa Kenya alivyokuwa anafanya akiwa Rais, kwani kwa kufanya hivyo atapunguza msururu wa maafisa na viongozi mbalimbali wa kuambatana naye. Tunashauri tena kuwa rais awe anatuma wasaidizi wake kwenye ziara za kawaida na yeye awe na jukumu la kushiriki kwenye ziara rasmi za Kiserikali (*State Visits*) na mikutano maalum ya Kimataifa kama *UN* na *AU*.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri mambo

yafuatayo yafanyike ili kupunguza gharama hizi kubwa za kuwasafirisha viongozi na misafara isiyokuwa na tija kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itengeneze kanuni za kudhibiti idadi ya maafisa na watu ambao watakuwa wakiambatana na Rais kwenye ziara za nje yaani (idadi ya wajumbe kwenye misafara iwe wazi na ijulikane).

(ii) Pawepo na kanuni za kuainisha kuwa ni nani watapaswa kupanda ndege daraja la kwanza na wale wenye haki ya kulala kwenye hoteli za daraja la kwanza wajulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara ya *Protocol* na mabilioni ya fedha za safari za nje; katika mwaka wa fedha 2011/2012, fungu 221100 *travel out of country* zilitumika sh. 36,121,942,870.00 kwa ajili ya safari za nje ya nchi kwa viongozi wakuu. Katika mwaka wa fedha uliopita wa 2012/2013, kifungu 1010 ambacho ni kwa ajili ya *protocol* walitengewa sh. 8,372,581,824 na fedha ambazo zilikuwa zimepokelewa na Wizara mpaka mwezi Februari 2013 zilikuwa jumla ya sh. 26,081,860,727.16! (randama ukurasa wa 4) jedwali la 2 na zilitumika kwa ajili ya kugharamia safari za viongozi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Bunge lilikuwa limetenga na kuidhinisha kiasi cha sh. 8,372,581,824 kwa ajili ya kifungu hiki cha *Protocol, travel out of Country* kwa mujibu wa kitabu cha matumizi ya kawaida, juzuu ya pili (*volume II*). Jambo la kushangaza ni kwamba, Wizara iliieleza Kamati na Bunge hili kuwa walishatumia zaidi ya bilioni 26.081 kutokana na fedha walizokuwa wamejitengea wenyewe Wizara ambazo hazikuidhinishwa na Bunge kiasi cha bilioni 29.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, inataka maelezo ya kina kuhusiana na mamlaka ya Wizara hii kwenda kutenga na kutumia fedha nyingi kuliko zilizokuwa zimeidhinishwa na

Bunge hili na zilikuwa fedha kwa ajili ya safari za kwenda nje ya nchi, ni nani aliipa Wizara mamlaka hiyo na kiburi hicho kiasi cha kupuuza maamuzi ya Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha 2013/2014, kitengo hiki cha Protocol kimetengewa jumla ya sh. 15,155,377,400.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo, ambazo katika mchanganuo wake kwenye kifungu 1010 kifungu kidogo cha 221100, *travel out of Country* zimetengwa sh. 9,381,328,850.00 kwa ajili ya kugharamia safari za kikazi za viongozi wa Kitaifa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kifungu kidogo cha 220700, *rental expenses* zimeombwa jumla ya sh. 2,925,445,000.00 kwa ajili ya kukodisha ndege, magari na kumbi za mikutano kwa ajili ya viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haikubaliani na kamwe haitakubaliana na ufujaji huu wa fedha za walipa kodi maskini wa Tanzania. Tunamtaka Waziri atoe maelezo ya kina kwa Watanzania ni kwa nini nchi maskini kama yetu tutumie fedha nyingi kiasi hicho kwa ajili ya safari za viongozi nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hatukubaliani na kitendo cha kutenga fedha kwa ajili ya kukodi ndege wakati Rais ana ndege yake ambayo ilinunuliwa na mabilion ya fedha za Watanzania. Ikumbukwe kwamba ndege hii ya Rais ilinunuliwa kwa mbwembwe nyingi kiasi kwamba, Waziri wa Fedha wa wakati huo Ndugu Bazil Mramba alisema Watanzania wafunge mkanda, hata kama watakula majani, lazima ndege ya Rais inunuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa wamekula majani sasa kiasi cha kutosha, bado tena Serikali inaendelea kuwanyonya ili ipate pesa za kukodisha ndege wakati Rais ana ndege? Hivi Serikali sasa inataka Watanzania wale mawe ndio ijue kwamba watu wamefunga mkanda kiasi cha kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje; mwaka 2012, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ilifanya ziara kwenye Balozi takribani zote na iliona matatizo yanayozikumba Balozi zetu huko na matumaini yetu yalikuwa kuwa, baada ya ziara ile ya Kamati ingehakikisha kuwa fedha zinaongezwa kwenye Wizara hii na hasa kwenye fungu la maendeleo ili tuweze kuboresha mazingira ya Balozi zetu. Kinyume na matumaini hayo, ni kwamba, hakuna jitihada zilizofanyika kuongeza bajeti ya Wizara hasa katika fedha za maendeleo.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kuishinikiza Serikali ili kuhakikisha kuwa katika mwaka huu wa fedha Wizara hii inaongezewa fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya Balozi zetu na hiyo ndio njia pekee ya kuonesha kuwa Kamati haikwenda kufanya utalii bali ilienda kuona matatizo ya Balozi zetu na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufisadi katika ununuzi wa jengo la Ofisi na makazi katika Ubalози wa Tanzania Jijini Paris, Ufaransa; katika mwaka huu wa fedha kwa mujibu wa randama ya Wizara ni kuwa, mwaka huu wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 28 (28,000,000,000.00) zimepangwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na kati ya hizo kiasi cha sh. 24,188,000,000.00 ni kwa ajili ya ununuzi wa jengo la ofisi na makazi ya Balozi Jijini Paris, Ufaransa (kwenye randama ukurasa wa 25) na kiasi cha sh. 3,812,000,000.00 ni kwa ajili ya gharama za ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi yaliyopo Ubalози wa Tanzania Maputo, Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma randama ya Wizara (ukurasa wa 120) katika kasma 6391, kifungu kidogo 411100, kiasi cha fedha kilichoombwa ni sh. 23,900,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa jengo la ofisi na makazi ya Balozi Jijini Paris, Ufaransa na sh. 3,700,000,000.00 kinaombwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi yaliyopo Ubalози wa Tanzania Maputo, Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika mwaka

huu wa fedha 2013/2014, kwenye kasma 6391, katika fungu la Maendeleo (randama ukursa 120) Wizara inaomba kutengewa kiasi cha shilingi milioni 400 (400,000,000.00) (kifungu 221100) fedha ambazo hazipo kwenye kitabu cha matumizi ya kawaida, juzuu ya pili (*volume II*) kwa ajili ya posho ya kujikimu na gharama za usafiri kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara. Miradi yenyewe ni miwili mmoja wa kununua nyumba Ufaransa na kukarabati jengo Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkanganyiko huu wa kimahesabu unatia mashaka makubwa sana kuhusiana na dhamira ya Serikali na Wizara hii hasa fedha zinapotengwa bila kufuata utaratibu wa kibajeti na bila kuingizwa kwenye vitabu vya fedha na mafungu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, inajuliza tunapitisha mafungu yapi sasa? Kwani kwenye randama fedha zinatofautiana kwenye fungu moja la maendeleo baina ya (ukurasa 25 na 120), vilevile kwenye kitabu cha matumizi ya kawaida, hali ni tofauti kwenye fungu la *travel out of the Country*, kwani sasa Wizara imejiongezea shilingi milioni mia nne kwa ajili ya kufuatilia miradi miwili ambayo ni kununua jengo Paris na kukarabati Jengo la ubalozi - Maputo, Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utata wa fedha unaendelea kuonekana kwenye randama ya Wizara katika kiambatanisho Na.1, utekelezaji wa ushauri na mapendekezo ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa' katika ushauri/mapendekezo Na. 5 Kamati iliitaka Wizara itoe mchanganuo wa matumizi ya fedha za bajeti ya maendeleo zilizopokelewa kutoka hazina katika mwaka wa fedha 2012/13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Wizara yalikuwa kama ifuatavyo, nanukuu randama ya Wizara: "Katika mwaka wa fedha 2012/2013, hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Wizara imepokea kutoka Hazina kiasi cha sh. 13,261,281,600.00 ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha sh. 9,660,000,000.00

zimetumika kwa ajili ya kulipia malipo ya awali ya ununuzi wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Balozi Paris, Ufaransa; sh. 995,930,000.00 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Serikali lililopo Maputo, Msumbiji; sh. 626,899,155.00 zimetumika kwa ajili ya ukomboaji wa vifaa vya ujenzi bandarini vilivyotumika katika ujenzi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere na safari ya kikazi ya wataalam katika Balozi za Maputo, Pretoria na Lusaka kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu wa miradi ya maendeleo iliyopo katika Balozi hizo na sh. 1,978,452,485.20 bado hazijatumika na zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kulipia gharama za ukarabati wa jengo la Serikali lililopo Maputo.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufuatilia na kufanya tathimini ya kina kuhusiana na majibu hayo ya Wizara kuhusu fedha za maendeleo kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la Maputo na kununua Jengo la Ofisi na Makazi ya Balozi Ufaransa na kukuta kuwa ni fedha nyingi sana kuliko uhalisia wenyewe. Kwa mfano, Waziri anataka Bunge na Taifa tuamini kuwa kufanya ukarabati wa jengo moja la ofisi Maputo Msumbiji tunahitaji kutumia kiasi cha sh. 4,695,930,000.00 kwa kutumia fedha inayoombwa mwaka huu wa fedha na zile ambazo tayari zilishalipwa katika mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha wakati Wizara inawasilisha majibu yake kwenye Kamati ya kudumu ya Bunge walisema kuwa (swali 12 ukurasa wa 5): “Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Serikali yaliyopo Maputo ni sh. 3,812,000,000.00.....kiasi hicho cha fedha kinatosheleza kukamilisha kazi ya ukarabati wa majengo hayo ya Serikali yaliyopo Maputo, Msumbiji. Aidha, kununua jengo moja la ofisi na makazi katika Jiji la Paris Ufaransa tunahitaji kutumia kiasi cha sh. 33,560,000,000.00”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu haya ya Wizara, ni kuwa tayari Wizara imeshafanya malipo ya shilingi bilioni 9.66 kama malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa jengo la ofisi na makazi huko Paris Ufaransa na kuwa tayari

tumeshafanya malipo ya awali kiasi cha shilingi milioni 995.930 kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Ubalози huko Maputo, Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika kiasi hiki ni kikubwa kupitiliza na hata utafiti na tathimini ambayo ilifanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilionyesha kuwa kununua jengo la ofisi katika Jiji la Paris kwenye Mji wa bei ghali kama Co'te d'Azur (*most expensive area in Paris*) huwezi kutumia fedha nyingi kiasi hicho kwa ajili ya manunuzi ya jengo la ofisi na makazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunakumbuka sakata la ununuzi wa jengo la Ubalози lililomkumba balози Profesa Mahalu huko Roma, Italia na yaliyofuatia mpaka kesi na fedha zetu tulizoambiwa kuwa zimepotea hazikuweza kurejeshwa baada ya Profesa Mahalu kushinda kesi hiyo Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu kuhusiana na mambo yafuatayo:-

(i) Ni eneo gani ambalo tumepata jengo la kununua kwa ajili ya Ubalози na makazi ya Balози huko Paris, Ufaransa na ni nyumba ya aina gani inayogharimu kiasi hicho cha fedha?

(ii) Je, Serikali inaweza kuonesha mkataba wa manunuzi wa nyumba hizo (Paris) kwa Bunge na tutalipa kiasi gani kununua jengo hilo?

(iii) Ni nani au Wakala gani wa Serikali aliyefanya tathimini ya hayo majengo na kuamua kuwa tulipe kiasi hicho cha fedha?

(iv) Ni kampuni gani iliyohusika katika kufanya makubaliano ya mauziano ya nyumba hizo na tunawalipa kamisheni ya shilingi ngapi?

(v) Nani aliidhinisha kutumika kwa kiasi kikubwa hivyo kwa ajili ya kununua jengo la Ubalozi na makazi huko Paris, je, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, ilishirikishwa katika manunuzi haya?

(vi) Ukarabati unaofanywa kwenye jengo la Maputo, Msumbiji ni wa aina gani, au tunajenga upya nyumba hizo?

(vii) Ni kampuni gani ya ujenzi inayofanya ukarabati wa jengo letu huko Msumbiji na mkataba wa ukarabati huo uko wapi? Tungetaka uwekwe hadharani ili tujue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inatoa hoja ya kumtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kufanya uchunguzi maalum (*Special Audit*) kuhusiana na ununuzi wa majengo haya na ukarabati unaofanyika kwenye jengo letu huko Maputo, Msumbiji na kuona kama thamani halisi ya fedha imezingatiwa na kama sheria ya manunuzi ya umma imefuatwa kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tungetaka sehemu ya fedha hizi zitumike kwa ajili ya kukarabati jengo letu la zamani la Ubalozi lililopo Washington ambalo kwa sasa halitumiki baada ya kutekelezwa kwani likikarabatiwa litaweza kuliongezea Taifa mapato kutokana na matumizi ya kibiashara ya jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Wizara wa kutoa *visa* kwenye Balozi tu haukubaliki. Kwa Mujibu wa majibu ya Wizara kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilionesha kuwa, ili Wizara iweze kukusanya fedha za kutosha kwenye Balozi zetu ni kwa kurudisha utaratibu wa utoaji wa *visa* kufanywa na Balozi zetu tofauti na utaratibu unaotumika hivi sasa ambapo wageni huweza kupatiwa *visa* pindi wanapowasili katika vituo vya kuingilia nchini yaani (*visa on arrival*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haikubaliani na wazo hili la Wizara kwani badala ya kuongeza wageni kuja nchini litapunguza sana hasa ikizingatiwa kuwa ni nchi chache sana ambako tuna ofisi za Balozi na pia kuna nchi nyingine kama Marekani ambapo, kama mgeni yupo California na anataka kusafiri kuja Tanzania atalazimika kwanza kusafiri kwenda Washington ambako ndiko kwenye Ubaloji atafute *visa* na ndipo aweze kuja nchini. Utaratibu huu utaongeza gharama kubwa za usafiri kwa wageni na watalii na hivyo kulipotezea Taifa mapato yatokanayo na utalii kwani wageni watapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunaikumbusha Wizara kuhusiana na Itifaki ya kuwa na *Single Tourist Destination Protocol* na uwepo wa hati ya kusafiria na *visa* moja ya utalii *Single Tourist Visas* kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hivyo, kama sisi tukifanya huo uamuzi, basi wenzetu Kenya wataendelea kupata wageni wengi zaidi kutokana na *visa* ya pamoja na wageni wataingia Tanzania kutokana na *visa* za Kenya chini ya Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Mabalazi wa mwaka 2013/2014, Wizara inahitaji kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufanikisha Mkutano wa Mabalazi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Wizara iliwasilisha maombi ya fedha hizo Hazina kama sehemu ya kipaumbele, lakini hazikuweza kupatikana.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuiondoa aibu hii na kutenga fedha hizo kwa ajili ya kufanikisha mkutano huo na tunapendekeza kuwa katika fungu la *protocol/safari* za nje ndipo fedha hizo zipunguzwe na kutumika kwa ajili ya Mkutano wa Mabalazi wetu ili waweze kupeana ushauri na uzoefu ili kuboresha ufanisi wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utaratibu wa Kupeleka Fedha kwenye Balozi; kutokana na utaratibu wa kupeleka

1 JUNI, 2013

fedha kwenye balozi zetu kuwa na mlolongo mrefu wa kwanza kutoka Hazina na kupelekwa Wizarani, ndipo Wizara isambaze fedha hizo kwenye Balozi zetu mbalimbali umesababisha fedha kuchelewa kufikishwa kwa wakati kwenye Balozi zetu na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa na ucheleweshaji wa kazi kwenye Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kubadilisha utaratibu huu na Hazina iwe inapeleka fedha hizo moja kwa moja kwenye Balozi husika badala ya kuzipitisha Wizarani kama ilivyofanya kwenye fedha za Halmashauri mbalimbali nchini ili kupunguza usumbufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Wenje na hasa kwa kuzingatia muda, hujaongeza hata dakika moja.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, maoni ya Kamati iliyochambua hotuba hii na leo baada ya kumaliza kusikiliza maoni ya Kambi ya Upinzani. Sasa tutaruhusu michango ya pamoja kwa maana ya mjadala wa pamoja.

Ninao wachangiaji watatu, lakini kwa uwiano wa Kambi tunaweza kuongeza mmoja na baada ya hapo tutaendelea na utaratibu wa kikanuni. Nitamwita kwanza Mheshimiwa Beatrice Shellukindo atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbowe na kama muda unatosha tutamruhusu Mheshimiwa Mariamu Kasembe. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo!

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwa kiasi fulani Wizara hii ya Mambo ya Nchi za Nje ambayo kwa kiasi nimebobeza kwenye masuala yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri na kubwa anayofanya Kimataifa. Huwezi kujua mpaka utakapotembelea nje, ukienda nje ya nchi ndipo utakapojua ni mambo gani makubwa na umuhimu wake ni wa kiasi gani kule nje kwa maslahi ya Watanzania. Binafsi namshukuru Mwenyezi Mungu napata fursa kadhaa kwenda maeneo tofauti na mara zote ukisikia kiongozi anayesifiwa wa kwanza ni Mheshimiwa Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi binafsi, naomba nimpongeza sana. Lakini vile vile nimpongeze pia kwa kuweka sifa ya Tanzania nje, heshima ya Tanzania. Niombe tu niseme Waheshimiwa Wabunge na wananchi mnaosikiliza, Tanzania sisi tunathaminika sana nje. Ukienda kwenye mkutano wowote akisimama kuongea Mtanzania kila mtu anakuwa makini kusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaheshimika pia kwa sababu tunajiheshimu, hapa ndani tunaweza tukajidharau, lakini nataka niwahakikishieni kabisa na kwa wale Watanzania ambao wanakwenda nje mara kwa mara, wanahudhuria mikutano watakubaliana name, heshima yetu ni kubwa sana huko nj. Tunaaminika kwa usalama, tunaaminika kwa uaminifu, tunaaminika kwa mambo mengi mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sisi wenyewe tusijidharau tupite vichwa juu. Mimi nikienda kwenye mikutano, tena naongea kwa ujasiri, naitwa Beatrice Shellukindo natoka Tanzania, basi utaona kila mtu makofi kwa sababu gani, heshima na sifa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mahali hata ndani ya familia ambapo hakuna upungufu lakini kwa kweli nipende kusema kwamba, Watanzania rasilimali peke yake tuliyonayo ni katika nchi chache sana duniani ambazo zinazo na hapo ni zile rasilimali ambazo tumeshazivumbua mpaka sasa na nyingine bado.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Watanzania, turinge, tupite vifua juu, tujue sisi tunathaminika, sisi ni wa muhimu na tunahitajika na watu wa ndani na wa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kupongeza kwa heshima hiyo hiyo Mheshimiwa Rais aliyoiweka nje, tumeweza kupata ugeni wa mikutano mingi mikubwa siwezi kuisema yote kwa sababu ya muda, lakini mikutano ya Kimataifa haikatiki hapa Tanzania. Sisi tuna kitu gani zaidi kama siyo heshima ambayo tumejiwekea? *Smart Partnership Dialogue* inaanza Marais zaidi ya kumi na tano wataingia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Bwana Mbilinyi ambaye ndiye Mkurugenzi Mkuu wa *TNBC* ambao wameendesha mikutano kwenye Wilaya, Mikoa na Kanda na sisi tulishuhudia Wabunge wa Mkoa wa Tanga, Pwani na Morogoro tuliitwa kujadili masuala mbalimbali ambayo yataingia kwenye hivi vikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya mikutano ya **SADCOPAC** na mingine mingi, kwa hiyo yote hii ni sifa ambayo ameweza kutujengea. Lakini vile vile viongozi wa juu ambao wameweza kufika hapa. Kuna nchi viongozi wengine hawafiki mara kwa mara, lakini Tanzania kwa sababu tunafahamika akina George Bush, Rais wa China na wengi kwa sababu ya muda siwezi kuwasema na kikubwa zaidi Rais Obama ambaye anakuja hivi karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaweza akaona ni jambo dogo, lakini si jepesi hivyo ni lazima ujenge jina hilo. Lakini niombe tu Watanzania tushirikiane ili tuilinde amani yetu kwa sababu tukiharibu tu hapo hizi sifa zote zitapotea. Tushirikiane tuweze kujenga usalama wetu ili kwamba na sisi tuweze kuwa salama na watu waendeleo kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unapoongelea ufanisi wa Tanzania katika medani ya Kimataifa huwezi kumuacha

Bernard Membe, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Membe kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mara kadhaa akiteuliwa kuongoza kwenye mikutano mbalimbali, kwa kweli mimi binafsi nampongeza na hata wengi mnaona kwamba, katika mikutano mbalimbali huwa anashiriki kikamilifu na kuweza kuweka heshima na sifa ya Tanzania. Nimpongeze pia Naibu wake, Katibu Mkuu pia Haule na watendaji wote, nawapongeza sana kwa kazi wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nipongeze Mabalizi wetu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Sura ya Tanzania nje pia ni pamoja na majengo yetu, jinsi ambavyo Balozi zetu zipo na kadhalika, lakini kwa kweli kumekuwa na matatizo makubwa sana kwa sababu ya muda huwezi kusema yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mungu pia nilikuwa kwenye Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, ambapo niliweza kushiriki katika ziara za nchi tofauti tofauti. Niwahakikishie hatukwenda kutalii, tulikuta mambo mengi sana, kwa mfano, kule maeneo ya Msumbiji tuliwahi kupewa jengo enzi za Samora kile kiwanja mpaka tukakipoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Zambia jengo ambalo baba wa Taifa na Rais Kaunda walikaa kufanya majadiliano nalo mpaka leo limekuwa *condemned*, halifai, Malawi Ubalizi wetu upo kwenye *shopping mall*, kuna maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Oman tumefika, Oman tumeahidi kwamba tutajenga jengo la Ubalizi na wamesisimkwa kweli na wako tayari, lakini utashangaa na makubaliano tumesainiana juzi, lakini mpaka sasa hivi fedha hakuna hata ya kujenga kule. Abuja ambayo ndiyo inawakilisha Nigeria, ndiyo inawakilisha Ubalizi wetu, nchi 13 za *West Africa*, nao wanasubiri *design* wameanza, hakuna fedha.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba sana tuangalie tunafanya nini. Wakati Balozi Majaha akiwa Uingereza aliomba mkopo katika Serikali ya Uingereza akakubaliwa, akachukua eneo lile ambalo liko katika eneo ambalo kila mtu analizungumzia, eneo la juu kabisa, *prime area*, lakini bado kibali hakikuweza kutoka mpaka ile fursa ikapotea. Sasa sijui tatizo ni nini? Ukiangalia Sheria pale kuna kipengele nimejaribu kuchambua kinaonesha Waziri anayo nguvu ya kuweza kuamua. Anaweza akafanya hayo maamuzi, lakini sijui panatokea ugumu gani na kwa nini hatufanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubalozi wa Nairobi *NSSF* walikuwa tayari kujenga tangu 2010 nakumbuka, akiwa Mheshimiwa Waziri Kapuya kama kumbukumbu zangu ziko sahihi na akakubali kwamba, ardhi yote tutachukua sisi asilimia yote, ni kwamba, tutalipa ule mkopo, lakini hadi leo hakuna jibu, lile eneo mpaka mtu ametaka kulidai, naomba sana Mheshimiwa Waziri pale ambapo ana ugumu atuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kwenye hotuba yake anazungumzia *mortgage financing* kwamba, Mabalizi waandike sasa andiko kuhusu maeneo kama hayo jamani, hiki kitu mbona kilishafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe jamani hizi fursa tutazikosa na siku zinavyozidi kwenda vitu vinazidi kuwa ghali. Kwa hiyo, inakuwa ni ngumu. Kamati ya *Foreign* ilipozunguka kwa kweli ilitoa taarifa nzuri sana, lakini nasikitika kusema juzi nafuatilia nakuta hata kipengele kimoja hakijashughulikiwa kwenye ile taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa ruhusa yako pengine ile taarifa igawiwe hapa Bungeni ili Wabunge kwa sauti moja tuweze kuelewa tunaongelea nini, tuweze kubadilisha sura na taswira yetu huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimesoma kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri umezungumzia kwa vizuri sana

1 JUNI, 2013

kwamba, unataka kuunda chombo kinaitwa *special purposes vehicle*, hiki kitakuwa kinasimamia mali zetu, majengo yetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kusema *TBA* ndiyo wenye dhamana ya majengo yetu ndani na nje, sasa tukianza kuunda chombo kingine tutakuwa tunafanya *duplication*. Niombe tuwape uwezo, tuwawezeshe *TBA* waweze kwenda nje, mali zetu ziko chini ya Mhakikimali wa Hazina, magari yetu yako chini ya *TEMESA*, sasa niombe tusiunde vyombo vingine, tukatumia hela nyingi na tukapoteza muda, ni gharama ya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kama inawezekana tuwawezeshe hawa waweze kwenda nje. Utashangaa *TBA* hawana orodha hata ya majengo yetu, hata haya mengine yanapotea potea. *South Africa* kuna jengo kidogo liondoke pale na lilikuwa la Serikali. Kwa hiyo, niombe kabisa kwamba, tuwawezeshe waweze kwenda kuhakiki mali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile niombe kikao cha Mabalozzi mara ya mwisho kilifanyika miaka sita iliyopita Zanzibar. Balozzi kukutana ni muhimu sana kwa sababu tunabadilishana zile changamoto. Niombe tu Mheshimiwa Waziri kwa sababu hili ni jambo pia hata yeye ameliona, lakini najua mengi yanakubana kwa sababu ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja tuhakikishe kwamba na Wizara hii inapewa stahiki kuweza kufanya kikao hicho. Kuna suala la Katiba, kuna masuala mbalimbali ambayo yanahitaji diplomasia ya mambo ya uchumi kuyajadili. Ni muhimu sana Mabalozzi wetu wakakutana na hasa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nije kwenye *APRM*. *APRM* jamani hiki chombo tulizungumzia mara iliyopita. Lile baraza linalosimamia limeshapitwa na wakati wake,

1 JUNI, 2013

lishakwisha muda wake, tatizo ni kwamba, sasa mambo mengi hayaendi kama inavyotakiwa na hiki ni chombo cha kutathmini utendaji wetu wa Serikali (*good governance*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe kabisa ile *Nation Governing Council* itafutiwe watu upya na wawe watu wenye nafasi, wenye muda wa kutosha kufanya hiyo kazi na wenye upeo. Lakini vile vile *APRM* wapewe nao kasma yao, (*vote*) yao hii kuweza kuegemea huku, inakuwa ni shida, fedha zisipokuwepo inakuwa ni shida. Niombe sana wapewe kasma yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, mwaka jana Mheshimiwa Waziri alitangaza kwamba kutakuwa na Balozi ndogo mbili Marekani ili kukuza diplomasia ya uchumi, lakini nimeona kimya, labda pengine ni suala la fedha, lakini naomba kama nia ilikuwa ni nzuri, basi tuendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, *dual citizenship*, huu uraia wa sehemu mbili naomba sasa ukamilike. Tumechoka kuliongea, kama kuna jambo ambalo Bunge hili linatakiwa lifanye, tufanye tumalize wale *Diaspora* hasa, kwa mfano, *Diaspora* wa Uingereza ambao wana mshikamano mkubwa sana, ukifika lazima uwatafute Watanzania nawapongeza sana *Diaspora* wa UK. Naomba niseme kwamba, sasa wanataka ili waweze kunufaika na hayo mambo ambayo yameelezwa hata na Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikihitimisha kabisa niombe niseme jamani tangu enzi za baba wa Taifa tumekuwa tukitetea nchi kujikomboa. Tumekuwa wasuluhishi wakubwa, sasa ifike mahali tuangalie Watanzania na sisi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili Mheshimiwa.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Beatrice kwa mchango wako, naona una uzoefu katika eneo hili. Waheshimiwa Wabunge naomba niendeleo na Mussa Haji Kombo.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi huu tulikuwa tunasheherekea miaka hamsini ya Umoja wa Afrika. Umoja wa Afrika uliokuwa ukiiwa *OAU* ulitusaidia sana nchi zetu za Afrika kuungana. Umoja wa Afrika huu umebadilishwa jina sasa ni *AU*. Kwa maendeleo ya sasa ingependeza zaidi umoja huu ukawa wa kiuchumi sasa, badala ya maneno, tuwe kama Waafrika siku zote tunavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungechukua mifano kama *EU*, haidhuru wametutawala sote, lakini sasa hii inazungumzia sana juu ya uchumi. Waafrika tuna *problems* kubwa, tuna maendeleo mazuri, tuna nyenzo nyingi sana za kujiendeleza, sasa tungeanza kuzipeleka hapa badala ya kukaa tu kila siku tukawa tunazungumzia matatizo ya nchi ambayo hayamaliziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia bajeti ya mwaka 2012/2013, maombi yake yalikuwa ni 93.3 bilioni. Maombi ya maendeleo yalikuwa ni 16.6 bilioni na matumizi ya kawaida ni 81.6 bilioni hadi tarehe 28 Februari, fedha za maendeleo zilizotolewa ni 6.6 bilioni maana yake bilioni 10 hakuna. Tunasema nini sisi, *are we serious?* Tuchangie nini na kwa mifano hapa tunaoneshewa kwamba, hatuhitaji kuendeleza maendeleo. Nafikiria tungejitahidi kidogo tukatazama maendeleo kwanza, halafu tukatazama mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri akija, anipe hesabu ya Balozi ngapi za Tanzania ziko ulimwenguni na katika Balozi hizo akatusaidia, kila Balozi anatoka katika nchi gani katika nchi mbili hizi zilizoungana ili

1 JUNI, 2013

nifahamu, inawezekana katika ule mgao wa 4.5 na Mabalози wanagawiwa hivyo hivyo kwa 4.5. Sasa nikifahamu hilo nitajua nini hali halisi ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalози wa Tanzania walioteuliwa nikimwomba Waziri kwa maana maalum aniambie ni Mabalози wangapi wanatoka Zanzibar basi, wa nchi nyingine kubwa kama hii ya Tanganyika, basi asitueleze, lakini atueleze wale wanaotoka Zanzibar. Atupe ufafanuzi kidogo ni wafanyakazi wangapi katika Balози zetu wanatoka Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri sana, hawa Maofisa wengine waliopo mwaka jana tulishawishika sana kule Zanzibar, tukawapeleka watu wetu kusoma katika diplomasia ili waweze kuajiriwa. Bajeti ya mwaka jana hawamo, bajeti ya mwaka huu hawamo inaonekana bado bwana mkubwa hajatoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya Upinzani ndani ya Bunge imezungumzia ulipaji wa *visa* kwenye Balози. Kwanza naomba Waziri anisaidie, Zanzibar ilitangazwa kwamba ni nchi yenye ugaidi na Serikali ya Muungano kupitia Waziri wake wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri atusaidie, imeharibika vipi biashara ya utalii kwa tangazo hili la ugaidi. Nini maana yake, nakusudia kusema watalii wengi duniani wakipata taarifa kama nchi ina ugaidi wanavunja safari zao kwa sababu ya kuogopa nafsi zao au afya zao au maisha yao yasiptotee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba hilo nipewe maelezo na Mheshimiwa Waziri tumeathirika vipi Zanzibar katika tamko hili la ugaidi.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri anisaidie haya mapato ambayo *visa* zinatoka nje, zinatoka ubalozi Zanzibar inapata fungu gani au ni ile 4.5 ambayo inatolewa na Serikali ya Muungano kwa Zanzibar inaunganishwa na yale mapato ya Ubalozi, nitaomba ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali sana kwamba Mheshimiwa Waziri ana uwezo mzuri, nakubali sana kwa sababu ni rafiki yangu wa muda mrefu, tunafahamiana tangu ofisi zetu zilivyokuwa, nakubaliana sana na Mheshimiwa Waziri, lakini nina tatizo dogo la kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wa Chama cha Mapinduzi waliomo humu ndani wakichangia husema naunga mkono mia juu ya mia. Sasa asilimia mia moja, naifahamu asilimia mia moja, maana yake haina tabu, haina mnukuo, haina chochote, ni safi, kama ni mtoto ka-*pass* kwa asilimia mia moja, ina maana kafaulu vizuri kabisa. Lakini maelezo yake ukiyasikia, basi ni balaa kubwa, sasa sitasema naunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu asilimia mia moja ningeunga mkono baada ya maelezo yangu kujibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa urafiki wetu tulionao asiwe na chuki ajibu kiusahihi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono. (*Makofi*)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mambo ya Nje. Kabla sijaanza kuchangia, naomba kwanza ninukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya bajeti ya

1 JUNI, 2013

mwaka 2011/2012, kwenye kitabu chake ambapo inapatikana kwenye ukurasa wa 29. Mheshimiwa Waziri alitumbia:

“Heshima ya Tanzania duniani na aliendelea kuelezea kwamba, kama nilivyoeleza awali nchi yetu imeendelea kujijengea heshima kubwa Kimataifa na Taifa lililokomaa katika nyanja za utawala bora, usuluhishi wa migogoro, demokrasia, utawala wa sheria, utawala unaojali haki za binadamu na utawala unaowekeza kwa watu wake. Hali hii imefanya nchi yetu kuzidi kuaminiwa na Mataifa mengine, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimenukuu kifungu hiki hasa pale alipozungumzia kwamba nchi yetu imekuwa ikiwekeza kwa watu wake, lakini tumekuwa tukiwekeza pia katika Mataifa mengi duniani na hasa kwenye Bara la Afrika. Kama tutakumbuka eneo moja ambalo Tanzania tuliwekeza kwa miaka mingi ni nchi jirani ya Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi jirani ya Msumbiji wenzetu walichelewa sana kupata uhuru, lakini nchi yetu ya Tanzania tulichukua jukumu la kuisaidia Msumbiji kuhakikisha kwamba wao wanapata uhuru, tukihakikisha kwamba, baada ya wao kupata uhuru, tutaweza kushirikiana nao katika mambo mengi sana, hasa ya kiuchumi, lakini vile vile hata suala la ulinzi litakuwa limeimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kile, kilikuwa ni kipindi kigumu sana kwa wananchi wa Mkoa ya Kusini. Tumelala kwenye mahandaki, tumepokea wageni wa kutoka Msumbiji, tumewakaribisha katika vijiji vyetu, na ukienda katika Mkoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma, utakuta kabisa kuna vijiji ambavyo ndugu zetu wa Msumbiji walipofika huku walitengewa maeneo wamekaa. Kwa mfano, Matekwe, Mheshimiwa Waziri anafahamu. Hii yote tulikuwa tunathamini kwamba, wale ni binadamu wenzetu na tuna haki ya kuweza kuwasaidia, na tumeendelea kuwasaidia katika miaka mingi hadi hivi sasa ninapozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatukuishia hapo tu, baada ya wao kupata uhuru, nchi yetu tuliona kwamba ipo haja ya kuunganisha mawasiliano yetu kati ya Tanzania na Msumbiji ili tuweze kuendelea katika shughuli zetu mbalimbali. Limejengwa daraja Mtambaswala kule Wilayani Nanyumbu, lakini vilevile kwenye Mkoa wa Ruvuma daraja limejengwa kwa ajili ya kwenda nchi ya Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza hapa, ni hali halisi inayoendelea kwa ndugu zetu wa Msumbiji. Sisi bado tumeendelea kuwapokea na wemeendelea kutumia huduma mbalimbali zilizopo katika nchi yetu. Kwa mfano, huduma za Afya, watu wanatoka Msumbiji wanakuja Mkoani Mtwara, wanakuja Masasi kuja kupata matibabu. Zahanati zetu zilizopo mipakani wenzetu wa Msumbiji wamekuwa wakinufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu cha kushangaza, kazi yote tuliyoifanya kwa miaka mingi ya kuhakiisha kwamba wenzetu wa Msumbiji wanapata uhuru, tukiwa na matumaini kwamba tutakuwa tumeshirikiana nao katika masuala ya kiuchumi, ninachooona sasa hivi, wanaonufaika katika hali hii, ni wenzetu wa Msumbiji wananufaika zaidi katika nchi yetu kuliko tunavyonufaika sisi kule Msumbiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalizungumza hili ili Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje aelewe ni nini wanachofanyiwa Watanzania wetu wanapokwenda

Msumbiji. Watanzania wengi wamekuwa wakitumia fursa hii kwenda Msumbiji kwa kufuata taratibu, vibali vyote vinavyotakiwa kwenda Msumbiji na wao wakienda kule kwa ajili ya biashara mbalimbali kama watu wa Msumbiji wanavyofanya wanapokuja Tanzania. Lakini ndugu zetu wanapokwenda Msumbiji, wameishia kupigwa, wanateswa, wananyang'anywa mali zao na hatimaye kufukuzwa na wengine wanakuwa wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, ninakuomba sana, suala hili limelalamikiwa sana na watu wa Mikoa ya Kusini, lakini ninaamini kabisa hata Watanzania wanaopata fursa ya kwenda Msumbiji, hali hiyo wamekuwa wakiiona.

Ninachoomba Mheshimiwa Waziri, ufanye mawasiliano na viongozi wenzako wa nje kule Msumbiji ili waone jinsi watakavyokuwa tunashirikiana vizuri kama ushirikiano wetu ulivyokuwa umeanza toka miaka ya nyuma kwa kutumia fursa hizi sote pamoja, bila kunyanyasana kama ambavyo sisi huku Watanzania hatuwanyanyasi wenzetu wa Msumbiji. *(Makofi)*

Hali iliyopo sasa hivi Mheshimiwa Waziri, kwa kweli kama itaendelea hivyo, wananchi hawataona maana ya kushirikiana na hawa ndugu zetu wa Msumbiji. Mateso yamekuwa ni makali mno, kwani watu wananyang'anywa mali zao. Vijana wetu wamekuwa wakitafuta mitaji midogo midogo wakidhani wakienda kule, pengine wanaweza wakakuza mitaji yao, lakini wameambulia kurudi wakiwa masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu ya msingi ilikuwa ni kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, afanye mazungumzo na nchi ya wenzetu Msumbiji, ili amani iliyokuwepo hivi sasa iweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Hoja yangu ilikuwa ni hiyo, kuzidi kuleta ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi ya Msumbiji. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimepokea taarifa kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa barua maalum hapa, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, hayuko ndani ya Bunge kwa majukumu maalum ya kichama na nafasi yake inakaimiwa na Mheshimiwa Ezekiel Wenje. Kwa hiyo, mtakapoonona kwamba hayupo kuchangia hapa, msije mkafikiri ameingia mitini, yuko nje kwa kazi maalum na Mheshimiwa Wenje anaendelea kushika nafasi yake.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2013/2014 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi uliotukuka. Pia nampongeza Naibu Waziri kwa uwezo mkubwa alioonyesha katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika hotuba ya Waziri ameonyesha dhahiri kuwa Serikali ipo makini kuhakikisha kuwa maeneo muhimu yanafanyiwa kazi na kuongeza ufanisi kiutendaji ili kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili ianzishe *electronic visa* haswa kwa nchi za Ulaya na Marekani. Hii itasaidia sana kukuza utalii nchini kwani utaratibu uliopo sasa upatikanaji wa visa unachukua muda mrefu na gharama kubwa kwa waombaji. Balozi zetu ziko mbalimbali sana kiasi cha kutoweza kufahamika kirahisi. Mfano mzuri ni nchi kama Hispania, Marekani kwa Majimbo ya Magharibi na Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu kumekuwa na hali ya wawekezaji kuja kuwekeza nchini na kuzua malalamiko kutokana na uwekezaji huo kutokidhi matarajio. Ili kukabiliana na hili, naishauri Serikali kwa kutumia Balozi zetu

1 JUNI, 2013

wafanye kazi ya uhakiki (*due diligence*) kabla ya makampuni haya kuja hapa nchini ili kuondokana na wimbi la makampuni ya kigeni kuja nchini na kutumia rasilimali zetu kama ardhi na madini kuweka dhamana za kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za makusudi zifanyike ili kuondoa hali mbaya kwa watumishi katika Balozi zetu nje ya nchi. Maslahi yao yatizamwe vizuri na yalipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iharakishe uthibitishaji wa Balozi ya *Trinidad and Tobago* kwani suala hili limechukua muda mrefu sana bila ya kupata suluhisho. Tuzingatie kuwa nchi hii imekuwa tayari kutoa msaada wa kitaalam haswa katika nyanja ya gesi na mafuta kwa uzoefu na utaalam walionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu kwa uwezo na uhai aliyonijalia na hatimaye leo naweza kutoa dukuduku langu, kero, maoni na ushauri kwa Serikali kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haiwezi kujitenga na mataifa mengine kwenye dunia ya sasa ndiyo maana Wizara hii ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninao wasiwasi na wenzetu wanaopewa nafasi wanapokuwa wamepata fursa ya kutuwakilisha nje ya nchi kama Mabalazi au Maafisa wa Ubalazi kwa idara mbalimbali.

Natamka haya kwa kulinganisha na wenzetu wanavyoyawakilisha mataifa yao ya nje ya nchi kwa mfano Kenya. Nchi ya Kenya inatambulika kwa vivutio vya utalii ambavyo havipo kwao lakini utangazaji wa nchi yao umekuwa mkubwa kuliko kwetu. Hii siyo tu inatokana na umahiri wa watu wao bali pia uzubaifu wa watu wetu.

Napendekeza sana uwepo mkakati mahsusi wa kutangaza vivutio vya utalii na huduma kama vile bandari vipatikanavyo katika nchi yetu kwa makusudi ya kukuza uchumi wa nchi na pato la Taifa. Hii kama itapuuzwa iko siku Watanzania wataanza kuhoji uwepo wa Wizara hii kama tutashindwa kukidhi ukuaji wa uchumi na pato la Taifa utakaokuwa unatambulika na Watanzania kuwa umechangiwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kuwa na ofisi za Ubalozi katika Miji Mikuu ya nchi za nje, napendekeza sana pia kuwepo na dawati la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika mipaka yote ya nchi (*border station*). Hii itasaidia kuwapa fursa wageni wenye matatizo kusikilizwa na dawati na mgogoro kama ni mdogo kutatuliwa kuliko kufika katika hatua za juu za utatuzi ambao ungefanikiwa kutatuliwa pale pale mpakani.

Nalisema hili nikiwa natambua uwepo wa idara nyingine nyeti pale mpakani ila dawati hili liwe tu kwa kuwasikiliza watu wa mataifa yote wanaotumia mipaka yetu na kuongeza ushirikiano na itasaidia sana kuongeza uingiaji na utokaji nchini wenye nia njema kwa ajili ya ukuzaji wa uchumi na ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa ofisi za Kibalozi miji ya kibiashara, natambua juhudi za Serikali katika kuanzisha ofisi ndogo za Kibalozi katika miji ya shughuli za kiuchumi ambayo Watanzania wengi wanakwenda. Ipo miji mitatu katika nchi ya China ambayo ni *Guangzhou*, Shanghai na Yiwu. Katika Miji hii Watanzania wengi sana wanaishi hapo na wapo wafanyabiashara toka Tanzania wanafika huko ila nasikitika huduma za Kibalozi ni duni na hazipo.

Napenda kujua juhudi za Serikali katika kupeleka huduma hizo katika miji hiyo ili huduma za Kibalozi zipatikane na kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kujua mipango ya Wizara ya kujenga katika viwanja vya Ubalozi tulivyopewa

1 JUNI, 2013

huko London, Dubai na kwingineko. Nategemea kupata majibu ya Wizara kutokana na mipango hiyo ikiwemo kupata hati katika jengo la Ubalozi nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwepo na hali mbaya sana ya uchakavu wa majengo katika baadhi ya Balozi zetu ikiwemo *Mozambique*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu wa fedha za viza, kumekuwepo na upotevu wa fedha nyingi sana kwenye uuzaji wa *visa* kwa kutumia mihuri ya kawaida badala ya *sticker*. Napenda sana kuishauri Serikali sasa ni vizuri kuhakikisha *visa* zote zitolewazo ziwe na *sticker* ili kuziba mianya ya upotevu wa fedha zitokanazo na uuzaji wa *visa* nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ngumu ya maisha Ubalozini, nasikitika sana kusema hali ya Mabalozini wetu huko nje na Maafisa wao wako katika hali ngumu sana kimaisha na wengine ilifikia muda wakawarudisha watoto wao nyumbani kwa ukosefu wa ada, hii ni aibu kwa Taifa. Kwa kuwa uchumi unakuwa basi ni vizuri kabisa uendane na hali halisi ya kuwahudumia watu wetu huko nje kadri uchumi unavyoruhusu. Ni vizuri kama Taifa kutafakari upya ni jinsi gani tunaweza kufunika aibu hii inayolikumba Taifa letu. Nategemea pia kupata ufafanuzi wa majibu kutoka kwa Waziri ni hatua zipi wanachukua kama Serikali aibu hii iondoke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe taswira ya mwonekano wa nchi yetu huko nje ni Balozi zetu kwa maana hiyo ni vizuri kuweka vema taswira ya nchi yetu kupitia Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa nami nichangie bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa bajeti nzuri yenye kuonyesha mikakati gani imewekwa ili kuendeleza ushirikiano kati ya Taifa letu na mataifa mengine katika nyanja mbalimbali. Kwa kufanya hivyo kutaifanya Tanzania iweze kupata fursa nyingi. Bajeti hii imelenga kutekeleza Iiani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya Watanzania waishio nje ya nchi yetu, wengi walikwenda huko kupata elimu na baada ya kuhitimu wakajikuta wakifanya kazi huko na hatimaye kupata uraia wa nchi hizo. Hiyo imetokana na nchi za wenzetu fursa kuwa nyingi, wafanyakazi wanalipwa vizuri lakini Watanzania hawa kilio chao kikubwa ni kuweza na wao kushiriki katika maendeleo ya nchi yetu lakini kikwazo kimekuwa ni uraia.

Taifa letu bado lina sheria ya kutambua uraia wa nchi moja tu kutokana na hilo Watanzania hawa kwa kuangalia fursa zilizopo kwenye nchi hizo ilibidi waombe urai wa nchi hizo za kigeni na hili si kosa kwani ni haki ya kila binadamu. Naomba Serikali itambue kuwa kutokana na tatizo hilo tunapoteza wataalam wengi waliopo nje ya nchi ambao wana uzoefu mkubwa katika mambo mbalimbali ambayo leo hii yangeweza kutusaidia nasi pia kwa kuruhusu uraia wa nchi mbili. Naishauri Serikali kulifanyia kazi jambo hilo ili nasi tuweze kufaidika na wataalam hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo katika ofisi zetu za Mabalizi, wafanyakazi wamekuwa wanafanya kazi kwa uzoefu tu, hapa tunahitaji mabadiliko kidogo kwani tuna vijana wetu waliomaliza vyuo katika fani za mahusiano ya kimataifa (*international relation*). Wataalam hawa wangepewa nafasi kufanya kazi katika Balozi hizi ili kuleta ufanisi wa kazi na kuboresha huduma katika Balozi zetu. Mabadiliko hayo yaendane pia na kuboresha ofisi za Balozi zetu pamoja na mishahara ya watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro uliojitokeza siku za hivi karibuni, mgogoro huo ni wa mpaka wa Ziwa Nyasa

1 JUNI, 2013

kati yetu na nchi ya Malawi. Napenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kusimamia kikamilifu mchakato mzima wa kutafuta suluhu ya mpaka huo. Naishauri Serikali kuendelea kutumia njia hizo hizo za kidiplomasia ili hiyo mipaka iweze kujulikana na hili jambo liweze kuisha pia kudumisha ushirikiano wetu na Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuweka utaratibu wa kuitangaza nchi yetu kupitia hizi Balozi zetu.

Kwa kufanya hivyo, itasaidia vivutio vyetu kujulikana na dunia na pia kuandaa utaratibu wa maonyesho madogomadogo ya bidhaa zinazotengenezwa na wajasiriamali wadogowadogo katika Balozi hizi, kufanya hivyo itasaidia kunyanyua kipato cha hawa wajasiriamali na kuitangaza nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nipongeze Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya kwa kuweka vizuri mahusiano ya nchi yetu na nchi nyingine hali ambayo imesaidia sana kuleta maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri na Naibu Waziri nawapongeza kwa kazi nzuri waendeleo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo changamoto au ushauri kwa Serikali, kwa kuwa uwezo wa Serikali ni wa wastani katika kuwapa *sponsorship* vijana wetu kwenda kusoma nje mfano *oil and gas* wako Watanzania ambao wamejitahidi kwenda kusomesha watoto nje kwa kozi mbalimbali na wanaporudi nyumbani Tanzania wanaishia ku-*report TCU*. Ndio mwisho wao lakini wengine wanabaki Ulaya wanafanya kazi zisizo na ujuzi waliosomea. Wanafunzi hawa hawana gharama kwa Serikali, wamejisomesha wenyewe kwa nini Serikali isifaidike na ujuzi wao?

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, misaada, michango, ufadhili na udhamini wa mataifa makubwa kwa Serikali ya Tanzania unatokana na kazi nzuri ya Wizara hii, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. JOHN S. MAGALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi za Wizara za kutambulisha vema nchi yetu katika mahusiano ya kimataifa. Pongezi maalum kwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kujenga urithi wa Taifa kuadikika kimataifa hivyo kuwa nuru ya mwendelezo wa mwenge wa uhuru ambao umevuka nje ya mipaka ya Taifa letu. Vivyo hivyo nampongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na timu yake yote ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania ina ushirikiano na nchi ya India na kwa kuwa nchi ya India ina ufadhili wa viwanda vya nguo Afrika, je, ule mpango wa kuwekeza kiwanda cha nguo ambao unavutiwa kwenda nchi ya Ethiopia dhidi ya Tanzania, sasa India imeamua msaada wake upelekwe katika nchi ipi kati ya Ethiopia na Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia kheri Mheshimiwa Waziri na timu yake katika kufanikisha mahitaji ya *APRM-Tanzania*. Je, kuna mikakati gani ya kuchangia mahitaji ya fedha na huduma za magari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo imekuwa ikisifika toka miaka ya 1960 kwa sababu kuu mbili, ilikuwa mstari wa mbele kabisa katika mapambano dhidi ya ubeberu na ukoloni na kuendelea kuwa kisiwa cha amani. Pamoja na mafanikio

haya, mimi nadhani Tanzania bado haijatumia vizuri fursa tulizo nazo kujitangaza na kutoa mchango kwenye nyanja ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ambayo Mataifa mbalimbali hutumia kujitangaza ni utamaduni na lugha. Ili kutimiza hili, Mataifa hayo huanzisha vituo vya utamaduni ambavyo vinakuwa vitovu vya kueneza utamaduni na lugha za Mataifa hayo. Mathalani, Uingereza ilianzisha *British Council* ambayo huhakikisha utamaduni na lugha ya Kiingereza inazidi kutangazwa na kuimarika. Ufaransa ilianzisha *Alliance Francais* na Ujerumani ilianzisha *Goethe Institute*. Vituo hivi kazi yake ni kueneza utamaduni na lugha za Mataifa yake, ni lugha za Mataifa haya hufundishwa katika vituo hivi. Viko vituo vingine pia, kituo cha Utamaduni wa Urusi, kituo cha Utamaduni cha Iran, India na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa kuanzisha vituo vya Utamaduni ni jambo linalohitaji rasilimali fedha na rasilimali watu ya kutosha, mambo ambayo huenda hayapo kwa wingi kwa sasa lakini kupanga ni kuchagua. Wakati tutajipanga kwa kuandaa mpango kabambe wa kuanzisha vituo vya Utamaduni na lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali, tunaweza kuanza kwa kuwa na Idara ya Kiswahili katika Balozi chache kwa ajili ya kuanzisha masomo ya Kiswahili kwa wageni katika Mataifa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza kuwa tuisubiri mpaka tujengeke kifedha. Tufahamu kuwa kuna ushindani mkubwa sana baina ya Kenya na Tanzania kuhusiana na nani "muuzaji" mzuri wa Kiswahili. Tanzania bado tuko mbele ya Kenya, lakini kwa kasi waliyonayo Wakenya, muda si mrefu watakuwa wametupita kama hatuchukui hatua makini za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nitakaloongelea ni tatizo tulilionalo la wakalimani. Hatuna wakalimani, ndiyo maana hata wanasiasa wanapotoa hotuba rasmi hulazimika kutumia Kiingereza badala ya Kiswahili. Ili tupate wakalimani inabidi tuwazalishe katika taasisi

mahususi – ambayo hapa nchini haipo. Wataalamu wa Isimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walishapendekeza kuanzishwa kwa Taasisi ya Tafsiri na Ukalimani Chuoni hapo lakini taasisi hiyo haijaanzishwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Nashauri Wizara ya Mambo ya Nje, ikishirikiana na Wizara ya Elimu na Serikali kwa jumla zikae na kuona namna ya kuanzisha Taasisi ya Tafsiri na Ukalimani ili tatizo la wakalimani litatuliwe. Halleti taswira nzuri kuwaona viongozi wetu wa Kitaifa wakitumia Kiingereza katika mikutano wakati Viongozi wa Mataifa mengine hutumia lugha zao zinazotafsirwa na wakalimani kwa Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii na natumaini Wizara itazingatia ushauri niliotoa.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabaki ya Mjusi huko Ujerumani *museum* (makumbusho) kurudi nchini. Kuna mabaki ya mjusi (Dainasoo) mnyama aliyesadikiwa kuwa mkubwa duniani, aliyeshi enzi za kale zipatazo miaka 200, ambaye hapa duniani mabaki ya mifupa yake imeonekana katika nchi tatu, Marekani – Los Angeles, Africa ya Kusini na Tanzania (Lindi, Mipingo, Tendeguvu). Inasemekana kuwa, mabaki ya Tanzania yalichukuliwa na Wajerumani na Waingereza mwaka 1910 na sasa mabaki hayo yapo huko na ni kivutio cha utalii nchini humo na huwaingizia pesa nyingi nchini mwao yaani Ujerumani na Uingereza nje ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, sisi Watanzania tunasaidiwa kutokana na fedha inayopatikana kutokana na mjusi huyo kuwepo Ujerumani na Uingereza nje ya nchi ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mimi Fatuma Mikidadi, nimekuwa kila mara nikiuliza swali Bungeni kuhusu mjusi huyo na mpaka sasa wananiita Mama Mjusi, hivi kwa nini nisipelekwe Ujerumani na Uingereza kwenda angalau kuiona mijusi hiyo ya Lindi kama historia tu, maana hatutegemei kupata chochote kutoka huko kwenda Lindi, Mipingo, Tendeguru, angalau kwa siku moja tu?

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara haiwashawishi Wajerumani kuleta miradi ya maji huko Mipingo au ujenzi na shule kama fidia ya kuchukua mali zetu, kupeleka Ujerumani na Uingereza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii iwashawishi Wizara ya Maliasili na Utalii, Kitengo cha Mali za Kale kufuatilia suala zima la mji wa Tanzania, Mipango- Tendeguru, Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Spika, bado mkakati wa diplomasia ya uchumi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa haujakaa vizuri. Kuna upungufu mkubwa wa kimuundo na kiuratibu katika eneo hili. Kuna haja ya Wizara kurekebisha mfumo wake pamoja na kuongeza wataalam wa fani hii Wizarani na katika Balozi zetu zote.

Mheshimiwa Spika, ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri ya kuwaajiri vijana 18 waliosomeshwa na kuhitimu Chuo cha Diplomasia kutoka Zanzibar bado haijatekelezwa. Ili kuondoa malalamiko ya kila siku kuhusu kutotekelezwa kwa ahadi, hususan zinazohusu Watanzania wa upande wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri alifafanua ni kwanini ahadi hiyo aliyoitoa hapa Bungeni mwaka 2012 wakati akiwasilisha bajeti yake haijatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengine ni kuhusu uteuzi wa Mabalozzi wanaowakilisha nchi yetu nje ya nchi. Zanzibar ina Mabalozzi wanaokadiriwa kutozidi watano. Je, hatuoni sasa ni wakati muafaka Mheshimiwa Rais ashauriwe aongeze idadi ya Mabalozzi kutoka Zanzibar kuwakilisha nchi yetu nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, suala la Tanzania kujiunga na *OIC*, Serikali itujulishe ni hatua gani imefikiwa? Kwanini imechukua muda mrefu kwa jambo ambalo litaipatia nchi yetu fursa nzuri ya kimahusiano na kiuchumi?

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kufanya vizuri katika nyanja hii ya diplomasia na mahusiano yetu na Mataifa mengine. Heshima ya Tanzania bado ipo juu. Napongeza pia hatua za kuongeza uwakilishi wetu nje.

Mheshimiwa Spika, napendekeza tena kwa nguvu, Tanzania kuikaribisha nchi ya Israel kufungua Balozi yake hapa nchini kwa sisi kuanza kufungua Ubalozi Tel Aviv/Jerusalem. Mahusiano kati ya nchi hizi ni mazuri, lakini yataboreshwa sana kama Tanzania itafungua Ubalozi nchini Israel. Hawa ni viongozi katika teknolojia nyingi zikiwemo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine ambayo Tanzania inapaswa kufungua Ubalozi haraka pia ni Korea ya Kusini (*Seoul*). Nchi hii inaipenda sana Tanzania, lakini urafiki unakuwa wa manati pale ambapo wao wana Ubalozi hapa sisi hatuna kule kwao.

Mheshimiwa Spika, napongeza hatua za kufungua Ubalozi Malaysia, Brazil na Comoro. Ni muda huu sasa Tanzania inapaswa kufungua Ubalozi pale Israel na *South Korea*.

Mheshimiwa Spika, nawatakia baraka tele za Mungu na mafanikio katika kazi zenu.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba umuhimu mkubwa uliopo katika uanzishwaji Balozi zetu zilizopo nje ya nchi, na nchi za nje kufungua Balozi zao hapa nchini, pamoja na faida za uhusiano wa nchi na nchi, lakini kubwa zaidi ni kuweka mazingira ya mawasiliano zaidi baina ya nchi na nchi kupitia Balozi hizo na pia kuwapatia urahisi wananchi wa nchi hizo kupata *Visa* za meli husika wakati wanapohitaji kuzuru nchi zenye mahusiano ya karibu.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa mimi nataka Mheshimiwa Waziri atuambie ni sababu zipi za msingi zilizozifanya baadhi ya nchi ambazo zina Balozi zao hapa nchini zikaondoa huduma za upatikanaji/utoaji wa *Visa* hapa nchini na kuhamishia huduma hizi katika nchi za Kenya? Je, kuna makosa yoyote ambayo nchi yetu ama wananchi wetu waliyafanya na kupelekea Balozi hizo kuhamisha huduma hii muhimu kuhamishwa katika nchi jirani?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali izishauri nchi hizo zenye Balozi zake hapa nchini zizingatie utoaji wa *Visa* upatikane hapa nchini na kama kuna tatizo lolote lililojitokeza lirekebishwe ili ufanisi wa jambo hili upatikane.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuiomba Serikali iziangalie kwa makini Balozi zetu zilizoko nje ya nchi, kwani kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya Balozi zetu ziko katika hali mbaya kutokana na ufinyu wa bajeti zinazopatiwa, kwani lazima tuelewe kwamba Balozi zetu zina majukumu makubwa ya kuiwakilisha nchi yetu, na pia kwa sasa yahitajika Balozi zetu zitangaze nchi yetu kibiashara pia.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka upande mmoja wa Muungano kwamba uteuzi wa Mabalozzi wetu nje ya nchi hauna uwiano na hata ukaribiano. Sababu hasa ni nini?

Je, ni kwamba upande wa Zanzibar wanakosekana watu wenye sifa za kuweza kuwa Mabalozzi au ni utashi tu wa Mamlaka ya Uteuzi unaamua unavyopenda? Mfano, hadi sasa, zaidi ya Mabalozzi 54 wa Tanzania walioko nchi mbalimbali duniani inasadikiwa ni Mabalozzi watatu tu wanaotokea upande wa Zanzibar. Hii haileti picha nzuri katika kudumisha uhusiano wetu na Muungano kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Serikali kuzitaka Balozi zetu kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa raia wetu wanaopatwa na matatizo mbalimbali nje ya nchi, kwani huo ni wajibu wao na ni moja kati ya malengo makubwa ya kuweko kwa Balozi hizo nje ya nchi, kwani kuna malalamiko

yameanza kujitokeza kwa baadhi ya Watanzania kukosa ushirikiano mzuri katika baadhi ya Balozi zetu wanapokwenda kutaka kupata msaada kwa matatizo wanayoyapata.

Mheshimiwa Spika, Mungu ibariki Tanzania. Ahsante.

MHE. ABASI Z. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, nina suala moja la sera kuhusu ajira. Tumepata nafasi za kazi nchini Qatar Doha. Kwa kuanzia, wanahitaji Madereva, *House Maid* na Wapishi. Visa zao zimekwama kwa Balozi wa Saudi Arabia. Sera ya Ajira Mambo ya Nje inasemaje?

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, kunakuwa na idadi kubwa ya vijana wazamiaji kutoka nchi yetu na sababu kubwa ya hawa vijana ni kutafuta ajira. Pamoja na Serikali kuchukua hatua mbalimbali, lakini kuna mambo matatu hayajafanyiwa kazi, nayo ni haya yafuatayo:-

(1) Utafiti ili kujua vijana wanaokwenda kuzamia wana ujuzi gani ili tuangalie upungufu tulionao ili kukidhi shida yao;

(2) Kuliimarisha Shirika letu la Meli ya ubia na China ili vijana wetu nao waajiriwe katika meli zao; na

(3) Kuimarisha Taasisi za Mabaharia ili ziweze kuratibu vizuri upatikanaji wa kazi katika nchi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kuboresha Balozi zetu, lakini kuna haja ya kuimarisha Balozi zetu ili ziweze kuhimili ushindani wa wawekezaji na kupanua masoko ya bidhaa zetu na ni vyema Serikali ikawa na kitengo maalum cha kushughulikia ukusanyaji na utawanyaji wa taarifa za wawekezaji za masoko yaliyoko nje na ndani ya nchi. Pia Serikali kwa kupitia Taasisi za Wafanyabiashara (*STAMICO*) na

NDC) ipate takwimu ya rasilimali zilizopo hasa katika Sekta ya Madini na Maliasili.

Mheshimiwa Spika, kuna Balozi nyingine zimekuwa hawatumii *Visa Sticker machine* kwa kisingizio zimeharibika au hawana, ni vyema Serikali ikanunua hizi *machine* na kuhakikisha kila Balozi wanakuwa na machine hizi za *Visa* badala ya kutumia muhuri. Ukosefu wa hizo *machine* zinasababisha upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Balozi ni mabovu sana na mengi mpaka hii leo hayajalipiwa kodi na *budget* iliyopewa katika Wizara hii ni ndogo. Naiomba Serikali walitizame jambo hili na ikiwezekana waongezewe hii *budget* na ile ya mwaka huu iliyobakia wapewe kabla tarehe 30 Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, migogoro yote utatuzi wake huwa kwenye mazungumzo (Mezani) wananchi huanza kupigana, lakini mwisho huja kwenye mazungumzo. Naipongeza Serikali yetu na ya Malawi walivyoamua kwenda meza ya mazungumzo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna haja ya Afrika kutumia umoja wetu katika kupinga au kuridhia maazimio kwa pamoja (*Block Voting*) hasa yale ambayo yataingilia uhuru wa ustawi wa nchi.

MHE. PHILIPA G. MTURANO: Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hotuba zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri, Kamati pamoja na ile ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, napendekeza maoni yote yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani pamoja na Kamati yazingatiwe na kupatiwa ufumbuzi kwa manufaa ya ustawi wa jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali iliyo zoeleka ya amani na utulivu katika nchi yetu, sasa hali hiyo imeanza kugeuka na kutishia amani ya nchi. Naomba Mheshimiwa

Waziri aeleze sasa, ana mkakati gani wa kuweza kurudisha imani ya Mataifa ya nje kuamini kwamba Tanzania kuna usalama ili tuendelee kuwa na marafiki kama ilivyokuwa awali na baadhi ya Mataifa ya nje.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa bado mgogoro wa Ziwa Nyasa kati ya Malawi na Tanzania bado haujatatuliwa. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, tumejipanga vipi? Hasa kwa kuwa Malawi wanaelekea hawataki muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuna watanzania wengi ambao wako katika Magereza mbalimbali nchi za nje. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaombea wafungwa hao warejeshwe nchini kutumikia vifungo vyao nyumbani? Ili waweze kupata haki zao za msingi za kuwasiliana na ndugu zao, na kama wapo ni wangapi basi ambao waliweza kupata uhamisho huo?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya 2012/2013 ya fungu la maendeleo ilikuwa ni ndogo sana kwa jumla ya Shilingi bilioni 16.6. Lakini kinachonisikitisha, hadi tarehe 28 Februari, 2013 fedha za maendeleo zilizotolewa ni Shilingi bilioni 6.6 tu. Je, ni kweli maendeleo ya kukarabati majengo yetu yaliyochakaa au uendelezaji wa viwanja vyetu, au kununua nyumba zinazohitajika itawezekana, kwa upungufu mkubwa wa fedha za maendeleo Shilingi bilioni 10 kutotolewa kabla ya miezi mitatu ya Bajeti kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, diplomasia ya kiuchumi (*economic diplomacy*) inapaswa kupewa nafasi kwa kuwezesha Balozi zetu nje, kwa kuwapatia fedha za kutosha za kufanya makongamano ya kutangaza vivutio vyetu Tanzania, shughuli za utalii wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozzi wetu na Maafisa Balozi zetu nje wanakuwa na wakati mgumu katika kutekeleza azma ya diplomasia ya kiuchumi. Pia Balozi zetu

zina uhaba wa wataalam wa fani za masoko na *investment* katika dhana ya diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni kwanini mnachukua muda mrefu kutowarejesha watumishi waliomaliza muda wao kwenye Balozi kwa kisingizio cha fedha huku mkitambua wazi muda wa kumalizika kwa muda wa watumishi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze, ni kwanini tuna maeneo mengi hatujawasilisha hati za utambulisho (*credentials*)? Mfano, Ubalozi wa Cairo Misri. Eneo la uwakilishi ni Misri, Israel, Lebanoni, Palestina, Libya, Iraq, Syria na Jordan, lakini ni Misri pekee ndiyo tumewasilisha hati. Je, ni lini Mataifa yaliyobakia tutawasilisha hati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo/kiwanja nambari 19 *Reneword* Uingereza hakiendelezwi na kuna hatari ya kunyang'anywa. Je, Serikali inasema nini?

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia. Napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii muhimu ambayo imeweza kutuwekea mazingira mazuri ya mahusiano na Mataifa mengine nje. Ukweli ni kwamba, wapo Watanzania wengi nje ya nchi yetu ambao wamekuwa waki-*enjoy* mahusiano mazuri huko waliko na kufanya shughuli zao bila bughudha yoyote. Pia tumekuwa na wageni wengi nchini mwetu, kama watalii, wawekezaji, wanasiasa, Viongozi Wakuu wa Serikali na kadhalika. Hayo yote ni kutokana na jina zuri au mazingira mazuri yaliyoandaliwa na Wizara hii na kuleta sifa kwa Taifa letu huko nje. Nawapongeza sana. Natambua Bajeti ndogo au ufinyu wa kamkate wanayopata, lakini bado wanajitahidi hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwepo au nilipata bahati ya kuhudhuria Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika – Addis Ababa. Kweli Mheshimiwa Waziri wa Mambo

ya Nje Mheshimiwa Membe, alionyesha umahiri mkubwa pale nilipoona anawasilisha kwa Mawaziri wenzake mambo ya Tanzania. Lakini, Mheshimiwa Rais wetu alitia fora na aliwasilisha kwa umahiri na kujiamini na nchi yetu tuliokuwepo tulikuwa *proud*. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, natoa ushauri kama ifuatavyo:-

(1) China ni kubwa sana. Nashauri kuwe na vituo vidogo vya Ubalози kila Mji Mkuu wa Majimbo.

(2) Fedha zipelekwe kwenye Balozi zetu, mfano, pango la nyumba Ubalози kushindwa kulipa, ni aibu ya Taifa. Mfano Ubalози wa India.

(3) Kuwe na dawati Wizarani la wana-*diaspora* ili kuwasaidia kwa mambo ambayo tumekubaliana wafanye hasa kuwekeza, kuajiriwa nyumbani, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

MHE. SAID SULEIMAN SAID: Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Wizaru kwa jitihada zake za kuendelea kuratibu uhamasishaji na ushirikishwaji wa Watanzania waishio nje ya nchi (*Diaspora*) kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kasi ya mchakato wa kupatikana sera ya *Diaspora* uende haraka zaidi, uweze kukamilika na kutoa fursa kwa Watanzania waishio nje ya nchi kuchangia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano kati ya Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi ziboreshwe.

Mheshimiwa Spika, naomba sura ya Utumishi kutoka Wizaru hii iendane na sura ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Wizara ya Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar. Ni wazi kwamba Wizara hii haiwatendei haki wahusika wa Muungano walioko upande wa pili wa Muungano wetu. Ni vyema sasa upande wa pili wa Muungano ukaangaliwa upya kuondoa manung'uniko na masikitiko yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadai kwamba Serikali ni mbili, lakini Serikali ambayo ina mamlaka na madaraka ya nje na ndani ni ya Jamhuri ya Muungano tu na hasa hasa juu ya mambo ya nje. Hili siyo sawa, kwani katika Muungano wetu hatukuiondoa kabisa Serikali ya Zanzibar, hivyo, siyo sahihi Serikali hiyo kuikoshesha fursa ya kuweza kupata misaada kutoka nje kwa ulazima wa kwamba misaada hiyo mpaka ipate baraka kutoka Jamhuri ya Muungano. Hii ni njia ya kuwadumaza Wazanzibari kimaendeleo pamoja na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwaeleza Wazanzibari ni uwiano gani uliotumika katika uteuzi wa Mabalozzi baina ya Tanganyika na Zanzibar hasa ikitiliwa maanani kwamba suala hili ni la Muungano na Serikali yenye mamlaka na madaraka ya kuteua Mabalozzi ni Jamhuri ya Muungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Wazanzibari hawana Wawakilishi wa kutosha nchi za nje kama Mabalozzi ambao watakuwa wanaiwakilisha moja kwa moja bila kupitia Tanzania Bara, hivyo ni maendeleo gani yatakayopatikana Zanzibar? Tumeshachoka vilevile kupewa nafasi chache za Mabalozzi wadogo Zanzibar, tunahitaji kuwa na Mabalozzi watakaoweza kuwakilisha Tanzania, lakini vilevile kuiwakilisha Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefanya ziara ngapi tokea kuteuliwa kwake? Amechukua Ujumbe wa watu wangapi? Ni wangapi walitoka Tanzania Bara na wangapi aliwaunganisha safari zake kutoka upande

wa pili wa Muungano, yaani Zanzibar? Ni faida zipi zilizopatikana kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Tanzania Zanzibar? Je, ni wastani wa asilimia ngapi zilizobakia Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar?

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, kuhusu uchakavu na Bajeti Ndogo kwa Balozi za Tanzania; hali hii ni ngumu sana hadi inasababisha Balozi kushindwa kujiendesha. Mfano, Ubalozi wa Tanzania nchini Uganda ambako mimi na Waheshimiwa Wabunge wenzagu tulitembelea Ubalozi na kujionea hali ngumu ambapo hata maji ama chai ya rangi hatukupewa. Hali hii inatisha. Ubalozi hauna hata uwezo ili kuitangaza Tanzania na kutafuta masoko. Hata nyumba iliyotolewa na Uganda kwa Tanzania imeshindikana kukabaratiwa.

Mheshimiwa Spika, Diplomasia ya Uchumi (*Economic Diplomacy*) ni dhaifu. Balozi zetu ziwezeshwe kwa kuongezea watumishi na wanataaluma wengine ili waweze kutekeleza hitaji hili kwa umadhubuti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uraia wa Nchi mbili (*Dual Citizenship*), ni vyema suala hili lifanyiwe utafiti kwanza bila uharaka ili kudhibiti wimbi la ugaidi linalozidi kuongezeka nchini. Pia wale wachache wanaostahili wabainishwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inajiandaa vipi kuzuia/ kudhibiti utoaji wa vitambulisho vya Kitaifa kwa wageni wanaohamia nchini au wenye nia mbaya ya kuhamia kiharamu?

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuwasilisha Bajeti yao, japokuwa ni finyu sana ukilinganisha na majukumu waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo ningependa kupata ufafanuzi wake. Kwanza, Sera ya Diplomasia ya Uchumi. Kwa kuwa Sera ya Diplomasia inaongozwa na dhana ya Diplomasia ya Uchumi; na kwa

kuwa Serikali yetu ina Balozi chache sana ukilinganisha na mahitaji; ningependa kujua Serikali inawashirikisha vipi Watanzania wanaoishi nje kama wadau katika utekelezaji wa Sera hii ya Demokrasia ya Uchumi; na je, tunawatumia vipi vijana wetu wanaoishi nje kutujulisha na kutufahamisha fursa mbalimbali ambazo kama Taifa tunaweza kufaidika nazo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa usalama wetu sasa hivi unakabiliwa na changamoto ambazo zinahusishwa na ugaidi (mikono kutoka nje); je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha suala la *Visa* zishughulikiwe na Balozi zetu badala ya kutolewa na Maafisa Uhamiaji katika Viwanja vya Ndege sababu kudhibiti wageni tusiowahitaji au hatari kwa usalama wa nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningepomba Serikali ichukue ushauri huu na ijaribu kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi sana, Watanzania wamekuwa wakinyimwa *Visa* kwa sababu za hisia tu; na kwa kuwa kumekuwepo na udhalilishaji, Watanzania kunyimwa *Visa* bila sababu ya msingi katika Balozi mbalimbali; kwa mfano; kuna kundi la Bendi ya Sanaa la hapa kwetu lilipewa mwaliko toka Serikali ya Finland na wakalipia gharama zote ili kwenda kufanya maonesho huko. Walipokwenda Ubalozini, vijana watano wakakataliwa kupewa *Visa* eti sababu hawana historia ya kusafiri nje ya nchi. Wakapatiwa *Visa* vijana wachache na iliwalazimu walipofika kule wawaingize vijana wengine toka Paris waje waungane kufanya shoo hiyo. Je, hiyo siyo dharau? Serikali yao imewaalika na kuwagharamia halafu Ubalozini unawakatalia; hiyo ni kutafuta aibu. Sasa huko siyo kuwalazimisha vijana wetu kutumia njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali ilianganalie suala hilo kwa sababu yapo malalamiko mengi sana mbona Balozi zetu au wakija katika viwanja vya ndege hawapati udhalilishaji huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dhana ya Diplomasia ya Uchumi utekelezaji wake umejikita zaidi katika kuvutia wawekezaji kutoka nje.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutekeleza Sera hiyo kwa kuwafungulia milango Watanzania kwenda kufanya shughuli halali nje ya nchi kama tunavyowatungulia wageni kuja nchini kwetu kufanya shughuli zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wawekezaji kutoka nchi za wenzetu wanaleta watu ambao hawana *qualification* kuja kufanya kazi hapa kwetu wakati wapo Watanzania wengi katika nchi zao ambao hawana ajira na wana utaalamu tosha. Kwa nini tusiwe na Sera ya kulazimisha Watanzania kufanya kazi hizo hapa kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko kwa baadhi ya Watumishi wa Balozi zetu kutofahamiana na Watanzania katika nchi wanazoishi; mfano, Ubalozi wa Sweden hawajawahi hata kufanya vikao na Watanzania wanaoishi Finland. Sasa nini faida ya Balozi katika nchi nyingine? Wanasingizia ufinyu wa bajeti, tunaomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zetu zinazungumzia nini juu ya mwanandoa aliyeoa au kuolewa nje ya nchi na anaamua kurudi nyumbani kuishi au kutembea? Tumeshuhudia wengi wakikosa vibali vya kazi na wanachukuliwa kama watalii, wanatozwa dola wakitaka kusajili kwenda Zanzibar na kadhalika. Wakati wenzetu wanatoa haki zote endapo Mtanzania ataoa au kuolewa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho; je, Wizara ina mpango gani wa kukuza Kiswahili nje ya nchi, pamoja na kuongeza ajira na kukuza lugha yetu? Tunao Walimu wa Kiswahili wanahitimu kila siku, uwepo mpango maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi zetu nyingi ni chakavu; ni lini Serikali itadhamiria kukarabati Balozi zetu? Vilevile Balozi zetu kasi yao ya kuitangaza Tanzania haiendani na wakati tulionao. Katika kuitangaza Sekta ya Utalii na vivutio tulivyo navyo nchini, Mabalozzi wetu wanatakiwa wachukue kigezo kwa nchi jirani ya Kenya; ni jinsi gani Kenya wameweza kujitangaza vizuri sana kuliko sisi katika Sekta ya Utalii, Ajira na Vivutio kwa Watalii na Wawekezaji Uchumi.

Kwa kuwa Zanzibar pia ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha Hotuba yake, aniambie ni Mabalozzi wangapi ambao wanaiwakilisha Tanzania kutoka Zanzibar?

Namwomba Mheshimiwa Waziri awafahamishe Watanzania ni Mabalozzi wangapi waliotokea Zanzibar ambao wapo kwenye Nchi za Bara la Ulaya, Amerika na Australia? Kuna dhana ambayo imejengeka kwa Wazanzibari kuwa, Mabalozzi ambao wanatoka Zanzibar wanapelekwa katika Nchi za Kiarabu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na usumbufu mkubwa sana wa upatikanaji wa *Visa* katika Ubalozzi wa Uingereza na *process* yake inakuwa ndefu. Kwa nini Ubalozzi wa Uingereza usiweke utaratibu mzuri wa Watanzania kupata *Visa* kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Watanzania kutohamasishwa katika uwekezaji; tunaomba Balozi zetu zilizopo nje, zijishughulisha na uhamasishaji kwa Watanzania waliopo nje ya nchi, maana baadhi yao wana mitaji ya kutosha kuja kuwekeza nchini. Pia tunaomba Mheshimiwa Waziri, Wizara yako ishughulikie haraka suala la uraia wa nchi mbili (*Dual Citizenship*) ili kutoa fursa kwa Watanzania ambao wameshapata uraia wa nchi nyingine ili waweze kushiriki katika kukuza uchumi wa nchi na washirikishwe katika kupiga kura ya Uchaguzi Mkuu wakiwa huko huko katika nchi wanazoishi.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Idara ya Mambo ya Nje iliyopo Zanzibar huwa haishirikishwi katika Mikutano ya Kimataifa? Vilevile Viongozi wa Wizara hawatembelei Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar. OC inachelewa kuingizwa na ni jambo ambalo ofisi hukumbwa na ukosefu wa fedha. Kwa nini Balozi zetu hazijikiti katika suala zima la uchumi na kuweka wataalamu waliobobea ili wakatafuta wawekezaji ambao wanaweza kutumia fursa zilizopo nchini na vilevile fursa za kuuza biashara zetu katika nchi ambazo Balozi zetu zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo gani linalosababisha fedha ambazo huidhinishwa na Bunge hili katika Bajeti ya Wizara hii huwa zinatolewa kwa kusuasua na kusababisha ucheleweshaji wa Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizocheleweshwa ni pamoja na shilingi bilioni kumi, ambazo hadi tarehe 28 Februari, 2013 zilikuwa bado hazijatolewa. Je, kutengwa bilioni 16.6 kwa bajeti ya mwaka uliopita na kutolewa *only 6.6 billion* ni uungwana na kuitakia mema Wizara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko wapi na tunalichukulia vipi suala la *diaspora* kwa masilahi yao na masilahi yetu? Majengo yako taabani; je, hivi kwa nyongeza na kutopatikana fedha kwa wakati tunaweza kweli kujikwamua na matatizo yanayokabili majengo yetu yanayotumiwa na wanadiplomasia wetu?

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 60, 70 na hata 80, dunia ilikuwa katika vita baridi baina ya kambi mbili kubwa; Mashariki na Magharibi, licha ya kuwepo kambi ya nchi zisizofungamana na upande wowote ikiwemo Tanzania. Licha ya nchi yetu kutofungamana na upande wowote duniani, lakini kutokana na siasa yetu ya ndani ya ujamaa na kujitegemea ilionekana kana kwamba, sisi tuko Kambi ya Mashariki.

Kwa vyovyote, uhusiano wetu nchi za nje uliathiriwa na kambi hizo mbili za wakubwa wa Dunia; Urusi na Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Kambi hizo uzito wao umepungua sana hasa Kambi ya Mashariki. Kwa hiyo, hivi sasa kinachoangaliwa Duniani ni uchumi; kwa hiyo ni diplomasia ya uchumi inayohitajiwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi zetu zikoje huko nchi za nje kuhusiana na diplomasia ya uchumi? Mabalozzi wetu wanaitekeleza vipi diplomasia ya uchumi huko Duniani na faida gani za waziwazi tulizozipata kutokana na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni ya Muungano, inavyoonekana hakuna uwiano wa Mabalozzi wetu walioko nchi za nje baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Hali hii haileti sura nzuri kwenye Muungano wetu. Mabalozzi na Watumishi mbalimbali katika Balozi zetu ni wachche mno kutoa Zanzibar nikilinganisha na Tanzania Bara. Je, Wizara ina mpango gani wa kuirekebisha hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya makazi na huduma nyingine kwa Mabalozzi wetu na Watumishi wengine huko nchi za nje hairidhishi hata kidogo. Hii inatokana na bajeti finyu iliyoko katika Wizara hii. Ieleweke Balozi zetu zilivyo huko nje ndiyo picha halisi kwa nchi yetu. Hivyo basi, ipo haja ya makusudi Wizara hii ifikiriwe upya na Wizara ya Fedha kwa kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ili iongezewe bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. ANNA MARY-STELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu, kwa kuniwezesha afya. Nianze moja kwa moja kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa KimaTaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji wa wanawake na kukoseshwa haki sawa kwenye elimu, kazi na uwezeshwaji, bado suala hili linaendelea katika nchi nyingi hapa Duniani. Migogoro mingi ambayo imekuwa ikitokea katika nchi nyingi kama vile migogoro inayotokana na Kisiaza, Udini na Ukabila.

Hii imekuwa ikiathiri hasa wanawake na watoto, yanapotokea mapigano na mauaji wanawake wengi wamekuwa ndiyo waathirika wakubwa na watoto kwa kuuawa na wengine kuingiwa na uwoga moja kwa moja kujitokeza katika masuala ya kimaendeleo, ikiwemo elimu, hivyo kukosa kazi na uwezeshwaji na hivyo kubakia na maisha duni. Ushirikiano huu unatakiwa kwa dhati kukaa pamoja na kujadiliana suala hili kwa upana ili kuhakikisha nchi zote wanawake na watoto wawe na matumaini ya amani na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Dunia ina wakati mgumu sana kulimaliza kabisa suala la VVU na UKIMWI, pamoja na kupungua kwa kiasi fulani, kwani kumekuwa na tatizo la uaminifu na uwazi hasa kwa wale ambao tayari wameshapata maambukizi na tayari wanatumia dawa za kurefusha maisha. Watu hawa wengi wanajificha na wanaendelea kuambukiza kwa makusudi kwa wengine ambao hawajapata maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, wageni wanatoka nje wanakuja kufanya kazi huku Tanzania, wanakuwa kwenye maambukizi tayari na wanatumia dawa za kurefusha maisha, wanapata marafiki huku Tanzania hasa wanafunzi wa kike wa vyuo vikuu na kuficha ukweli wao na kuanza kuambukiza hovy huku wakiendelea kufanya kazi za mkataba. Pindi wamalizapo mkataba wanaondoka kurudi nchini kwao na kuacha maambukizi. Je, Serikali kwa hili inaliongeaje katika Ushirikiano huu wa Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anijibu wakati wa majumuisho. Pia umoja wa Ushirikiano wa Kimataifa uhakikishe dawa hizi za kurefusha maisha zipatikane bila kukoma na zisambae kwa wingi hasa vijijini na mipakani vijengwe vituo vya ushauri nasaha na huduma zote zipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Mambo ya Nje ishirikiane na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ili waweze kujadili hasa masuala ya utamaduni wa

1 JUNI, 2013

kila nchi na kuhakikisha utamaduni wa nchi husika unafuatwa bila kupoteza tamaduni zao na badala yake zithaminiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika jitihada za kulinda amani duniani chini ya mwavuli wa Umoja wa Kimataifa. Bado suala la kuzingatia haki ni muhimu sana, kwani amani bila haki, bado amani ni ya kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi zinaingia kwenye migogoro au machafuko kutokana na tamaa, ukabila, udini na rushwa. Haya yote yanaweza kuondoa amani na kuleta machafuko. Hivyo, nashauli haki izingatiwe sana katika jamii kwani amani bila haki, amani haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa - Mheshimiwa Bernard Membe, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mahadhi Juma Maalim, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote, walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri, yenye mpango kazi wa kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake za juu za kuinadi nchi yetu pamoja na kutafuta wahisani mbalimbali kusaidia nchi yetu wakiwemo wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitampongeza Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, kwa kazi kubwa aliyofanya ya kusaidia nchi yetu kujulikana Kimataifa kwa kushirikiana na Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu Waziri; Mungu awabariki sana na awape nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ijitahidi kwa hali zote kukarabati majengo ya Balozi zetu huko nje ya

nchi mfano majengo ya Ubalozi wa China yamechakaa sana na kupasuka. Napenda kujua ni fedha kiasi gani zimetengwa kukarabati majengo hayo pamoja na Balozi zingine? Nasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo nchi mbalimbali ambazo tunashirikiana bali hakuna Balozi kutoka nchi, yetu jambo ambalo linasumbua Watanzania kupata *Visa* wanapotaka kwenda kwenye nchi hizo. Napenda kujua ni lini Serikali itateua Mabalozzi wengi kuwapeleka nchi ambazo hazina?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kutenga fedha za kutosha kupeleka kwenye nchi ambazo Balozi zetu zipo. Ninasema hivi kwa sababu fedha wanazopewa ni ndogo kiasi kwamba wanashindwa kutoa hata ukarimu kwa Viongozi na Watanzania wanaotembelea huko. Ninaamini kuwa, Mabalozzi wetu ni wakarimu sana, bali wanakuwa hawana fedha ndiyo maana hata likizo wanashindwa kurudi kwa kukosa fedha. Ninasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Watanzania wengi ambao wamekamatwa na kukabiliwa na kesi za kukamatwa na madawa ya kulevya; mfano, Nchi ya China wako karibu ya Watanzania 100. Hii ni aibu kubwa sana, ni muhimu Serikali iangalie njia ya kukomesha tabia ya namna hii ili kuondoa aibu. Ninaomba kupata maelezo ya Serikali ya kukomesha tabia hii mbaya inayoitia aibu nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna watu wanaingia nchini mwetu ambao hawana kibali na mara nyingine wanakuwa siyo watu wema. Naiomba Serikali kuimarisha suala la ulinzi ili wahamiaji hawa haramu kukoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninamalizia kwa kuunga mkono hoja hii na kuendelea kumtia moyo Mheshimiwa Waziri Membe, kukaza buti kwa kuchapa kazi, kwani kazi yake ni nzuri, hakuna sababu ya kuwasikiliza wale wanaokutaka kujuzulu wamekosa mada.

1 JUNI, 2013

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua ile fursa ya wanafunzi wa Zanzibar kwenda kusoma Chuo cha Diplomasia utekelezaji wake umefikia wapi; hiyo ilikuwa ahadi ya mwaka jana?

Mheshimiwa Naibu Spika, magari kwa Ofisi ya Zanzibar imefikia wapi ingawa ofisi yako tayari imenunua magari hayo na uliahidi pia Zanzibar watapewa. Naomba kujua hatua hiyo kwa Zanzibar imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Zanzibar ni jengo lililokuwa la Kiongozi wa upinzani, na aliondoka Zanzibar kwa kukimbia wakati wa Mapinduzi. Je, Wizara itajenga lini ofisi Zanzibar na je, kiwanja tayari kimetafutwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasikiliza hawa wachangaiaji, naomba sasa niwape nafasi Waheshimiwa Mawaziri waweze kujibu hoja zetu na tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri una dakika ishirini.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje. Naomba nianze kwa kuchangia baadhi ya maelezo yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani, halafu nitachangia pia baadhi ya hoja zilizoletwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.

Kwanza, naomba nigusie suala la kiwanja kilichopo Dubai kwa maelezo ya Kambi ya Upinzani, lakini pia na baadhi ya Wabunge wametaka kujua tunafanya nini kukiendeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, hatuna kiwanja chochote Dubai, na kwa maana hiyo hakuna

mpango unaofanyika wa kuendeleza kiwanja ambacho hakipo.

Kulikuwa na suala la magari kwa Ubalozi wetu uliopo China. Tayari Ubalozi wetu uliopo China umepatiwa magari na pia tumetoa magari kwa Balozi nyingine 19. Naomba niunganishe hili pia na suala ambalo liliulizwa kwa upande wa Ofisi ya Zanzibar ambayo nayo pia imeshapatiwa magari kwa kazi zake.

Kulikuwa pia na hoja ya kuanzishwa kwa Ubalozi Mdogo Guangzhou, jili limeletwa na Kambi Rasmi ya Upinzani lakini pia limeletwa na Waheshimiwa Wabunge wengine. Ni kweli kulikuwa na ahadi iliyotolewa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri iliyopita kwa Mji huu na Miji mingine ya kibiashara. Lengo lilikuwa ni kuimarisha mahusiano yetu na nchi hizo na pia kukuza biashara katika Miji ya kibiashara. Lubumbashi ilitajwa na Miji mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili hatukuweza kulitekeleza kwa mwaka huu, lakini bado pilika za kuanzisha Ofisi hizo zinaanza. Kilichofanyika na ambacho hakikuhidiwa kwa mara iliyopita, kama ilivyoelezwa katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kwanza kufungua tena Ubalozi wetu ambao ulifungwa kwa miaka mingi *the Hague* na ambao Kamati ya Mambo ya Nje ilikuwa inasisitiza na tukakubaliana juu ya umuhimu wa kufanya hilo. Lakini pia tumeweza kufungua Ubalozi Comoro.

Kwa hiyo, kadri hali itakavyoruhusu tutaweza kuongeza Balozi zetu sehemu mbalimbali na pia, kufikiria kuweza kufungua Balozi ndogo. Kwa hili la Guangzhou taratibu za kidiplomasia zinaendelea na zitakapokamilika tutaweza kuanzisha Ubalozi huo mdogo.

Kulikuwa na hoja ya kwamba, nafikiri inahusiana pia na jukumu letu katika Diplomasia ya Uchumi na Mahusiano ya Kimataifa kwamba, nchi yetu imegeuzwa kuwa kitega uchumi cha nchi zilizoendelea kwa kisingizio cha ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haiwezi kujitenga na dunia. Hivi sasa kila mmoja anajaribu kuvutia uwekezaji nchini kwake. Siyo kweli kwamba uwekezaji uchumi umekuwa na manufaa hasi kwetu, isipokuwa uwekezaji huu na juhudi nyingine zinazofanyika chini ya Serikali ndizo zilizoweza Tanzania kuingia miongoni mwa nchi kumi ambazo uchumi wake unakuwa kwa kasi zaidi duniani.

Kulikuwa kuna maelezo ambayo sidhani kama yanahitaji kuchukua muda mrefu, ambapo kumeelezwa kwamba, kitendo ambacho Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekiweka katika Ilani na inakifutilia, ile ahadi ya nchi zilizoendelea kuchangia sehemu ya uchumi wao, 0.7 ya pato lao la Taifa kuwa ni uvivu wa kufikiri wa CCM.

Kwanza, walioahidi hilo hatukuwa sisi, ni nchi zenyewe ndizo zimeahidi kwamba, zitatoa asilimia hiyo ya 0.7 ya pato la Taifa lao na chini ya makubaliano mbalimbali. Kwa hiyo, kukumbushia makubaliano hayo ambayo yametokana na ahadi yao wenyewe, siyo uvuvi wa kufikiri. Nafikiri ni kum-*quote out of context* Mwalimu Nyerere pale aliposisitiza haja ya kutumia rasilimali zetu. Mwalimu Nyerere hata siku moja hakusema kwamba hatuhitaji misaada katika kuendelea, ila alichosisitiza ni kwamba tunahitaji zaidi kutumia rasilimali zetu, na hicho ndicho kinachoendelea kufanyika hadi leo.

Pia, kulikuwa na maelezo walitaka Mheshimwa Waziri afanunue, kwamba kuhusiana na tukio la bomu la Arusha, na ambapo Kambi ya Upinzani imeeleza hapa kwamba, Balozi wa Vatican Tanzania alipeleka taarifa kwenye Baraza la Usalama, kuonyesha kwamba Tanzania siyo nchi salama.

Balozi wa Vatican Tanzania kwanza, hakupeleka barua hiyo. Aliyepoleka ni Balozi wa Vatican UN, na alichopeleka ni barua kueleza tukio hilo lilovyotokea. Hakueleza kwamba kulikuwa na ukosefu wa Usalama Tanzania. Wala hakusema kwamba, Tanzania siyo salama kutembelewa na wageni. Alichoeleza ni kwamba, ni kitendo cha kigaidi na kuomba Jumii ya Kimataifa iungane katika kupiga vita Ugaidi. Jambo ambalo sisi tunakubaliana nalo,

kwamba jamii ya Kimataifa lazima iungane popote pale kupinga vitendo kama hivi. (*Makofi*)

Pia, Kambi Rasmi ilitaka kujua nini kauli ya Serikali kuhusiana na tukio hilo? Kauli ya Serikali ilishatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, sidhani kama kuna haja tena ya Waziri wa Mambo ya Nje kulitolea kauli tena suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nigusie baadhi ya hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Kulikuwa na suala la Diplomasia ya Uchumi. Hili limeguswa na Kamati yetu ya Mambo ya Nje, ambapo kuna maelezo mbalimbali, wengi walitaka tuzidi kujipanga kutekeleza hili, tuonyeshe mafanikio ya Diplomasia ya uchumi na wengine walitaka tutume wataalam maalum wa Diplomasia hiyo ya uchumi kwa sababu inaonekana Maafisa wetu labda hawawezi kutekeleza jukumu hilo vilivyo.

Kwanza, tunatambua kwamba Diplomasia ya Uchumi ni suala ambalo linagusa kila Nyanja. Lakini nieleze mbele ya Bunge hili kwamba, Wizara ya Mambo ya Nje ina wataalam waliobobea katika nyanja mbalimbali. Kwa hiyo, wanatekeleza majukumu haya na ufanisi ambao unaonekana wa kuweza kuongeza watalii nchini, kuongeza wawekezaji, wote wanaotokana na juhudi za Mabalizi na Maafisa ambao wako katika sehemu hizo.

Kwa kutambua kwamba siyo Maafisa wetu tu ndio wamebobea katika Diplomasia ndiyo wanatosha, tumeweka wataalam wehemu mbalimbali ambao tunaona ni muhimu katika sehemu hizo kuweza kuchangia suala hili la Diplomasia ya Uchumi. Mahali kama Geniva utakuta wataalam wa biashara wako pale, mahali kama Nairobi kuna kuwa na wataalam wa mazingira. Uganda kutokana na umuhimu wake, kuhusiana na Nile, kuna wataalam wa Maji. Sehemu nyingine tumekuwa tukiomba Wizara na Idara zinazohusika kutupa wataalam hao na sisi huwa tunaweka utaratibu tu, wataalam hao kuweza kufanya kazi katika sehemu mbalimbali.

Kwa hiyo, wazo la kuongeza wataalam ni zuri tunalichukua. Lakini napenda nilihakikishie Bunge hili Tukufu kwamba, tumekuwa tukifanya na pale ambapo tunahisi kuna utaalam maalum unahitajika, wataalam hao wamepelekwa.

Kumekuwa na suala ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, la Diaspora na uraia wa nchi mbili. Wapo ambao wamekuwa wakisisitiza kwamba suala hili sasa lifanyike haraka, lakini pia, wapo walioleta michango yao wakisema kwamba tuwe makini zaidi, kwani suala hili halihitaji kuharakishwa.

Tukiri kwamba, suala hili wakati linaanza kuletwa na Wizara lilikuwa na watu wengi zaidi ambao hawaliungi mkono. Hivyo ilibidi tuwe makini na kuhakikisha kwamba utaratibu huu unakuwa shirikishi zaidi. Tayari limefanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa, lakini pia Wizara imelipeleka hili kama moja ya mchango wake katika Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa upande wa Uraia wa nchi mbili. Kwa hiyo, tunatarajia punde itakapotoka rasimu ya Katiba labda suala hilo litakuwa limezingatiwa.

Kwa upande wa Diaspora hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa, mikutano mbalimbali ya Watanzania wanaoishi Ughaibuni imekuwa ikifanyika katika sehemu mbalimbali. Viongozi wetu Wakuu kila wanapopata fursa kutembelea sehemu hizo wamekuwa wakijitahidi kuhakikisha wanakutana na Watanzania wanaoishi nchi hizo kubadilishana mawazo, lakini pia kuwakumbushia mchango wao katika nchi yao waliyotokea au ya asili.

Kuna suala la hali mbaya ya Balozi zetu, nayo imezungumzwa na Waheshimiwa wengi. Ni kweli kuna Balozi ambazo majengo yake yako katika hali mbaya na yameelezwa na ambao wametembelea Ofisi hizo. Lakini hilo linatokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali. Pia, kadri inavyowezekana tumekuwa tukishukua hatua mbalimbali za kuimarisha hali ya majengo hayo na pale inapowezekana kuongeza baadhi ya majengo mapya. Mfano, utengenezaji

wa jengo la Maputo ambalo limetajwa hapa, ni katika hatua za kuimarisha majengo hayo.

Kambi ya Upinzani ilikuwa inashangaa kwa nini tunatumia Shilingi bilioni tatu kama sikosei au nne. Lakini imedhihirika kwamba kwa bahati mbaya jengo hilo hawajalifahamu. Nimshauri tu Mheshimiwa Waziri, kadri inavyowezekana awe anamchukua Waziri Kivuli katika Sehemu kama hizi ili kuweza kuondoa hizi fikra mbaya. Kwa sababu jengo ambalo wamelitaja kwa mfano, ni la ghorofa tisa. Hivyo siyo jengo dogo, na lilikuwa linahitaji matengenezo makubwa. Kwa hiyo, lazima gharama zake nazo zitakuwa ni kubwa, na lilikuwa halijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu sana.

Kuna suala ambalo lilikuwa *specific* limeulizwa kuhusu nini mwelekeo wa Tanzania, au sera yetu kuhusiana na uajiri na hasa kuhusiana na kuzuliwa kwa Visa za watu ambao walikuwa wamepata nafasi kufanya kazi za ndani na udereva *Qatar*. Tanzania sera yetu ni kwamba, Watanzania wafanye kazi, kwa sababu hiyo ndiyo inajenga utu na heshima yao, lakini kazi zile zenye heshima, ndani na nje kwa kuzingatia sheria za nchi hiyo.

Kwa upande wa *Qatar* kwanza tunatakiwa kuingia mkataba na nchi husika, na tulishakubaliana. Bahati mbaya ratiba za pande mbili, kwa tarehe tuliyokubaliana mwanzo kwa sisi kuingia mkataba na wao, upande wetu tukawa hatuna nafasi, tukapendekeza tarehe nyingine, na wao tarehe ile ikawa haikubaliani na ratiba yao. Kwa hiyo, bado tunatafuta watushauri tarehe nyingine ambayo ni muafaka na tuweze kwenda kuwekeana mkataba. Sasa utaratibu huo utakuwa ni rasmi na wataanza kwenda huko.

Kulikuwa na hoja ya *Prof. Kulikoyela Kahigi*, ambayo pia imegusiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati, kwamba Tanzania haijatumia vizuri kujitangaza kupitia vituo vya utamaduni na lugha. Ni kweli tunachukua ushauri huo, kwamba tunaweza tukaitumia fursa ya kujitangaza kiutamaduni na kilugha, kama ambavyo wenzetu

wamekuwa wakifanya. Lakini ni suala ambalo siyo kwamba Wizara hatujaliona, na tunalipa uzito unaostahili. Ni kweli tunahitaji wataalam zaidi, lakini tumeanza angalau. Tumeanza kwa kuwa na sehemu ya ufundishaji lugha ya Kiswahili, hadithi na Mabalozzi kutoka nchi mbalimbali za kiasia, lakini pia na dunia wamekuwa wakitumia fursa hiyo kujifunza lugha yetu pale.

Pia, tumeanza kituo kama hicho, kwa upande wa London. Kwa hiyo, tunaweza tukaona ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukakuza zaidi lugha yetu, kwa kutumia zaidi fursa hii ya kufundisha utamaduni na lugha yetu sehemu mbalimbali duniani.

Kulikuwa na suala ambalo limegusiwa na Waheshimiwa Wengi, ikiwemo Mheshimiwa Musa hapa, na Waheshimiwa wengi walioleta michango yao kwa maandishi kwamba Mabalozzi wangapi wanatoka Zanzibar? Ni suala ambalo nafikiri limekuwa likiulizwa kila mara na kila bajeti tumekuwa tukilipata.

Balozzi ambazo zilikuwepo kabla ya kuongezwa mbili ambazo tumezisema sasa hivi, au kurejeshwa ni ya *the Hague* na Comoro, tulikuwa na Balozzi 33. Sasa hivi jumla ziko Balozzi 35. Kati ya Mabalozzi walioko huko, kwa hivi sasa kuna Mabalozzi watano ambao wanatokea upande wa Zanzibar, Cairo, Stockholm, Muscat, na Abu Dhabi. Kuna Balozzi yupo NewYork lakini kwa utaratibu wa kituo pele yeye ni Makamu Balozzi, lakini *rank* yake ni Balozzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ambao wameshamaliza taratibu zote lakini hawajatajwa, Manaibu Balozzi (*Deputies*), watakuwepo mji wa *New Dell* India; na pia kutakuwa na Naibu Maskati ambao watatokea upande wa Zanzibar. Kwa hivi sasa hatuwezi kuwataja kwa sababu bado hawajatangazwa rasmi, lakini taratibu zote zimekamiliika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulinganisha na hilo pia kulikuwa na suala ambalo limegusiwa na watu wengi walioleta michango ya maandishi na pia liligusiwa na Kamati

ya Mambo ya Nje, kuhusu ahadi ambayo Mheshimiwa Waziri aliitoa katika Bajeti yake ya mwaka 2012 ya kuajiri vijana kutoka Zanzibar. Kwanza hii ilikuwa ni juhudi maalum ya Mheshimiwa Waziri kwa kukiri kwamba kuna haja ya kuongeza uwiano. Hilo alilikiri wazi, na hatuwezi tukafikiria tu kuleta uwiano huo katika ngazi ya Mabalozzi bila kwanza kujenga uwezo katika ngazi ya chini. *(Makofi)*

Kwa sababu hiyo ni kuondoa utaalam, na katika nchi ambayo inajitahidi, kwa wale ambao wanajua taratibu hizo, kwamba tuna Mabalozzi wengi wataalam na wachache ndio wale ambao wanakuwa *political appointees*. Kwa hiyo, unaweza ukasema, kwa kuleta *political appointees* ungeweza ku-cover hilo kirahisi. Lakini kama unataka kujenga utaalam, ni lazima kwanza ujenge kuanzia chini.

Kwa hiyo, kwa kulitambua hilo Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba atachukua vijana kwa idadi kubwa ambayo haijawahi kutokea tangu Wizara kuanzishwa kwa pamoja, ili waingie sasa katika kada hii na wakue katika Wizara hii na baadaye itaweza kuondoa hiyo *gap* iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia alisema kwamba, kwanza lazima waende kujifunza katika Chuo chetu cha Diplomasia. Sasa vijana hawa wamemaliza mafunzo yao jana. Sasa leo ukisema kwamba hakuna hatua iliyochulikuliwa, nafikiri ni bado. Wamemaliza jana, na kwa hiyo, sasa ndiyo hatua nyingine zitaendelea. Kwa hiyo, tayari ahadi hiyo imetekelezwa kwa vijana hao kupelekwa Chuo cha Diplomasia, ambapo wamemaliza, na hatua nyingine sasa zitaendelea ili kuweza kuondoa tatizo hili ambalo limekuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru, sasa ninaomba nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Mheshimiwa Bernard Membe, unazo dakika 40. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuwashukuru wote ambao wamechangia kwa maandishi na kwa kuzungumza. Michango yao mikubwa na mingi tutajaribu kuijibu kama alivyofanya Naibu wangu. Lakini nianze kwanza kutoa pongezi, ingawa mwenzangu wa Msemaji wa Upinzani, Waziri kivuli hakunipa pongezi.

Taarifa aliyotoa, ingawa ilikuwa na migogoro mikubwa, lakini ilikuwa *balanced*. Kuna mambo makubwa na mazito ameyasema, ambayo yanahitaji kujibiwa sasa, lazima ku-*appreciate*, na nitakwenda moja kwa moja katika mambo hayo. Kwa sababu katika shughuli hizi za Mambo ya Nje, unahitaji ku-*balance* masuala ya Utawala na masuala ya Sera za Mambo ya Nje, na alifanya kazi hiyo vizuri, ukiachilia mbali ukurasa wa nane ambao ulikuwa unamtoa jasho. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda nianze kwanza kwa kusema, lipo pendekezo la kutoa Visa Ubalozini; na waliochangia ni wawili, Mheshimiwa Wenje na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Mheshimiwa Wenje alisema, ni vizuri kabisa Visa zitolewa nyumbani na siyo Ubalozini; Mheshimiwa Kabati anasema, Visa kwa wageni wanaoingia nchini zitolewe Ubalozini, na mimi nasema, ni wazo zuri sana la Mheshimiwa Ritta Kabati, kwamba ni vyema Visa zikatolewa kule nje, na ningependa kutoa sababu zifuatazo:-

Moja, mgeni anapoingia kwenye nchi yetu, ni vizuri kuwe na chujio la kujua kama huyu mtu ni safi, kama huyu mtu ni gaidi, au ana makosa ya jinai aliyoyafanya huko nje. Ni vigumu sana mgeni atakapoingia Tanzania, au Namanga au Dar es Salaam, ukalifanya chujio, baadaye ukagundua hafai ukamrudisha kwa Ndege alikotoka. Ni vigumu sana akishaingia kuanza kufanya taratibu kumrudisha alipotoka. Wenzetu duniani, Balozi hizi ndiyo zinakuwa chujio, pale pana vyombo vyote vya ulinzi na usalama na pana wataalam.

1 JUNI, 2013

Kwa hiyo, tunapoomba mtu apatie *visa* kwenye Ubalazi, pale anapitia kwenye tanuru la kuchujwa, kama ni mtu anayestahili kuingia Tanzania.

Kuna siku tatu, siku nne, zinazowapa fursa watu wa Ubalazi kuangalia *records* za huyu mtu kama anastahili au hastahili. Ndiyo maana hata nchi kubwa kama Marekani, huwezi kuchukulia *Visa* pale Marekani. Utachukulia huku nje, pamoja na teknolojia yote. Ndiyo maana ninawaomba Wabunge wenzangu, tutaleta *paper* maalum.

Chujio ni Ubalazi. Sababu ya kukaa kule nje siyo kuangalia tu haki za Watanzania au maslahi ya Watanzania, ni pamoja pia kuhakikisha kwamba hatuleti fisi humu ndani, kenge, watu wengine wasiofaa, wanapitia kwenye tanuru lile. Hiyo ndiyo sababu moja. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Ritta Kabati, dada yangu, kwamba huu ndiyo utaratibu mzuri.

Sasa, fedha za maduhuli, zinazopatikana kwenye Balazi zetu, sisi hatuzili zile. Sisi zile ni Bajeti, na hii itajibu sehemu ya rafiki yangu Haji Musa Kombo. Zile fedha zote tunazozipata za maduhuli ya *Visa*, zinaingia kwenye Bajeti. Ndiyo maana hapa tunasema, kwamba katika kipindi cha mwaka 2012/2013 au 2013/2014, tunategemea kuingiza Shilingi bilioni 16, zinaingia kabisa kwenye mfuko wa *Treasury*. Sasa *treasured of course*, ndiyo inajaribu kugawa fedha kote, pamoja na Zanzibar.

Sasa, lipo suala la upotevu wa fedha za safari ya Mheshimiwa Rais, na rafiki yangu anasema, inakuwaje leo Waziri huyu huyu baada ya upotevu wa *3.5 billion*, bado anaendelea kuwepo, wakati wenzake waliondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siondoki kwa sababu ifuatayo:-

Watanzania mnanisikia mliko, hakuna hata senti moja iliyoibiwa. Niseme mara ngapi? (*Makofi*)

1 JUNI, 2013

Narudia tena kwa *record* ya *Hansard*, hakuna hata Shilingi moja kati ya *3.5 billion*, zilizoibiwa! Nitamke mara ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea, ni kwamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Waziri wake, na Naibu wake, waliposafiri kwenda Angola kwenye Mkutano, huku nyuma zikaombwa fedha za safari ya Mheshimiwa Rais, *3.5 billion*. Hazina ikaidhinisha.

Baada ya kuidhinisha, zikaingia kwenye *account*. Zilipoingia kwenye *account* ndiyo tukarudi! Tuliporejea, tukakuta fedha hizi tayari zimeshatoka Hazina, zimeingia kwenye *account* yetu. Lakini tukagundua kwamba, inakuwaje Katibu Mkuu ndio Afisa Masuuli, anapokuwa hayupo, fedha *3.5 billion* zinaidhinishwa na zinaingia kwenye mfuko kwa safari ya Mheshimiwa Rais, sisi wenyewe tukiwa hatupo.

Je, Mheshimiwa Wenje wewe msaidizi wako anaweza kwenda benki akachukua fedha bila wewe kuweka idhini yako, lakini akakuletea zile fedha? Hutajuliza hapo utaratibu wa benki ukoje? Lakini hazikuibiwa. Kwa hiyo, wanaume tulichofanya pale ni kuangalia utaratibu tu uliotumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuligundua kwamba, taratibu zile zilikosewa, sisi wenyewe wenye nyumba tulikuwa nje, tuliporudi fedha zote zile tunazo, na tukazitumia vizuri, na *Auditor General* aka-*confirm*. Lakini tukasema, kwa sababu tulikuwa nje, taratibu zile, mwanya ule unaweza ukatuletea hatari mbele ya safari! Ndiyo maana vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama, wakiwemo TAKUKURU, tukaunda Kamati, na niliunda mimi. Wakaunda Kamati wakachunguza, wakagundua kwamba hapa kilichotokea ni udhaifu tu wa utaratibu wa fedha, mwanya ule, lakini fedha hazikuibiwa. Sasa nitatokaje kwenye Wizara hii? (*Makofi*)

Wewe na mimi tupo mpaka mwaka wa 2015, tuna kazi za kuzifanya humu ndani. (*Makofi*)

Lipo suala la utekelezaji wa *Economics Diplomacy*, nalo hili limeliliwa, kwamba utekelezaji wa *diplomacy* unakwenda vibaya. Lakini mimi nadhani ni uelewa tu. Naomba nirudie tena kwa Watanzania, Wizara ya Mambo ya Nje, inayo majukumu mengi. Moja ya majukumu ambayo tumejipangia wenyewe, ni suala la *peace keeping*, yaani kulinda amani, suala la utatuzi wa migogoro, na lingine, kusaidia Wizara za Uchumi nchini, Biashara na Viwanda, Kilimo, Utalii, kuzisaidia kutafuta wawekezaji, kuzisaidia kuleta watalii, kuzisaidia katika shughuli ya biashara. Tumejipa wenyewe kazi hii, kwa hiari yetu. Tungeweza kufanya kama nchi nyingine. Nchi nyingine hazifanyi hiyo.

Sisi tumejitakia wenyewe, kwamba kwa kuwa tuna Balozi 31, ni vizuri kule tuliko, tutafute wafanyabiashara, tutafute nafasi za uwekezaji nchini, za ndani na za nje, ni vizuri kule tuliko, tu-*promote* utalii. Tumejitakia wenyewe. Kutoka ukurasa 26 mpaka wa 52 wa hiki kitabu changu, ndicho tulichoeleza, tulichokifanya mwaka mzima wa mwaka 2012.

Sasa kwa nini unayeuliza swali la udhaifu wa *Economic Diplomacy*, kwa nini hukusoma kwanza toka ukurasa wa 26, ujue tulivyofanya katika Kanda zote, katika nchi, na katika Balozi zetu, ukurasa 26 mpaka 52? Kwa nini tunasumbuana? Kwanini wewe Mheshimiwa hukuzisoma kwanza, ukaniunga mkono? (*Kicheko*)

Kwa hiyo, tulichofanya sisi ni kwamba, kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009, tunatoa sasa takwimu na orodha, wapi tumefanya kitu gani. Kutokana na ufinyu wa Bajaji, lazima nizishukuru Wizara, hasa Wizara ya Utalii. Wizara ya Utalii inatusaidia kutoa fedha kwenye Balozi zetu, na ninawaomba wasisite kufanya vile, kutengeneza *brochures* za ku-*promote* utalii kule nje. Kwa hiyo, kazi tunaifanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna suala zima la kuanzisha kifungu cha *APRM*, na sisi tunasema sawa kabisa. Napenda kumshukuru ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimiwa John Shibuda, alifanya kazi moja nzuri sana ya kuhakikisha tunapata fedha za kulipia, lakini pia alishiriki

1 JUNI, 2013

kwenye kikao chetu cha *Addis Ababa*, na aliona kazi nzuri iliyofanywa na Tanzania, iliyofunywa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kazi ilikuwa nzuri sana. (*Makofi*)

Sasa kilichobaki ni kazi ya Kitaifa ya kufuatilia yale yaliyosemwa, lakini ndugu yangu hapa anazungumza kwamba kuna taarifa za kufadhaisha, moja ni ya uchawi.

Ngoja niwaambie Watanzania. Nenda Nigeria, nendeni Kongo, nendeni Gabon, nendeni Sierra Leone, mkaelewe uchawi, mkakutane na vichwa vya fisi vinavyofanya kazi yake kwenye uchaguzi na sehemu nyingine. Hili suala ingawa tunalikemea na hatulikubali, lipo kwenye utamaduni wa Kiafirika. Wala ninaposimama kule nje sioni aibu na wala sioni fedheha nikiambiwa bwana, kuna watu walikuwa wanaamini katika uchawi katika Tanzania. *Continent* yote ina imani hizo.

Nataka niwaambie leo tena, nendeni China. Siyo kwa kusema hivyo siamini, lakini jambo hili lipo. Ndiyo wanasema Kamati za ufundi; jamani, lipo! Wala halipo Tanzania peke yake! Wala sioni aibu kama Waziri wa Mambo ya Nje, ninapokwenda kule wakisema wewe bwana una uchawi, nawaambia, timu yangu inakuja kesho, mtaona cha mtema kuni! Tatizo liko wapi? Lakini ukishaliingiza katika mambo mengine, ya uongozi, ya usomi, na vitu vingine unaweza ukasema hizo *metaphysics* siyo nzuri. Lakini wala siyo jambo ambalo la kulionea aibu. Limeanzia enzi za mababu zetu, sisi wasomi ndio tunaliondoa taratibu, ku-*introduce science*, lakini siyo kitu cha kuonea aibu hata kidogo.

Wewe ukikuta paka amechinjwa pale, wewe ruka tu uendelee na safari, wala usione aibu, ndiyo mambo yanavyokwenda. (*Kicheko*)

Sasa lipo suala hapa la rafiki yangu Musa Haji Kombo, limesemwa lakini naomba nisisitize, na limekwenda kidogo na Mheshimiwa Masauni. Sasa kilichotokea Zanzibar, na kilichotokea Arusha ni vitendo vya kigaidi. Lakini Zanzibar siyo nchi ya kigaidi, wala Tanzania siyo nchi ya kigaidi. Villivyotokea

vile ni vitendo vya kigaidi. Ni *isolated*. Wala siyo tabia. Kwa hili ningependa kulihakikishia Taifa, kwamba kwa yote mawili yaliyotokea, wala hayajaathiri, hatujawa bado na takwimu zinazoonyesha, kwamba yameathiri *influx*, yaani kuingia kwa watalii. (*Makofi*)

Ningependa kwa kuongeza hapo hapo, tuwe waangalifu wakati wa kutoa matamshi hayo. Kwamba sisi, vitendo vile vilivyotokea ni vya kigaidi, lakini nchi zetu siyo za kigaidi. Ndiyo maana Viongozi wa dunia wanakuja na wataendelea kuja, watalii wanakuja na wataendela kuja, kwa sababu kitabia, sisi ni nchi ya amani, siyo nchi za kigaidi ukiliganisha na wenzetu. Kwa hiyo, athari mpaka sasa hivi hatujapata na sidhani kama kutakuwa na athari hiyo. (*Makofi*)

Sasa, matumizi makubwa ya *protocol*, na niunganishe hapo na safari za Mheshimiwa Rais. Ni kweli kwamba katika kipindi cha miaka miwili mfululizo, sasa tulikuwa tunatumia Shilingi bilioni 15. Tunapata Shilingi bilioni 15 za safari. Sasa fedha hizi, wala siyo Wizara yangu inayozitumia zaidi, ni wageni wetu wanaoingia nchini. Kuna kitu kinaitwa *courtesy*, na tulipopata wageni wa Kimataifa ambao hawakuingia kwenye Bajeti; kwa mfano, ujio wa Rais Obama, au ujio wa Rais Xi Jinping, sisi hatukujua kwamba angekuja. Mtakubaliana na mimi kwamba ujio wa ghafla unapokuja, hatuwezi kusema bwana, kwa kuwa ujio huu hatukuuweka kwenye Bajeti, wasije, mpaka kwanza mwakani tukakapoweka kwenye bajeti. Itakuwa kichekesho.

Kwa hiyo, kinachotokea, Wizara tunaionba Serikali, tunaomba *Treasury* kwamba jamani tuna ugeni unakuja. Ugeni huu unahitaji kupanua ulinzi, unahitaji *courtesy*, mapambo, washabikiaji, magari ya kukodi, chai, chakula cha jioni, utamaduni, na vitu kama vile, vinakuwa *computerized* tunajua gharama, ndiyo tunaziomba. Hiyoy moja.

Pili, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, kuanzia mwezi wa Nane mwaka 2012, sisi Tanzania tulipata heshima ya kuwa Mwenyekiti wa nchi za *SADC*, kwa upande wa

Kitengo cha Usalama, Ulinzi na amani. Hii imesababisha tuwe na mikutano mingi ya dharura kutokana na matatizo ya *Madagascar, DRC* na ya Zimbabwe. Achilia mbali kwenda ku-*monitor* uchaguzi uliofanyika Zimbabwe. Lakini siyo hilo peke yake, tulipata nafasi pia ya kuwa Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Baraza la Umoja wa Afrika, na tumehudhuria vikao vingi, na Mheshimiwa Rais amekwenda kule na kurudi.

Siyo hilo tu, tumekuwa pia Mjumbe wa Kamati ya Kazi ya *Common Wealth, Ministerial Action Group* ya *Common Wealth*. Kwa hiyo, yote haya yalikuja ghafla ghafla katika kipindi cha mwaka mmoja, tukalazimika kutumia zaidi.

Kwa hiyo, mkusanyiko huu wa ziara za Viongozi kutoka nje, majukumu ambayo Mheshimiwa Rais Kikwete ameyapata na sisi Wizara tumeyapata katika kipindi cha mwaka mmoja mzima. Kumefanya matumizi ya *protocol* yawe makubwa, lakini yote yameainishwa, yote yamechunguzwa, na yote yanakwenda vizuri, hakuna wizi uliotokea pale. (*Makofi*)

Upo ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mangungu, wa kuanzisha *Electronic Visa* na Balozi kuhakiki Wawekezaji. Huu ni ushauri mzuri, tunauchukua, wala sina haja ya kueleza vizuri zaidi.

Kuna suala la kuongeza Mabalozhi toka Zanzibar, Naibu Waziri amelieleza. Tuna Mabalozhi watano, tuna Manaibu sasa wawili, tuna *Head of Treasury* mmoja, Vijana 18 waliokuja tutawa-*absorb*. Jana nimetunuku Vyeti vyao, na baada ya kutunuku vyeti jana mchana, sasa wataanza kuingia kwenye mchakato wa kuwapa mafunzo pale *Head Quarters* kabla hawajapelekwa duniani kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini baadhi ya nchi wameondoa huduma za *Visa* na kuhamishia nchi nyingine? Mheshimiwa Khatib Said Haji, ni swali zuri sana. Sasa nchi hapa ambazo zimetuathiri sana ni Canada ya Uingereza, na tumeziandikia, na tumefanya vikao, na tunaendelea kufanya

vikao. Sababu ya msingi iliyowafanya wahamishe, ni mwaka 1989 mpaka 1991, hali yetu ya hospitali nchini, huduma za hospitali walisema zilikuwa duni. Wakati ule tulikuwa tunapeleka wanafunzi wengi sana katika nchi hizi. Sasa kulikuwa na kitu kinaitwa *medical checkup* kwa ajili ya wanafunzi wanaokwenda nje.

Sasa Hospitali ambayo ilikuwa *designated*, iliyochaguliwa kwa ajili ya kuchukua vipimo vya wanafunzi wanaokwenda nje, hasa Uingereza na Canada, ilikuwa Nairobi. Kwa hiyo, kwa udhia ule, kwa ghafla tu na bila kushauriana na Serikali, ndiyo wakahamishia huduma za kutoa *Visa* Nairobi, kwa sababu wengi waliokuwa wanaosafiri kwenye nchi hizi walikuwa ni wanafunzi, na *medical checkups* zilikuwa zinafanyika pale Nairobi.

Tumekutana, tumewaambia kwamba haturidhiki na hali hiyo, na tunaomba huduma hizi zirudi nchi. Naahidi kulifuatilia suala hili na tutakapokutana tena nitakuwa natoa taarifa ya nini kinachotokea. Lakini ninakiri usumbufu wanoupata wananchi kutokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mtemvu alisema, wafanyakazi hasa wa ndani, walioko *Qatar* wamezuiliwa *Visa* zao Saudi Arabia, na hili ninaahidi kulifuatilia. Mheshimiwa Makamu wa Rais aliniarifu pia kuhusu tatizo hili, na mimi pamoja na Wizara yangu tutafuatilia kujua hasa kilichojiri ni kitu gani. Mheshimiwa Abasa Z. Mtemvu pia alisema, kuna wageni wengi sasa wanaingia hapa nchini na wanaleta Ukimwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunao ushahidi wa wageni wanaoingia hapa nchini na wanasambaza Ukimwi, tufahamishwe tu ili tuviarifu vyombo vinavyohusika, ikiwemo na Wizara ya Afya kuchukua hatua.

Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, alisema kuhusu kufungua Vituo vya Utamaduni katika Balozini hasa vya Kiswahili. Mheshimiwa Naibu Waziri amelizungumzia; hili ni jambo jema. Suala la Paris hili ndilo Mheshiwa Wenje alikuwa analizungumzia pia. Lakini kama alivyosema Naibu Waziri,

naomba nilirudie tena. Tunanunua majengo mawili kwa mpigo.

Ninarudia, tunanunua majengo mawili kwa mipigo. Tumeyapata kwa bei nzuri sana kwa sababu Serikali ya New Zealand ilijenga majego yake na ilinunua majengo yake moja ni ile ya ghorofa tano ambayo ni Ofisi na lingine ni jengo la ghorofa nne ambayo ni makazi. Lazima tununue vitu vile kwa sababu hadi sasa hivi tulikuwa tunakodisha kwenye jengo la Uganda. Kwa hiyo, tumepata majengo mawili kwa mpigo. Ukigawanya kwa mbili na majengo yalivyo imara naahidi kukuchukua Mheshimiwa Wenje huko Paris. *(Makofi)*

Ukiangalia uhodari wa majengo yale, wewe mwenyewe utashangaa kwa nini bei imekuwa ndogo kuliko ulivyofikiria. Ukiona imezidi Shilingi moja au Dola moja nitajiondoa mwenyewe kabla ya kufika tena hapa mwakani. Kundi la *TBA*, kundi la Maafisa wa Ardhi, kundi la watu wa lkulu, kundi watu wa Usalama, walimiminika kule mara tatu, kwenda kuangalia kama anachokisema Membe ni na Wizara yake ni sahihi au hapana. Wamerudi na *clear check*, wakasema mpango huu ni mzuri na hatuwezi kuuacha na lazima tununue majengo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa *4.6 million* tumeshazipeleka. Tumenuua kwa halali, bila kuchukua hata senti moja. Ndiyo maana nitaendelea kuwepo hapa, kutafuta majengo mengine ili tuweze kuhudumia watu wetu. Ni majengo mawili kwa mpigo. Hapa katikati ina pana kiwanja kikubwa aina hii; upande wa kushoto kuna jengo na sehemu nyingine jengo la kulala. Balozi anapita ndani kwa ndani. Sehemu za ku-*pack* magari zimo kule ndani. Wageni kama wewe ukija mna ghorofa ya tano ya kukaa kule ndani. Haijapata kutokea! Ndiyo namna yake! Hela hizi huwa haziliki, kwa sababu kuna vyombo vingi vinaniangalia hapa katika suala kama hili, hailiki hata senti moja. Tunafanya kwa uaminifu na kwa kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimebakiwa na muda gani.

MBUNGE FULANI: Bado.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: *Very good!*

Sasa, suala la kuwa na Mikutano ya Mabalozzi. Kamati ya Mambo ya Nje ilisema, na ninataka niwathibitishie. Kwamba kilichotokea ni hiki. Tulipokuwa tunapanga kuwa na Mkutano wa Mabalozzi mwaka 2012. Tulikuwa na Mabalozzi 19 wana-*retire*. Yaani wamefikia muda wao wa ku-*retire*. Tukasema hakuna sababu ya kuwa na Mkutano mwaka 2012, na watu wanao-*retire*, yaani baada ya kikao kile mwingine anakwambia nimebeba na masanduku yangu, kwaheri.

Kwa hiyo, *logic* tuliyoifanya siyo kwamba hatuoni umuhimu. Tukasema tuchague vijana wachapakazi wapya. Mheshimiwa Rais ameifanya kazi hiyo na leo hii tunamtangaza Balozi mwingine jioni. Tunatangaza Mabalozzi wote wapya. Sasa *it makes sense*, kwamba baada ya kupata safu ya Mabalozzi wapya hawa, sasa ndiyo mnakuta kuwapa (a), (b), na (c) na changamoto za kuzifanya wanapokuwa kule duniani, badala ya kumchukua Balozi wa miaka 68 ambaye ana-*retire* leo, kumpa Semina ya namna ya kufanya kazi na keshokutwa anarudi nyumbani kufuga kuku wake. Ndicho tunachokifanya!

Kwa hiyo, tumesubiri kwanza, na tunatimiza, tuna Mabalozzi wanne tunawatangaza. Leo mmoja anatangazwa, kwa sababu barua zile zinarudi kwa mujibu wa nafasi za nchi zile tulizoomba Ubalozzi. Sasa wanaturudishia. Jana wameturudishia moja ya China, tutamtangaza leo. Sasa tukishamtangaza, huyu ndiye wa kumpeleka kwenye Mkutano ambao tunatoa Sera zetu na kueleza nini kitafanyika. Kwa hiyo, siyo kama tulifanya uzembe, tuliangalia mbele. Nani tumpe semina? Sasa tutatoa Semina kwa Mabalozzi wapya. (*Makofi*)

Hali ya Majengo ni mbaya, ni kweli kabisa. Kwa hili ninaungana na wote mliozungumzia suala hili. Kama nilivyosema mwaka 2012, ninarudia tena. Mimi ninawashukuru

Bunge, naishukuru Kamati ya Mambo ya Nje na wote nyinyi, kwamba sisi huko nyuma hatukuwa tunapata Bajeti ya Maendeleo. Miaka mitano iliyopita ndiyo tulianza kupata Bajeti ya Maendeleo. Majengo yale 92 tuliyonayo, tuliyokuwanayo mengine toka mwaka 1963, ni kweli yalikuwa kwenye hali mbaya sana.

Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, alipoingia sasa kama Rais, na kwa kujua kwamba alikaa miaka 10, kama Waziri wa Mambo ya Nje, sikupata shida kumshawishi kwamba sasa lazima Wizara hii tuwe na bajeti ya Maendeleo. Kwa hiyo, ni kipindi cha miaka mitano tu tuliyopata Bajeti ya Maendeleo. Tunajitahidi kufanya mambo matatu.

Jambo la kwanza, kununua majengo mapya. Pili, kukarabati majengo ya zamani, lakini tatu, kusaidia kwa kadri ya uwezo wetu hata kule *Honorary Council*, au kwenye *General Councils*, kupata majengo ili wafanyakazi waishi kwenye majengo yao wenyewe. Kwa hiyo, ni mpango wa miaka mitano tu iliyopita, hatuwezi kuwa tumefanya *miracles*. Kama mnavyojua safari hii tumepata Shilingi bilioni 28, mwaka 2012 tulipata Shilingi bilioni 16, mwaka 2011 pia tulipata Shilingi bilioni 16. Sasa 32 na 28 ni Shilingi bilioni 62. Shilingi bilioni 62 zisingeliweza kuhudumia majengo 93 yaliyoko kote duniani. Achilia mbali kununua mapya. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mshirikiane tu na sisi katika kutuunga mkono katika kupata pesa za maendeleo ili tuweze kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimeulizwa swali. Kwanini fedha za Shilingi milioni 400, hili nalijibu mapema nisije nikaondolewa, Shilingi. Kwa nini hizi Shilingi milioni 400 zinatumika kwa ajili ya safari za kwenda Maputo na sehemu nyingine, badala ya fedha hizo kutoka kwenye mfuko mwingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni hili, kwamba kumbe upembuzi yakinifu unapofanyika, pesa zile zinatoka kwenye Bajeti ya Maendeleo, haitoki kwenye mfuko mwingine. Hawa wanaosafiri kwenda kwenye maeneo haya ni wale wanaofanya upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, wanayo haki ya

kuwa na *air tickets*, kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo; *ground travelling* kutoka kwenye Mfuko wa Mendeleo, na gharama za kufanyia upembuzi yakinifu, ndiyo maana kuna zile Shiligi milioni 400, zipo zinatoka katika sehemu ile. Lakini nitaeleza zaidi kama kutakuwa kuna suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo swali sasa linalohusu Rwanda. Hili niliseme, mmoja ameliandika vizuri sana, nataka niliseme kwa faida ya Watanzania na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku sita zilizopita, Serikali ya Rwanda, imetoa tamko la kuipinga au kupinga ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Alipokuwa kwenye kikao Addis Ababa, Mheshimiwa Rais Kikwete tarehe 26 Mei, 2013, alishauri Serikali ya Rwanda kwamba, kwa kuwa Serikali ya Rwanda ina vikundi visivyopungua 20 kwenye misitu ya Kongo, inayoipiga vita Rwanda; na kwa kuwa kikundi kimoja cha M-23 sasa hivi kipo kwenye mazungumzo kati yake na Serikali ya Congo, nchini Uganda katika Mji wa Kampala, chini ya Uenyekiti wa Rais Museveni; Mheshimiwa Rais Kikwete akapendekeza kwa Rais Paul Kagame, kwamba wakati huu sasa ni muafaka wa wewe Rais Paul Kagame kuamua kufanya mazungumzo ya amani ya *opposition* na akatoa sababu. (*Makofi*)

Sababu yenyewe ni kwamba, tangu mwaka 1997, miaka 16 iliyopita, Serikali ya Rwanda ilikuwa inajaribu kuwapiga *FDR*, yaani *The Front For Democratic Change* ya Rwanda, ilikuwa inajaribu kuwapiga vita, kwa muda wa miaka 16 hawawawezi.

Kwa hiyo, kama *solution* ambayo Rwanda inadhani, kama *solution* ya kuondoa upinzani Rwanda ni vita, wamefanya hivyo kwa muda miaka 16 na wameshindwa, na kwa hiyo, Serikali ya Tanzania yenye uzoefu wa kufanya mazungumzo haya kwa amani; tumefanya Burundi, tumefanya Rwanda, tumefanya *DRC*, tumefanya Madagascar, tumefanya Zimbabwe, tumefanya na Angola; kwa uzoefu huo tukawashauri ndugu zetu wa Rwanda,

1 JUNI, 2013

nendeni kwenye mazungumzo ya amani na wapinzani wenu. Sasa anaambiwa aombe radhi, amefanya matusi. Kwa nini? Kwa sababu huwezi ukaongea na wauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Isaac Rabin - Waziri Mkuu wa Israel, mwezi Novemba, 1995 alitamka hivi: *"We make peace and we negociatte with our enemies, not friends."* Tunatengeneza amani, au tunazungumzia masuala ya amani na kujadlii masuala ya amani na maadui zetu, sio marafiki. *(Makofi)*

Ni wajibu wa Serikali ya Rwanda kama inanisikia, kufanya mazungumzo ya amani na maadui, wasingoje kufanya mazungumza ya amani ya Tanzania ambao ni marafiki. Una-*avoid* nini? Kama Palestine na Israel wanaweza kuzungumza, wewe ni nani unayekataa kufanya mazungumzo na maadui zako? Mtapigana mpaka lini? Kama kwa muda wa miaka 16 mmepigana na mmeshindwa, mnashindwa nini? Mnaona aibu gani kuzungumza hata na wauaji mnaowaita hivyo? *(Makofi)*

Ningependa Serikali ya Rwanda ijue, kwamba Serikali ya Tanzania kwa tabia yetu toka wakati wa uhuru, tunatoa kipaumbele kwa mazungumzo ya amani kwanza. Hata hivi sasa tulivyokwenda kwa M-23, kuleta amani *DRC*, bado tumemhiza Rais Museveni afanye mazungumzo.

Ninaomba kumwambia Waziri mwenzangu na pamoja na uongozi wa Rwanda; Tanzania tunayo nia njema tu. Wetu ni ushauri, kama hamuutaki, uacheni. Lakini hamwezi kumwambia Mheshimiwa Rais wetu aombe radhi kwa kitendo cha ubinadamu na cha kweli kabisa cha kuwataka maadui mnaongombana mzungumze amani. Hatuwezi kufanya hivyo, na Mheshimiwa Rais hawezi kuomba radhi kwa jambo la kweli. Mnauana wenyewe! *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilitaka Watanzania walielewe hili, kwamba tunatakiwa kuomba radhi, eti kwa sababu ya ushauri wa kuwataka mahasimu waongee. Hatuombi! Tunachosema,

wazungumze na sisi tuko tayari kusaidia. Lakini wasianze sasa kunung'unika! Watafika mahali lazima wazungumze.

Ninazo dakika ngapi?

MBUNGE FULANI: Kumi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Ah, bado zipo. Yapo mengi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pia suala hili ambalo mmoja wenu alikuwa ameliuliza pia, suala la kwamba hatujajiweka sawa, vizuri katika utatuzi wa Malawi na alikuwa anaomba *progress report*. Sasa *progress report* nilishaitoa, lakini naomba nirudie tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba katika kesi ya Malawi, jopo la Wanasheria saba wa Kimataifa limeundwa. Marais Watatu wa *SADC* wakiongozwa na Rais Mstaafu Joachim Chissano wako pale.

Ni jopo la watu kumi. Jopo hili linakutana sasa, kuangalia ni namna gani wamwite Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, mimi, kwenda Maputo na hivyo hivyo kwa upande wa Malawi. Sisi wanne tutaitwa; Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje; Mwanasheria Mkuu wa Malawi na Waziri wake wa Mambo ya Nje tutaitwa pale Maputo. Tutakapofika pale, sasa tutapewa hadidu za rejea na namna kuendelea na kazi ya kutoa ushahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu hilo sasa litahama kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, kwenda kwa Wanasheria Wakuu wa Serikali ya Tanzania pamoja na Malawi. Sisi tutakuwa wasikilizaji wakati sasa masuala ya kisheria yanakwenda pale.

Tutakwenda hivyo mpaka kitakapoeleweka. Kitakachotokea, jopo lile sasa la Marais, pamoja na Wanasheria wa Malawi watatoa ushauri wao. Inawezekana

1 JUNI, 2013

ni ushauri wa kueleza kwamba sasa Tanzania kweli mnastahili kupata Ziwa nusu. Kwetu yatakuwa yamekwisha. Inawezekana ni ushauri wa kusema kwamba haya mambo ni makubwa, songeni mbele. Sisi tutakwenda. Inawezekana ni ushauri wa kusema tunaomba muda zaidi wa kuliangalia suala hili, hatuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninataka niwahakikishie Watanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, na Wizara ya Mambo ya Nje, tumeandaa ushahidi sawa na Mlima Kilimanjaro. Ushahidi ambao utatuhakikishia kabisa ushindi wa suala hili. Sasa hatuwezi kuyasema hapa wasije wakasikia na kujiandaa. Lakini nataka niwahakikishie tena. Kesi hii hashindwi mtu! Si tupo! Kesi hii hashindwi mtu! Maji yale ni yetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Msumbiji ilikwenda kwenye kesi ikashinda kupata nusu ya maji kwa ziwa hilo hilo, kwa nini sio sisi?

Kwa hiyo, mkae vifua mbele, tsubiri, *it is just a matter of time*, kazi itafanywa. Nina imani kubwa sana na Mwanasheria Mkuu - Jaji Werema pamoja na timu yake watakaongoza jopo la Wanasheria kutoka nchi hii kuifanya kazi ya kihistoria ya kutaka haki yetu kisheria itambuliwe ili watu wa kwenye Ziwa lile wajue kwamba wana haki kwenye nusu ya maji yale. *(Makofi)*

Sasa nilitaka niliweke hilo vizuri. Lakini pia liko suala hapa la *DRC*. Ninataka pia nitoe taarifa, kwamba kwa upande wa *DRC*, tulisema hapa nikiwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwamba tunakwenda kule.

Ninataka niliarifu tena tumeanza kwenda kule. Vijana wetu wako kule na wanafanya kazi kubwa na nzuri na wamepokelewa kwa shangwe kubwa sana. *(Makofi)*

Nataka niwaambie wananchi wa Tanzania, hata zile propaganda zilizokuwa zinapigwa, sasa tutazipunguza kwa kupeleka kikosi cha Waandishi wa Habari, ambao watoa

1 JUNI, 2013

taarifa rasmi kwa nchi yetu, badala ya kutegemea mitandao yenye propaganda ya kuwapotosha wananchi wetu au viongozi wetu kwamba mambo yanakwenda kombo kule. Tutapeleka kikosi cha waandishi wa habari nane ambao watakuwa kule.

MBUNGE FULANI: Na Wabunge!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Na Wabunge! Hapana. Labda Mheshimiwa Wenje. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutapeleka kikosi cha Waandishi wa Habari nane ili waweze kwenda chini ya Uongozi wa Jeshi, ili kunapotokea kitu chochote au jambo lolote Watanzania wapate nafasi kama ilivyokuwa kwa Comoro, kupata fursa ya kuliambia Taifa ukweli na mambo halisi yanayotokea pale kwenye eneo la *peace keeping* na *peace making*, eneo la Goma pamoja na Kivu, ili msipate tu habari kutoka kwenye mtandao, mpate habari kutoka kwa vijana wenu *committed* na *patriots* wanaokwenda kule. Waweze kutoa sura halisi ya mambo yanavyoendelea kule, badala ya watu kupandikiza maneno ya uwongo, picha za uwongo, sura za uongo, zikielezea kwamba pengine Wanajeshi wa Tanzania wanafanya vitendo vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu lina sifa kubwa, sifa nzuri, ambayo limepelekea kushinda kila vita, kwa sababu ya nidhamu yao ya hali ya juu sana. (*Makofi*)

Ningelipenda kuchukua nafasi hii kwa moyo wa dhati kabisa kulipongeza Jeshi letu. Lina vijana wenye akili, wenye utaalam, na wanaoipenda nchi yao, na wako tayari kuifia nchi yao na wako kule wanafanya kazi nzuri sana. Hongera Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Wanafanya kazi nzuri sana! Tutaendelea kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama mnavyojua, wengine tunao Darfur Askari zaidi ya 850 wanafanya kazi yao nzuri sana.

1 JUNI, 2013

Sasa hivi Kamanda mpya wa *UNAMID*, yaani *United Nation Missions in Darfur* ni Luteni Jenerali Meela, Mtanzania ndiye anayeongoza Majeshi kule. (*Makofi*)

Pia ningelipenda kusema jambo lingine, nimeandikiwa hapa. Hiyo kengele ya ngapi.

MBUNGE FULANI: Ni ya kwanza.

WAZIRI WA MAMBO NA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia suala la Darfur, ni vyema nijibu hoja moja ya Mheshimiwa Mbunge, nadhani ni mwanamichezo. Alikuwa anaulizia usalama wa wachezaji wetu wakakaokwenda Darfur kwa ajili ya mechi kule.

Ninaomba nikiri kwamba Wizara yetu bado haijapata uhakika mzuri wa usalama wa vijana wetu wanaokwenad Darfur, kwa ajili ya mechi ya soka.

Ninasema hivyo kwa sababu tatu. Sababu ya kwanza, Darfur hakuna hoteli nzuri ya aina yoyote ambayo wachezaji wanaweza kufika wakakaa.

Pili, wageni wote wanaokwenda Darfur, huwa wanapokelewa na magari ambayo ni *bullet proof*, na wanakabidhiwa *vests za bullet proof*.

Nimeshangaa mipango hii ya kupeleka wachezaji wa Tanzania bila maandalizi makubwa ya aina hii. Siyo kwa upande wetu, najaribu kujiliza swali, wale walioandaa michezo hii Darfur, huku wakijua hakuna hoteli; huku wakijua kwamba wageni wote wanaoingia lazima wapokelewe na vikosi vikiwa na *bullet proof vehicles* na *bullet proof* zao; huku wakijua kwamba usalama wa vijana na wengine wote unakuwa kwenye mashaka; bado najiliza busara iliyotumika katika kuchagua Darfur kuwa kiwanja kimojawapo kitakachotumika katika michezo hii ya Afrika.

1 JUNI, 2013

Mimi Wizara yangu pamoja na vyombo vinavyohusika, tutajitahidi kutoa taarifa ya awali kabla hatujatoa mapendekezo kinyume chake ili tuzuie uwezekano wa vijana wetu kuwatosha kwenda sehemu ambayo inaweza kuhatarisha usalama wao na hivyo kuleta fedheha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikomee hapo ili sasa tujibu maswali ya kwenye vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mtoa hoja, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe, ametoa hoja yake na imeungwa mkono. Naomba nimwite Katibu ili atupeleke kwenye hatua inayofuata!

KAMATI YA MATUMZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuketi, sasa tunaingia kwenye hatua inayofuata na sasa ni hatua ya Kamati ya Matumizi kwa Bunge zima na naomba sasa nimwite Katibu ili aweze kutuongoza.

Kif. 1001 *Administration and General...* Tshs. 8,315, 559,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni na kama muda utaniruhusu nimewaona wote mliobakia isipokuwa nafasi yangu inakwenda kwa Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Chomboh, Mheshimiwa Ezekiah D. Wenje na Mheshimiwa Musa Haji Kombo. Kwa hiyo, kama muda utaniruhusu basi wengine wote jicho la Mwenyekiti limewaona. Tunaanza na Mheshimiwa Mkosamali!

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naomba kuuliza swali moja la kisera kuhusu Wizara hii namna inavyokabidhiana madaraka hasa kwa Awamu ya Tatu na Nne. Serikali ilifungua kesi kuhusu aliyekuwa Balozi wa Italy, Profesa Mahalu kwa tuhuma mbalimbali. Serikali ilivyofungua kesi ile Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa akaenda Mahakamani kutoa ushahidi kinyume na Serikali na kusababisha Serikali kushindwa kesi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi, kwa nini Serikali ilifungua kesi bila kupata ushahidi vizuri na kutasababishia Watanzania kutumia fedha nyingi kuleta mashahidi kutoka nchi za nje kuja kuendesha kesi ambayo Serikali ilijua kwamba aliyekuwa Rais alikuwa anamjua kwamba yule ni mtu msafi akaja kutoa ushahidi wa kumsafisha yule mtu kinyume na Serikali. Je, Serikali hizi mbili hazina mawasiliano kabla ya kuingia gharama za namna hii? Naomba majibu sahini, ni kitu gani na ni vigezo gani vilitumika kufanya jambo hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Wenje.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Hiki kikundi cha *FGLR* ambacho kimeleta shida kidogo kutokana na *remarks* za Mheshimiwa Rais wetu, hiki kikundi ndiyo kinatuhumiwa kwa *genocide* ya Rwanda ya mwaka 1994 na hiki kikundi *UN* yenyewe inaki-*describe* na

inakitambua hiki kikundi cha *FGLR* kama *terrorist organisation*. *UN* imeanzisha *International Criminal Tribunal for Rwanda* Arusha na moja ya watu wanaotafutwa ni Sylvester ambaye ndiye Mwenyekiti wa *FGRL* na *UN* imetoa pesa taslimu *about five million* nafikiri *dollars* kwa mtu atakayetoa taarifa ya kufanya huyu Sylvester akamatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *remarks* aliyotoa Mheshimiwa Rais imeudhi Wanyarwanda na Tanzania sisi ni nchi ya watu wastaarabu hatutaki kuudhi watu na Wanyarwanda wamekasirika na wameudhika na Mheshimiwa Waziri humu ndani ameendeleza msimamo uleule unaoudhi zaidi Wanyarwanda. Swali langu ni kwamba kama hawa watu wanatafutwa na *UN* na sisi Tanzania ni moja ya nchi ambayo tupo kwenye *UN*, je, msimamo wa Rais wetu anapingana na msimamo wa *UN* kuhusu hawa *rebels* wa *FGRL*? Mheshimiwa Waziri atuambie ni toka lini sisi Tanzania, Rais wetu amekuwa msemaji wa *FGRL* na kuudhi Wanyarwanda?

MWENYEKITI: Haya, ahsante. Mheshimiwa Chomboh.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nina jambo moja ambalo nataka kuongelea kuhusiana matatizo ya nyumba ya Balozi zetu nchi za nje. Mheshimiwa Waziri amejaribu kueleza kwa kirefu zaidi lakini pia alisema ni kwa sababu ya ukata au upungufu wa bajeti kwa ajili ya matengenezo lakini kuna kitu kimoja ambacho nataka kujua, Ubalozi wetu Tanzania Kenya, tumepewa kiwanja siku nyingi tu na ninakumbuka mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya *POAC* na siku moja katika kuhoajiana na moja katika Shirika letu la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) walituambia kwamba wameshakubaliana na Wizara ya Mambo ya Nje lakini pia wameshapata *go ahead* kujenga lile jumba kama moja ya kitega uchumi katika ubalozi wa Tanzania kule Kenya lakini hadi hivi leo wala hatukusikia kitu chochote kuhusiana na suala hili. Nataka Mheshimiwa Waziri anijulishe mpango huo umefikia wapi wakati *NSSF* wako tayari ku-*invest* kama walivyokuwa wameji-*commit* kwa ajili ya maslahi ya nchi na tunajua *NSSF*

1 JUNI, 2013

ni shirika ambalo linatusaidia sana nje na ndani ya nchi katika kujenga miundombinu ya ofisi, vyuo na kadhalika. Ahsante! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chomboh amenifilisi ilikuwa niulize swali hilo. Ahsante!

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi kwanza napongeza kwa ugeni mkubwa wa kimataifa unavyokuja nchini. Mwezi wa tatu alikuja Rais wa China na akatangaza sera au msimamo wake kwa nchi za Afrika, akatangazia hapa Tanzania lakini bado tunatarajia ugeni mkubwa sana wa Mheshimiwa Rais Obama, naye anakuja kufanya hivyo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie sisi Watanzania, kwanza kuna kitu gani hasa kinachowavutia hawa wakuu wa hizi nchi kubwa kuja kufanyia shughuli zao hizo nzuri hapa Tanzania na je sisi Watanzania sasa tunafaidika nini na ujio wao mkubwa kama huo? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kombo.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje kwa kuifanya Zanzibar kama si nchi ya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hii diplomasia ya uchumi, Balozi zetu za Beijing na Ujerumani zinawakilisha nchi za Ujerumani, Uswisi, Jamhuri ya Czechoslovakia, Poland, Hungary, Bulgaria, Australia, Romania na Vatican. Kwa nia njema ya kiuchumi na nia njema ya maendeleo ya kupata

1 JUNI, 2013

watalii na biashara nyingi, Balozi hizi zimepeleka hati kwa nchi nne tu ambazo ni Ujerumani, Uswisi, Australia na Vatican. Sijui kwa nini hawakupeleka hati mpaka sasa kwa Jamhuri ya Czechoslovakia, Holland, Hungary, Bulgaria na Romania maana yake hii ni kwamba hata kama sisi Balozi wetu anasimamia nchi hizi lakini uhalali wao haupo. Tutawezaje kufanya biashara hii nzuri ambayo itatusaidia sisi? Nashukuru sana! (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, nafasi iliyobakia wazi ni ya Mheshimiwa Maua Daftari badala ya Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri ya hotuba yake. Nina jambo dogo tu ambalo nataka anifafanulie au anisaidie. Tanzania tumepakana na nchi kama saba na tumeishi kwa amani kwa sababu sera ya Tanzania ni amani na utulivu nchini. Hivi sasa magomvi yameanza na wenzetu wa nchi jirani labda Mheshimiwa Waziri anisaidie tuna mkakati gani tuliouweka ambao utatusaidia kudhibiti masuala ya mipaka yetu na migogoro imalizike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sisi wenyewe tunajiandaa vipi...

MWENYEKITI: Ni swali moja tu Mheshimiwa!

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja zote zilizotolewa hapa hazina nia ya kuondoa shilingi, kwa maana hiyo tutakwenda kupata majibu na baada tutapitisha. Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze na swali la Mheshimiwa Chomboh ambapo aliuliza

kuhusu matatizo ya majengo yetu na zaidi suala la jengo la Nairobi ambalo ana taarifa kwamba *NSSF* walikubali kuingia ubia na sisi kwa ajili ya kujenga jengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na mazungumzo na *NSSF* na walikubali kulijenga lakini makubaliano hayo yalikuwa kwa misingi ya kwamba tunajenga jengo hilo na kwamba wao watakuwa wanamiliki 80% na Wizara ichukue 20% ya jengo hilo. Sasa lengo kubwa la kujenga majengo hayo ni kwa ajili ya kupata sehemu za kufanyia kazi Balozi zetu lakini pia ziweze kutusaidia kama vitega uchumi ili tuweze kuendesha Balozi nyingine na pale ambapo tumekuwa na majengo kama vitega uchumi yametusaidia kupunguza matatizo ambayo Wizara na hasa Balozi zetu zinayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili halikuonekana kama linatusaidia sana sisi Wizara kwa ajili ya kutoa kiwanja chetu na katika mpango ambao sisi tutapata *only 20%*. Kwa hiyo, tulifikia mahali mazungumzo hayo yakavunjika lakini tumeanza kuzungumza upya kwa ajili ya kupata makubaliano ambayo Wizara kweli yatatusaidia na siyo yale ambayo tutawanufaisha zaidi wao *NSSF*. Makubaliano kama hao yamefanyika kwa mifuko mingine, Bunge hili kama lilivyozungumzwa limejengwa hawaku-*claim* 80% na pia Chuo cha Dodoma kimejengwa kwa msaada wa Mifuko ambapo pia hakuna asilimia kama hiyo ambayo inamilikiwa na Mifuko hiyo. Kwa hiyo, tunachokitaka ni Mifuko hii itupatie fedha na tuweze Serikali kulipa fedha hizo bila ya wao kuwa wamiliki au angalau basi ingeweza kubadilika kuwa sisi tunamiliki 80% na wao 20% lakini siyo kinyume chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja pia ambayo ilizungumzwa na Mheshimiwa Martha Mlata kwamba kwa nini viongozi wa China na *USA* wanakuja Tanzania na hapa wanaitumia kama sehemu ya kutangazia sera zao. Kwanza, ni heshima kubwa kama ambavyo imeelezwa na wajumbe mbalimbali waliochangia lakini na Mheshimiwa Waziri lakini pia kwa kuchagua wameona kwamba sehemu hiyo labda itakuwa ni nzuri zaidi kwa kutangaza. Watakumbuka

1 JUNI, 2013

kwamba Rais Obama katika awamu iliyopita alimua kwenda Cairo na kutangaza sera yake kuhusiana na nchi za Kiislamu kutegemeana na historia ya Cairo, jukumu la nchi hiyo katika ulimwengu wa Kiarabu, kwa hiyo, bila shaka wamezingatia jukumu la Tanzania katika Bara la Afrika na uzito wa Tanzania katika Bara letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini faida ambayo tunaipata ni kwamba kwa kutembelewa tu na viongozi hawa unapata kutangaza nchi yako bila gharama kubwa kwa sababu wote tunajua kwamba kwa kulipia matangazo *CNN* au *BBC* ni gharama kubwa mno lakini kiongozi mkuu anapokuja hivi vyombo vinatangulia wakati mwingine hata mwezi kabla na kila siku vinazota *report* zake kutoka Tanzania na hiyo inakupa wewe *credit* bila kulipia. Pia inaimarisha uhusiano wetu na tunapata fursa ya kuzungumza masuala mbalimbali baina ya nchi zetu kwa ajili ya maendeleo ya upande wetu. Ahsante!

MWENYEKITI: Nakushukuru, maswali yaliyobaki Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwomba Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumjibu Mheshimiwa Mkosamali na mimi nijibu maswali matatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *FGLR*, mimi naomba niseme tena kwamba Umoja wa Mataifa ni kweli wanawatafuta viongozi wa *FGLR* akiwepo Sylvester kama ilivyokuwa inamtafuta Johnbosco Ntaganda ambaye sasa yuko *The Hague* lakini bado wanachama wake na wafuasi wake wanafanya mazungumzo Kampala chini ya Uenyekiti wa Rais Yoweri Museveni kati ya *M23* na Serikali ya Kongo. Kwa hiyo, kutafutwa viongozi waliofanya vitendo hivi ni jambo moja lakini kuendeleza mazungumzo na watu wengine katika kundi hilo ili kuwa-*integrate* katika Jeshi la Taifa, ili kuwarudisha katika nchi yao, ni jambo lingine. Hii ndiyo sehemu ambayo Rais Kikwete alikuwa anaizungumzia kwamba hata ukiwa katika kundi hilo la watu unaowatafuta

na wakashikwa wakapelekwa *The Hague* unafanyaje kuhusu *the rest*? Ni lazima uzungumze nao. Kama nilivyosema, tunazo *Terrorist Organisations* zinazoitwa *terrorists* inategemea umesimama upande gani. Waisrael wanawaita Wapalestina *terrorists* lakini wanazungumza na nchi nyingi sana zimefanya hivi...

MBUNGE FULANI: Hata *ANC*.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Hata *ANC* ya *South Africa* mbele ya macho ya *Apartheid South Africa*, hizi zote zinazoitwa *Liberations Movements* katika nchi zetu zilikuwa zinaitwa *terrorist organisations* lakini mazungumzo ya amani yalifanyika sana na pale iliposhindikana ndiyo mtutu ulitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Kikwete anachozungumzia hapa ni *the opposition*, kama nilivyosema, vipo vyama zaidi ya 20, wala hatujikiti kwa kimoja, sisi tunasema Rais Kagame pamoja na Serikali ya Rwanda kumekucha, sasa ni wakati wa kufanya mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la migogoro ya mipaka yetu, kwenye upande wa migogoro ya mipaka, tunayo NUU, Nje, Ulinzi na Usalama, tunazo Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa yote ya nchi yetu hasa ya mipakani na Kamati hizi hukutana na kutathmini hali ya usalama na kushauri vyombo ya juu, kazi hii inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunakuwa na JPCs, mikutano ya maelewano ya ujirani mwema na kila tunapokutana ajenda mojawapo kubwa inakuwa ni suala zima la ulinzi na usalama, tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna Afrika Mashariki na *SADC*, tuna vitengo vya ulinzi na usalama, tuna vitengo vya mambo ya nje ambavyo wakati wote vinafanya kazi ya kuhakikisha kwamba tunakuwa salama na tunaishi na majirani zetu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee kuhusu safari ya Mheshimiwa Obama, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, suala la usalama na amani ya nchi yetu, ni kigezo kimoja kikubwa sana. Suala la uchaguzi wa haki na huru, ni kigezo kikubwa sana kinachotumika na mataifa makubwa. Suala la kuona matunda ya *investments* na *businesses* wanazozifanya katika nchi hii, ni kigezo kingine cha tatu kinachowavutia sana. Pia suala la michango mizuri na mikubwa inayotolewa na Rais Jakaya Kikwete, hasa katika masuala ya maendeleo na migogoro katika dunia, ni kivutio kingine kinachowaleta viongozi wa dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida zake kwa Watanzania kama alivyosema Naibu Waziri ni nyingi sana. Nimezungumzia wiki iliyopita dola chap chap kwa wenye taxi, hoteli, *restaurants*, starehe, miziki, utamaduni na kadhalika, wachangamkie safari hii kwa sababu anakuja na watu 700. Pia mazungumzo yatakayofanywa kati yake pamoja na CEOs, wakuu wa mashirika na makampuni, tena wa Tanzania watakapokuwa pale ni fursa nyingine kwa Watanzania kueleza na kuwaona wenzao wa kufanya nao uwekezaji na biashara katika soko kubwa la Marekani. Kwa hiyo, faida hizi zitapatikana na tunaubiri kwa hamu sana ugeni huu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, bado kulikuwa na swali la Mheshimiwa Musa Haji Kombo, halafu tutamaliza na AG.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Mheshimiwa Musa Haji Kombo, amezungumzia suala la *accreditation* kwamba ziko Balozi zinaachwa. Utaratibu ni kwamba, sisi kwenye Wizara ya Mambo ya Nje kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais, tulipewa jukumu la kufanya *review* kwamba unapoiambia nchi kama Canada iishike Cuba ni sahihi? Kwa nini isiwe Marekani ambayo ipo kilomita 56 tu kutoka visiwa vya Cuba ndiyo wakawa *accredited* kule? Kwa hiyo, kuna timu yetu inafanya kazi ya kuangalia upya *accreditation* kutoka kwenye Ubalozhi halali ili tuone kama kuna uhalali wa Ujerumani kuzishika zile nchi au ipo nchi ambayo tumefungua

1 JUNI, 2013

Ubalozi au ipo jirani inayoweza kufanya shughuli zile. Kwa hiyo, hilo ndiyo zoezi ambalo tunalifanya na baada ya kulikamilisha tutapeleka taarifa kwa Mheshimiwa Rais halafu Mabalozzi wetu watapata hati, tena Mabalozzi wapya. Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo mafupi sana kuhusu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali, kuhusiana na hii kesi ya Profesa Mahalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, hakufanya kosa lolote kutoa ushahidi upande wa Profesa Mahalu kwa sababu Profesa Mahalu ni mtuhimiwa tu na si mhalifu. Nimeambiwa kwamba, Mheshimiwa Mbunge ni Mwanasheria na kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 13(6)(a) na (b), nafikiri kwa heshima yako Mwenyekiti nisome, inasema kwamba, kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, mamlaka ya nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba:-

(a) Wakati haki na wajibu kwa mtu yeyote inapohitajiwa kufanyiwa maamuzi na Mahakama au chombo kingine chochote kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na pia haki ya kukata rufani au kupata nafuu nyingine yoyote kisheria kutokana na maamuzi ya Mahakama au chombo hicho kinginecho kinachohusika.

(b) Ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali wala mimi mwenyewe sikusononeshwa na Mheshimiwa Rais Mstaafu

1 JUNI, 2013

Benjamin Mkapa kwenda kutoa ushahidi dhidi ya Profesa Mahalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya kushtaki, ni ya Mkurugenzi wa Mashtaka, maamuzi yake hayaingiliwi. Katika busara yake aliona mashtaka yale yaende Mahakamani. Sasa naomba pia kutoa taarifa kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka amekata rufaa dhidi ya maamuzi ya Mahakama. Kwa hiyo, suala hili bado liko Mahakamani linaendelea, lakini nimeona nitoe maelezo hayo mafupi kuondoa hii dhana kwamba ukiishakuwa Rais huwezi kutoa ushahidi kwa mtu ambaye amekuomba utoe ushahidi, kwa sababu hapa kama anavyofahamu ni *issue* ya *facts* kwamba, je, ilikuwa hivi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais Mstaafu alikuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kufahamu yale kwa sababu kilikuwa ni kipindi chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

| | |
|---|----------------------|
| Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> | Shs.669,166,000/= |
| Kif. 1003 - <i>Foreign Affairs Office Zanzibar...</i> | Shs.512,325,000/= |
| Kif. 1004 - <i>Policy and Planning... ..</i> | Shs.557,354,000/= |
| Kif. 1005 - <i>International Cooperation... ..</i> | Shs.2,290,346,000/= |
| Kif. 1006 - <i>Europe and America... ..</i> | Shs.500,150,000/= |
| Kif. 1007 - <i>Asia and Australia... ..</i> | Shs.440,735,000/= |
| Kif. 1008 - <i>Africa... ..</i> | Shs.4,205,880,000/= |
| Kif. 1009 - <i>Regional Cooperation... ..</i> | Shs.5,025, 023,000/= |
| Kif. 1010 - <i>Protocol... ..</i> | Shs.15,309,153,000/= |
| Kif. 1011 - <i>Legal Services... ..</i> | Shs. 1,802,508,000/= |
| Kif. 1012 - <i>Government Comm. Unit... ..</i> | Shs.318,276,000/= |
| Kif. 1013 - <i>Middle East Division... ..</i> | Shs.419,834,000/= |
| Kif. 1014 - <i>Internal Audit Unit... ..</i> | Shs.246,145,000/= |
| Kif. 1015 - <i>Procurement Unit... ..</i> | Shs.232,449,000/= |
| Kif. 1016 - <i>Info. and Comm. Technology ...</i> | Shs.191,847,000/= |
| Kif.1017- <i>Diaspora Engagement & Opportunity</i> | Shs.242,744,000/= |

| | |
|---|-----------------------|
| Kif. 2001- <i>Embassy of Tanzania–Addis Ababa... ..</i> | Shs. 1,517,308,000/= |
| Kif. 2002 - <i>Embassy of Tanzania – Berlin...</i> | Shs. 3,079,804,000/= |
| Kif. 2003 - <i>Embassy of Tanzania – Cairo...</i> | Shs.1,175,584,000/= |
| Kif. 2004 - <i>Embassy of Tanzania–Kinshasa...</i> | Shs.1,058,047,000/= |
| Kif. 2005 - <i>Embassy of Tanzania –Abuja...</i> | Shs. 2,196,082,000/= |
| Kif. 2006 - <i>High Commission of Tanzania –London</i> | Shs. 2, 957,019,000/= |
| Kif. 2007 - <i>High Commission of Tanzania –Lusaka</i> | Shs.1,007,381,000/= |
| Kif. 2008 - <i>High Commission of TZ–Maputo</i> | Shs.1,863,376,000/= |
| Kif. 2009 - <i>Embassy of Tanzania–Moscow...</i> | Shs.2,441,252,000/= |
| Kif. 2010 - <i>High Commission of TZ – New Delhi</i> | Shs.2,007,850,000/= |
| Kif. 2011- <i>Permanent Mission to the UN- New York</i> | Shs.4,407,538,000/= |
| Kif. 2012- <i>High Commission of Tanzania – Ottawa</i> | Shs.1,694,168,000/= |
| Kif. 2013 - <i>Embassy of Tanzania – Paris...</i> | Shs. 2,665,486,000/= |
| Kif. 2014 - <i>Embassy of Tanzania – Beijing...</i> | Shs.2,086,476,000/= |
| Kif. 2015 - <i>Embassy of Tanzania – Rome ...</i> | Shs.2,441,132,000/= |
| Kif. 2016 - <i>Embassy of Tanzania – Stockholm</i> | Shs.2,299,053,000/= |
| Kif. 2017 - <i>Embassy of Tanzania – Tokyo...</i> | Shs.2,793,366,000/= |
| Kif. 2018 - <i>Embassy of Tanzania – Washington</i> | Shs.3,526,087,000/= |
| Kif. 2019 - <i>Embassy of Tanzania – Brussels...</i> | Shs.3,554,049,000/= |
| Kif. 2020 - <i>Permanent Mission to The UN-Geneva... ..</i> | Shs.4,169,729,000/= |
| Kif. 2021 - <i>High Commission of Tanzania Kampala</i> | Shs.1,196,082,000/= |
| Kif. 2022 - <i>High Commission of Tanzania – Harare</i> | Shs.1,282,537,000/= |
| Kif. 2023 - <i>High Commission of Tanzania – Nairobi</i> | Shs. 2,738,563,000/= |
| Kif. 2024 - <i>Embassy of Tanzania – Riyadh...</i> | Shs.1,617,227,000/= |
| Kif.2025 – <i>High Commission of Tanzania – Pretoria</i> | Shs.2,362,295,000/= |
| Kif. 2026 - <i>Embassy of Tanzania – Kigali...</i> | Shs.1,204,571,000/= |

1 JUNI, 2013

Kif. 2027 - *Embassy of Tanzania – Abu Dhabi...* ... Shs. 2,081,105,000/=

Kif. 2028 - *Embassy of Tanzania – Bujumbura ...* ... Shs.1,176,729,000/=

Kif. 2029 - *Embassy of Tanzania – Muscat ...* Shs.1,213,737,000/=

Kif. 2030 - *High Commission of TZ–Lilongwe...* ... Shs.1,053,476,000/=

Kif. 2031 - *Embassy of Tanzania – Brasilia...* Shs.2,370,431,000/=

Kif.2032- *High Commission of TZ- KualaLumpa...* ... Shs.1,842,910,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kif.1004 - *Policy and Planning ...* ... Shs.28, 000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kukamilisha hatua ya Kamati ya Matumizi, naomba sasa nimwite mtoa hoja ili aweze kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Bernard Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya Mapato ya Matumizi ya

1 JUNI, 2013

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba ya Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, viongozi wa Bunge na Bunge zima, naomba Mheshimiwa Waziri nikutakie kila la kheri katika kwenda kutekeleza majukumu mazito ya Wizara yako. Nchi yetu inategemea sana hayo mahusiano na ushirikiano wa Kimataifa ili kuendeleza kwanza amani ya nchi yetu lakini kuchukua kama nafasi hiyo ni mchango muhimu wa maendeleo ya Taifa letu. Kwa hiyo tunaridhia leo upewe fedha hizo tena na wewe pamoja na timu yako, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, wataalamu wetu wengine wote na Mabalozi wetu, basi tunawatakiwa kila la kheri na tunaamini mtatusaidia sana. *Inshallah* Mwenyezi Mungu awasaidie mfanye kazi vizuri, tutakutana kwenye unguwe kama hiihii tena mwaka ujao wa fedha mwakani hapa ndani na tunaamini tutakuwa tumepiga hatua kubwa ya kimaendeleo katika majukumu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, bado ninazo shughuli kadhaa hapa Mezani na kuna Mbunge mmoja hapa

1 JUNI, 2013

ameniandikia meseji ameniambia Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwa uko *fit* na sisi tunakwambia tuko *fit* lete Wizara nyingine tuanze nayo sasa hivi hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa kweli maneno haya yanatia moyo sana na kadri ninavyowatazama Waheshimiwa Wabunge mmetulia kwa idadi ya kutosha, mko *fit* kweli. Watanzania naomba tu muone ni namna gani Waheshimiwa Wabunge hawa wanawajibika kwa ajili ya Taifa letu. Kwa kweli nakubaliana sana na huyu aliyetoa hii hoja hapa tungejua mapema tungepanga Wizara nyingine tuanze nayo leo. (*Makofi*)

Kabla sijaendelea na hatua nyingine, nina tangazo hapa. Tafadhali naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho tarehe 2 Juni, 2013 saa 4.00 asubuhi kutakuwa na Semina ya Wabunge wote kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itakayofanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tunapewa taarifa.

Halafu naomba uwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo jioni kutakuwa na Mechi ya Kirafiki ya Mpira wa Miguu na Mpira wa Pete kati ya Timu ya Waheshimiwa Wabunge yaani *Bunge Sports Club* na timu ya *NSSF*. Mechi hizo zitachezwa katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma kuanzia saa 9.00 alasiri. Aidha, Kamati ya Ufundi chini ya Mheshimiwa Profesa Majimarefu imekasimu madaraka yake leo kwa timu nyingine mpya ambayo itaonekana katika viwanja hivyo na Waheshimiwa Wabunge msishangae ni mambo hayo hayo aliyoyasemea Waziri wa Mambo ya Nje utamaduni wa Kiafrika. Kwa hiyo, Kamati ya Ufundi leo itajitokeza kwa utaratibu mwingine ndio tangazo hapa nililopewa. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge tumepokea Maelezo Binafsi kutoka kwa Mheshimiwa Mpina, kwa hiyo kwa mujibu wa Kanuni hizo hizo nampa nafasi Mheshimiwa Mpina ili aweze kuwasilisha Maelezo yake Binafsi, Mheshimiwa Mpina.

**Maelezo Binafasi Juu ya Mapato na Matumizi ya Serikali
ya Mheshimiwa Luhaga J. Mpina**

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

MWENYEKITI: Una dakika 15 tu kwa mujibu wa Kanuni.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Sawa. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hotuba yangu hapa ni ndefu mno nilijua ni nusu saa, kwa hiyo, nitajitahidi sana ili niingie kwenye hizo dakika 15, lakini naomba uipokee kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 28(8), naomba kutoa maelezo binafsi juu ya matumizi ya kawaida ya Serikali kuwa makubwa kuliko mapato ya ndani na hivyo kupelekea deni la Taifa kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kipindi cha maswali na majibu tarehe 16, Aprili 2013 hapa Bungeni niliuliza swali la nyongeza katika swali la msingi namba 47 la Mheshimiwa Thuwayaba Idrisa Muhammed (Mbunge wa Viti Maalum) kuhusu deni la Taifa na pia katika Mwongozo niliouomba kwako ambapo nilieleza kuwa moja ya sababu ambayo inasababisha deni la taifa kuongezeka ni pamoja na Serikali kuwa na matumizi makubwa ya kawaida kuliko uwezo wa mapato yake ya ndani na hivyo imekuwa ikikopa fedha ndani na nje ili kufidia pengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum wakati akijibu swali langu la nyongeza alikana kwamba Serikali kwa namna yoyote ile haikopi fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida bali inakopa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo pekee. Pia hata wakati akitoa maelezo juu ya Mwongozo niliouomba tarehe 24/04/2013 aliendelea na msimamo huo na akaongeza kuwa katika fedha za matumizi ya kawaida (*recurrent expenditure*) kuna kiasi kikubwa (*big*

chunk) ya fedha za maendeleo zifikiazho trilioni 1.6 kama *Human Capital Investment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sijaridhika na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Fedha kwa nyakati zote mbili yaani wakati akijibu swali la nyongeza na hata alipopewa nafasi ya kujibu Mwongozo wangu, kwani maelezo yake hayakuweza kujibu hoja mahsusi na hii ni kinyume na masharti yaliyowekwa na kifungu cha 46(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, hivyo nimeamua kuwasilisha maelezo binafsi ili nipate ufafanuzi wa kina na kwamba niweze kuishauri Serikali juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yake yameleta mkanganyiko mkubwa kwani badala ya Naibu Waziri wa Fedha kuthibitisha alichokieleza kuwa Serikali haikopi kugharamia matumizi ya kawaida, ameleta tafsiri mpya ya shughuli gani ni matumizi ya kawaida (*reccurent expenditure*) na ipi ni matumizi ya maendeleo (*development expenditure*). Amekwenda mbali zaidi kwa kusema hata fedha inayotengwa kulipa deni la Taifa na semina ni fedha za maendeleo, je, tafsiri hii ya Naibu Waziri inazingatia viwango gani? Kwani kwa mujibu wa hotuba za bajeti za Waziri wa Fedha zimekuwa zikiyagawa matumizi katika makundi mawili yaani matumizi ya kawaida (Mishahara, Deni la Taifa na matumizi mengineyo) na matumizi ya maendeleo kwa mujibu wa viwango vya kitaifa (*Government Standing Orders*) na kimataifa (*IMF, World Bank, Accounting International Standards*n.k)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ushahidi wa kitakwimu unaothibitisha kuwa matumizi ya Serikali ni makubwa kuliko mapato ya ndani na kwamba Serikali imekuwa ikilazimika kutafuta misaada na mikopo ili kuziba pengo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa fedha ya mwaka 2011/2012 inaonyesha kuwa mapato ya ndani yalikuwa trilioni 7.3 wakati matumizi ya kawaida yalikuwa trilioni 8.6 hii ni tofauti ya trilioni 1.3. Hotuba ya bajeti ya

mwaka wa fedha 2012/2013, mapato ya ndani yalikuwa trilioni 9.1 wakati matumizi ya kawaida yalikuwa trilioni 10.6 hii ni tofauti ya trilioni 1.5. Kwa mujibu wa takwimu hizi pengo la mapato linaongezeka kila mwaka na kila mapato ya ndani yanapoongezeka matumizi ya kawaida huongezeka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika vitabu vya hotuba ya Waziri wa Fedha ya zinaonyesha kiasi cha shilingi trilioni 3.05 (2011/2012) na shilingi trilioni 2.31 (2012/2013) ni misaada na mikopo kugharamia miradi ya maendeleo na shilingi trilioni 2.48 (2011/2012) na shilingi trilioni 2.89 (2012/2013) zilikopwa kwa ajili ya kuziba pengo la mapato. Ni dhahiri kwamba fedha hizi zilikopwa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Umasikini na maendeleo ya watu (*PHDR -2011*) matumizi ya Serikali yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka 15.1% ya *GDP* (2000/2001) hadi kufikia 26.3% (2009/2010). Pia pengo la mapato ya ndani na matumizi ya kawaida limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka, nakisi ya kibajeti (*Fiscal deficit*-bila misaada) limekuwa likikuwa kila mwaka kutoka 4.3% (2001/2002) hadi 10.9% (2009/2010) ya *GDP* na nakisi ya kibajeti ikijumuisha misaada imekuwa toka 0.4% hadi 4.7% (2009/10) ya *GDP*. Hivi sasa nakisi ya kibajeti (Kujumuisha misaada) limefikia 6.6% (2011/12) ya *GDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Taifa liweze kutoka hapa lilipo sasa ni lazima tuongeze bidii katika ukusanyaji wa mapato yetu ya ndani, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima sambamba na kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato na matumizi holela. Tumekuwa tukishuhudia ndani ya Bunge hili kupitia hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu kuwa Serikali itapunguza matumizi yake yasiyo ya lazima lakini kwa sababu zisizojulikana matumizi haya yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa upande wa kuongeza mapato, jitihada mbalimbali zimewekwa lakini mafanikio yake yamekuwa ni ya kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida (*reccurrent expenditure*) ya Serikali hujumuisha deni la taifa, mishahara na matumizi mengineyo (*OC*) ukipitia vipengele hivi vyote utagundua kuwa endapo jitihada madhubuti zitachukuliwa tunaweza kupunguza matumizi ya Serikali kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mengineyo (*Other Charges-OC*) kwa Wizara, Mikoa na Halmashauri; eneo hili limekuwa ni kichaka cha ufisadi. Kumekuwa na manunuzi yasiyokuwa na tija, samani za ofisi zenye gharama kubwa kila mwaka, posho za safari (ndani na nje ya nchi), ununuzi wa magari ya kifahari, mtiririko wa warsha na semina, mafuta, mafunzo, samani, viburudisho, matengenezo hewa ya magari, maonyesho ghali yasiyo na tija, ongezeko la shughuli za kiutawara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa uchambuzi wa bajeti unaofanywa kila mwaka na Shirika la *Sikika* katika maeneo sita pekee ya bajeti yaani: posho, gharama za safari (ndani na nje), semina (ndani na nje ya nchi), mafuta na vilainisho, viburudisho na ununuzi wa magari. Matumizi haya yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka, kama ifuatavyo: shilingi bilioni 626.3 (2011/2012), shilingi bilioni 681.2 (2012/2013) na mwaka ujao wa fedha (2013/2014) inakadiliwa kuwa shilingi bilioni 714.1. Kwa hiyo, matumizi haya yamekuwa yakipanda licha ya Serikali kuahidi kuwa itapunguza matumizi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu umekwenda mbali zaidi na kuonyesha kuwa katika mwaka ujao wa fedha (2013/2014) ofisi ya Mkaguzi na Mdhhibiti wa Mahesabu ya Serikali imepunguza gharama za mafunzo kwa kiasi cha shilingi milioni 888 sawa na punguzo la 38% lakini wakati huo huo Wizara ya Fedha imeongeza mara kumi gharama za mafunzo kutoka shilingi milioni 885 (2012/2013) hadi shilingi bilioni 8.8 (2013/2014).

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ni matumizi yenye utata na yanayolalamikiwa sana ndani na nje ya Bunge lako

1 JUNI, 2013

Tukufu. Kwa mujibu wa uchambuzi uliofanywa na Sikika, jumla ya shilingi bilioni 360 zimepangwa kutumika kulipa posho tu katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kuna ongezeko la 15% ukilinganisha na mwaka 2012/2013. Ripoti ya Bunge ya Novemba 2011 iliyochunguza skandali ya Jairo ni mfano na ushahidi tosha jinsi matumizi mabaya ya posho na dizeli kwa magari yasivyo na tija kwa uadilifu na maendeleo ya nchi. Vilevile kwa mujibu wa *MTEF* 2011/2012-2013/2014 ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii bei ya mafuta ilichajiwa hadi shilingi 4,000/= kwa lita badala ya shilingi 2,200/= iliyoko sokoni. Mambo haya yote Waziri wa Fedha anajua na Waziri Mkuu anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari za ndani na nje ya nchi pamoja na warsha ni matumizi mengine yaliyogubikwa na ufujaji yaliyolalamikiwa sana hadi kufikia Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda kuagiza watakaotaka kufanya semina na safari watafute kibali kutoka ofisi yake. Haidhuru bajeti katika maeneo haya imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mmoja tu kufafanua ufisadi wa semina na safari, Tanzania ilialikwa katika moja ya vikao vya Umoja wa Mataifa katika Tume ya Haki za Kiuchumi, Jamii na Utamaduni (*United Nations Committee for Economic, social and cultural rights*) vilivyofanyika Geneva, Uswiss kuanzia tarehe 12-30 Novemba 2012, Tanzania ilipeleka jopo la watu 34 ikiwa ni msafara mkubwa kuliko nchi nyingine zote zilizoalikwa, mfano Bulgaria (16), Ecuado (9), Iceland (6), Mauritania (13) na Equitorial Guinea (8), Pamoja na jopo hilo kutoka Tanzania kuongoza kwa ukubwa lakini wakati wa majadiliano katika kikao hicho Watanzania walishindwa hata kujibu maswali, kwa makadirio ya chini ziara hiyo ilitumia zaidi ya shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi zimenukuliwa kutoka tovuti ya UN

http://www2.ohchr.org/english/bodies/cescr/docs/list/DelegationTanzania_49.pdf na, <http://www2.ohchr.org/english/bodies/cescr/cescrs49.htm>

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha vipengele hivyo sita hapo juu yapo maeneo mengi yanayosababisha upotevu mkubwa wa fedha za umma, mfano; ununuzi wa kila mwaka wa samani, ununuzi wa vifaa (sare, *stationary* n.k) zaidi ya mahitaji na vyenye bei kubwa kuliko iliyopo sokoni, gharama kubwa za pango, gharama kubwa za matengenezo na ukarabati (barabara, majengo na magari) na uhamisho holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi ahadi ya Serikali ya kupunguza matumizi yasiyokuwa na tija haina ukweli wowote. Ushauri wa CAG, Wabunge na wadau mbalimbali hauzingatiwi na Serikali kwani bajeti zimekuwa zikiwasilishwa kwa sura ileile. Mimi binafsi nilikataa bajeti ya Serikali ya mwaka 2012/2013 ilipowasilishwa kutokana na miradi ya maendeleo kutengewa fedha pungufu huku matumizi yasiyokuwa na tija kutengewa fedha lukuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa hatua nyingine katika mwaka ujao wa fedha baada ya Serikali kushinikizwa na Wabunge imekubali kupunguza Matumizi Mengineyo (OC) na kuongeza fedha za Maendeleo katika Wizara mbalimbali, mfano, Maji (Shs.bilioni 184.5), Uchukuzi (Shs.bilioni 30), Viwanda (Shs.bilioni 30) na Vijana (Shs.bilioni 9). Swali la kujiuliza ni kwa nini Serikali kwa muda mrefu imekuwa na kigugumizi cha kupunguza matumizi haya? Huu sio utaratibu mzuri wa kupunguza matumizi ya Serikali kwa sababu Serikali ilipaswa kukaa na kupitia matumizi yake kifungu kwa kifungu na kuona matumizi ambayo hayahitajika na siyo ya lazima ambapo Watanzania wanaingizwa kwenye deni kubwa na hivyo kushindwa kutumia fedha zao kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwani kwa muda mrefu miradi ya maendeleo imekuwa ikitengewa fedha kidogo na Taifa kuingia mikopo isiyo ya lazima na kuzidi kuongeza mzungu mkubwa wa madeni. Hii si sawa kuendekeza matumizi ya namna hii wakati Watanzania wengi wakifa kwa kukosa huduma

muhimu za afya, elimu, barabara na maji. Endapo eneo hili litadhhibitiwa vizuri tunaweza kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 700.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: AG, Serikali itapata nafasi ya kuyajibu.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye ...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inahitaji...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina, hebu dakika moja.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inahitaji msomaji asome karatasi aliyoandika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina alichokuwa anasema AG ni kwamba sasa unaruka yale uliyotukabidhi hapa unayo mengine ambayo sisi hapa hutuna.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosoma hapa ni *summary* ya dakika 15, lakini ninayosoma hakuna ambalo halipo hapa. Ninayosoma yote ni *summary* ya haya niliyokuwa nayo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina hebu naomba ukae, utulie kidogo. Nakubaliana na wewe ni kwamba unasoma *summary* hata sisi tunapokuja na *summary* inatakiwa yale unayoyasoma katika Kanuni hizi zinazoongoza Maelezo Binafsi unatakiwa kwenda moja kwa moja kwenye *document* yako, ukiruka *page* unayotaka kuiacha unakwenda katika *page* ambayo unataka kuisoma. Sasa wewe huna ruhusa ya kuingia Bungeni ukiwa na Maelezo Binafsi ukiwa na *document* mbili, ya *summary* na ile ambayo umeigawia Kiti na unayo wewe mwenyewe. Kama ni suala la kuruka katika hii *document*

1 JUNI, 2013

yako, ruka mengine, unayotaka yasikike yaseme, lakini iombe *Hansard* irekodi hii hotuba yako yote kama ilivyo, naomba uendelee. (*Makofi*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Utuongoze sasa huko ukurasa gani ili tukufuatilie.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Niko ukurasa wa saba, mishahara.

MWENYEKITI: Ukurasa wa?

MHE. LUHAGA J. MPINA: Ukurasa wa saba.

MWENYEKITI: Haya twende.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utalinda muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mishahara nalo lina matatizo mengi, kwanza, ni mishahara ya watumishi hewa ambayo imekuwa ikilipwa na vilevile kuna suala la pesa zinaidhinishwa kwenye bajeti...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina uko *paragraph* ipi?

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *paragraph* ya kwanza ile ya mishahara, ukurasa wa saba.

MWENYEKITI: Ukurasa wa saba?

MHE. LUHAGA J. MPINA: Sasa hii ya kwangu ina *font* kubwa, angalia kuna kipengele nimeandika Mheshimiwa Spika, mishahara, ya kwangu ina *font* 16 nadhani kurasa zinaweza zikawa zimechanganyikana kidogo.

MWENYEKITI: Hebu samahani kidogo, Wahudumu naomba mumpelekee Mheshimiwa Mpina hii taarifa ambayo ameigawanya kwa Wabunge halafu usome kwa kuzingatia hii ambayo umewagawia Wabunge. Kwa hiyo, sasa utuongoze ukurasa huo wa mishahara uko ukurasa gani kwa sababu hata mimi hapa Mezani sina hiyo ya kwako.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Niko ukurasa wa tano, *paragraph* ya mwisho imeandikwa pale, Mheshimiwa Spika, mishahara.

MWENYEKITI: Haya tuendeleo sasa.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinde muda wangu.

MWENYEKITI: Sina neno, nataka tu twende pamoja kusudi tuelewane.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Hamna tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara, katika eneo hili tumeshuhudia mishahara hewa kwa muda mrefu sasa. Kwa mujibu wa taarifa CAG shilingi bilioni 1.8 (2009/2010) na shilingi milioni 142.7 (2010/2011) zimelipwa kwa watumishi hewa katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, mishahara mipya imekuwa ikitengwa katika bajeti wakati kibali cha ajira hakijatolewa, vilevile kumekuwepo na ongezeko kubwa la umbile la Serikali (*Government structure*) usiozingatia uwezo wa mapato ya ndani. Mfano, utitili wa Mashirika ya Umma ambayo kwasasa yanafikia zaidi ya 200 na mengi yakifanya kazi zinazofanana, katika mwaka wa fedha 2012/2013 ruzuku ya mashirika ya umma katika matumizi ya kawaida ilifikia shilingi trilioni 1.7. Hii ni sawa na 11.3% ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukubwa wa Wizara zinazofanya kazi zinazofanana mfano TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hata baada ya shughuli za Elimu ya msingi na sekondari kuhamishiwa TAMISEMI ukubwa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi umebaki vilevile.

1 JUNI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Taifa, utaona kwamba nchi kukopa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina soma ulichokiandika.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kwamba Serikali imekuwa ikikopa ndani na nje ya nchi ili kugharamia Miradi ya Maendeleo (*Development Expenditure*) pamoja na kuziba Pengo la mapato (*Recurrent Expenditure*) na kwamba hivi sasa Deni la Taifa limefikia shilingi trilioni 21 sawa na 47% ya Pato la Taifa (*GDP*). Hii inamaanisha kwamba karibia nusu ya pato la Taifa liko kwenye Deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kukopa siyo dhambi ila tatizo linaanzia pindi tunapokopa kwa ajili ya matumizi makubwa yanayoweza kuepukwa, kupunguzwa na kugharamiwa na fedha za ndani. Pia kumekuwa na tatizo la kutokulipa marejesho ya mikopo kwa wakati na kusababisha malimbikizo makubwa ya riba kunakopelekea kuongezeka kwa deni la Taifa kila mwaka, mfano hadi kufikia Septemba 2012, malimbikizo ya riba yamefikia dola za kimarekani milioni 781.06 (Tsh trilioni 1.27).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwepo na kasi kubwa ya ongezeko la dhamana za Serikali (*Excessive use of Government Guarantees*) kwani hii inaongeza deni kwa Serikali pindi mzaminiwa anaposhindwa kulipa (*Contigent Liabilities*). Hadi Disemba 2011 dhamana za Serikali zilifikia shilingi trilioni 1.4, ipo mifano mingi ya makampuni ambayo hayafanyi vizuri katika biashara baada ya kupata dhamana ya Serikali. Pia kwa mujibu wa CAG madeni mengine hayana maelezo na hivyo ni mikopo hewa, hii si hali nzuri kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kitendo hichi kupelekea kuweka rehani mapato ya siku za usoni lakini pia ni mzigo mkubwa unaolielemea Taifa. Ni lazima nchi yetu sasa iwe na mtazamo mpya katika ukopaji na udhibiti wa ongezeko la Deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Maendeleo (*Development Expenditure*). Serikali hutegemea misaada, mikopo na fedha za ndani katika kugharamia eneo hili. Kutokana na fedha za ndani kuzidiwa na matumizi ya kawaida, Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo sana za ndani katika eneo hili na zimekuwa hazitolewi kutoka hazina kwa wakati, pindi zinapotolewa huwa pungufu ya kiwango kilicho idhinishwa katika bajeti na wakati mwingine hazitolewi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo imekuwa ya kusuasua hususani tangu mdororo wa uchumi ukumbe Dunia mwaka 2008, kumekuwa na masharti magumu na maswali yasiyokuwa na majibu kutoka kwa wahisani na wakati mwingine wahisani wamekuwa wakijitoa kutokana na kukosekana kwa nidhamu na uadilifu wa matumizi ya fedha za umma nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia fedha zimekuwa zikitolewa kwa kuchelewa na pungufu ya kiwango kilicho ahidiwa. Kutokana na kusuasua kwa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kumepelekea miradi mingi kutokamilika kwa wakati na hata kutotekelezwa kabisa. Mfano, miradi ya maji ilitengewa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 140 katika mwaka wa fedha 2012/2013 lakini hadi kufikia robo ya pili fedha iliyokuwa imetolewa ni shilingi bilioni 29 sawa na 20.7% tu ya fedha iliyoidhinishwa; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 120.4 lakini hadi kufikia machi 2013 ni shilingi bilioni 22.96 tu sawa na 19% ya fedha zilizoidhinishwa ilikuwa imetolewa, pia katika Halmashauri na mashirika mengi nchini hadi bajeti inafikia mwisho yanakuwa yamepokea fedha chini ya 50% ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimia Wabunge ni muda sasa kuwaeleza Watanzania ukweli kwamba Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP-1) unadalili zilizo wazi kutokutekelezeka hata PAMANDU (*President's Delivery Bureau*)

iliyoanzishwa haitaleti mabadiliko yoyote tusipotatua tatizo la ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya ndani. Mapato ya ndani hutegemea mapato yatoakanayo na kodi na yasiyo ya kodi yaani maduhuli. Mapato yote ya kodi hukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) wakati maduhuli hukusanywa na Wizara, Taasisi na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wigo wa mapato. Kwa mujibu wa *TRA* ni watu milioni 1.6 tu wanaolipa kodi ya mapato kati ya watu milioni 14.2 ambao wanastahili kulipa. Hii ni idadi ndogo sana ya walipa kodi ikilinganishwa na nchi jirani ya Kenya ambayo walipa kodi wake wamefikia zaidi ya milioni 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa *TRA* kukusanya mapato. Licha ya *TRA* kufikia malengo na wakati mwingine kuvuka malengo ya kukusanya mapato lakini kumekuwa na hisia kuwa malengo mara nyingi yako chini ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi na mahitaji muhimu ya Taifa. Mwenendo wa makusanyo ya kodi kwa miaka mitatu shilingi trilioni 5.2 (2010/2011), shilingi trilioni 6.2 (2011/2012) na inakadiriwa shilingi trilioni 8.1 (2012/2013). Makusanyo haya ni madogo mno ikilinganishwa na rasimali za Taifa na idadi ya watu iliyofikia milioni 44.9 (Sensa, 2012).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa Wizara, Taasisi na Halmashauri kukusanya maduhuli. Ukusanyaji wa maduhuli umekuwa wa kusuasua kwani licha ya rasilimali zilizopo, mapato yasiyokuwa ya kodi ni chini ya 10% ya makusanyo ya mapato ya Serikali, mwenendo wa makusanyo wa maduhuli shilingi bilioni 442.9 (2010/2011), shilingi bilioni 911.7 (2011/2012) na inakadiriwa shilingi bilioni 644.6 (2012/2013). Hii inaonyesha dhahili kuwa hakuna usimamizi thabiti wa ukusanyaji wa mapato nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafiti mbalimbali ikiwemo Kamati Maalum ya Spika (Mapato- 2012)

zinaonyesha udhaifu mkubwa uliopo wa ukusanyaji kodi na maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, madini mengi yamekuwa yakitoroshwa na kuuzwa nje ya nchi kwa njia za panya na hivyo kukwepa kodi, pia makampuni ya madini yamekuwa yakikwepa kodi kiasi cha shilingi bilioni 525 kila mwaka kwa kuingiza katika hesabu matumizi yasiyo ruhusiwa, licha ya *TMAA* kuthibitisha ukwepaji huu lakini *TRA* haijakusanya mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya simu kuendelea kukwepa kodi kwa kuficha taarifa muhimu za kukokotolea kodi, gharama kubwa za matangazo zisizokuwa na kikomo, gharama zisizokuwa na ukomo za *management* na *service fee*, pamoja na misamaha lukuki ya kodi. Inakadiriwa kuwa kila mwaka makampuni ya simu hukwepa kodi kiasi kisichopungua shilingi bilioni 600. Tanzania inakusanya kodi ya mapato kidogo sana katika sekta ya simu kuliko nchi nyingine yoyote Afrika Mashariki, mfano mwaka 2010 Kenya (USD 79.3 Milioni), Uganda (USD 31.3 Milioni), Rwanda (USD 14 Milioni) wakati Tanzania ilikuwa na USD 1.7 Milioni tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari. Katika Bandari mapato mengi yamekuwa yakipotea kutokana na ucheleweshaji wa kupakia na kupakua mizigo, wizi wa mizigo, rushwa ambapo baadhi ya wafanya biashara huungana na watendaji wa Serikali kuibia Serikali mapato. Kwa mujibu wa Taarifa za Benki ya Dunia (*Opening the Gate*, 2012) zinasema zaidi ya mapato yapatayo USD bilioni 1.8 (TSH trilioni 2.9) yalipotea bandarini kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta nyingine kama uvuvi Serikali inakosa mapato ya shilingi bilioni 362 kila mwaka kutokana na udhibiti hafifu wa uvuvi haramu pamoja na kukosekana takwimu za kukokotolea mapato. Katika sekta isiyo rasmi kila mwaka tunakosa mapato ya shilingi trilioni 1.3 kutokana na kushindwa kuwatambua walipa kodi katika sekta hii na kwamba mfumo wa kodi uliopo unawaacha

nje. Pia sekta ya misitu na nyuki tunapoteza shilingi bilioni 93 kila mwaka kutokana na rushwa na utoroshaji wa magogo ghafi nchi za nje, wakati mashirika ya umma hupoteza zaidi ya shilingi bilioni 50 kila mwaka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoroshaji wa fedha nje ya nchi. Kwa mujibu wa tafiti za hivi karibuni Utoroshaji wa fedha nje ya nchi umeougezeka na umefikia wastani shilingi bilioni 600 kila mwaka. Pia kwa mujibu wa Mwenyekiti wa *United Nations High Level on Illicit Financial Flow from Africa*, Hon. Thabo Mbeki anasema kuwa utoroshaji wa fedha nje ya Bara la Afrika umefikia USD billion 50 (TSh triloni 81.5) kila mwaka. Pamoja na ongezeko hili linalolitishia kufilisika kwa Taifa na Bara zima lakini kwa sababu zisizoeleweka Serikali imenyofoa kipengele cha utoroshaji wa fedha nje ya nchi katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP-1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata vyanzo vipya vya mapato vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ukurasa 82-96 yaani *Superprofit tax on minerals, controlling Illicit Outflows, Taxation on Financial Transactions, Tanzania in the Diaspora* na kadhalika havijaanza kufanyiwa kazi. Wakati huohuo Tanzania hivi sasa tunajitegemea kibajeti kwa 54%-60% tu ikilinganishwa na nchi jirani ya Kenya ambayo inajitegemea kibajeti kwa 98%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misamaha ya kodi. Misamaha ya kodi inayotolewa na Serikali kama uvutio vya uwekezaji nchini ni mikubwa mno kiasi cha kuathiri wigo wa mapato nchini. Kutokana na mapato madogo ya ndani Taifa limeshindwa kugharamia miradi ya maendeleo, kulipa watumishi wake mishahara mizuri pamoja na kugharamia shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Serikali. Hali hii imelifanya Taifa kuendelea kutegemea misaada na mikopo kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba za bajeti za Serikali za miaka mitano mfululizo zimeonyesha nia ya Serikali kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia 1% ya pato la Taifa na hata katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano

(FYDP-1) ilikubalika kuwa misamaha ya kodi ishuke hatua kwa hatua hadi kufikia 1% ya pato la Taifa ifikapo mwaka 2015/2016. Katika taarifa za *CAG* za kila mwaka wa fedha amekuwa akishauri misamaha ya kodi ipunguzwe ili kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya ushauri na ahadi hizo za Serikali na makubaliano katika mpango wa maendeleo hakuna jitihada madhubuti za kupunguza misamaha ya kodi nchini kwani badala yake misamaha imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, mfano kwa mujibu wa taarifa za *CAG* mwaka wa fedha 2009/2010 (bilioni 680.6), 2010/2011 (trilioni 1.01) na mwaka 2011/2012 (trilioni 1.8). Kwa mujibu wa takwimu hizi misamaha ya kodi imepanda toka 2.9% (2010/2011) hadi 4.3% (2011/2012). Vilevile misamaha ya kodi imepanda toka 19% hadi 27% ya makusanyo ya kodi. Hivyo utaona kuwa endapo tu Serikali isingengeza misamaha katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali ingepata mapato ya ziada ya shilingi bilioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali la 3 la Ongezeko la Thamani (*VAT*) lilikuwa na makundi matano mwaka 1997 lakini hivi sasa jedwali limefikia makundi 26 tofauti na nchi nyingine kama Uganda, Malawi na Kenya ambazo hazina jedwali lefu kama letu. Tanzania inatoa misamaha mikubwa ya kodi (4.3%) ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika mashariki, mfano Kenya (1%) na Uganda (0.4%) tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti na usimamizi wa fedha za umma. Tafiti mbalimbali na taarifa za *CAG* na *PPRA* zimekuwa zikionyesha ufujaji, wizi na rushwa kubwa katika matumizi ya fedha na rasilimali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (*PPRA*) imekuwa ikitoa taarifa kuhusu manunuzi ya umma, aidha imekuwa ikibainisha jinsi wakaguliwa (*procurement entities-PE*) zinavyokiuka manunuzi kwa makusudi, mfano kulipa zaidi ya mkataba, kulipa kazi ambayo haikufanyika, kulipa kwa bei kubwa zaidi ya bei iliyoko sokoni na miradi kutokuwa na

thamani halisi (*value for money*); mfano, katika ukaguzi wa viwango na thamani (*value for money*) ambapo miradi 137 ilikaguliwa ni mikataba 63 tu sawa na 46% ndiyo iliyokuwa na thamani halisi na mikataba iliyobaki ilikuwa imechakachuliwa. Kwa mujibu wa CAG na PPRA ni zaidi ya 70% ya bajeti ya mwaka inatumika katika manunuzi ya bidhaa na huduma, Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi sana katika eneo hili. Endapo eneo hili litasimamiwa kikamilifu ili kila shilingi ifanye kazi yake stahili tutaokoa zaidi ya 10% ya fedha zilizoidhinishwa katika manunuzi. Mfano, bajeti ya mwaka 2012/2013 tungeweza kuokoa kiasi kisichopungua shilingi trilioni 1.1 ambazo zingeweza kugharamia maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya unyeti wa suala zima la manunuzi lakini Serikali imekuwa mpinzani namba moja wa kukwamisha udhibiti wa raslimali za umma kwani chombo hichi (PPRA) kimekuwa hakitengewi fedha za kutosha kukiwezesha kutekeleza majukumu yake ya ukaguzi. Mamlaka hiyo katika mwaka wa fedha 2011/2012 iliweza kukagua wakaguliwa 121 tu kati ya zaidi ya 400 ambao walipaswa kukaguliwa hii 30% tu. Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 ilifanyiwa marekebisho mwaka 2011 ili kuipa uwezo zaidi wa kulinda na kudhibiti manunuzi ya umma na tukatunga sheria mpya ya Manunuzi (PPA, 2011). Mheshimiwa Rais alikwisha saina sheria hii mpya tangu tarehe 30, Desemba 2011 lakini cha kushangaza ni karibia miaka miwili sasa Kanuni hazijatolewa na hivyo sheria hajaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), CAG pia amekuwa akitoa taarifa na mapendekezo yake dhidi ya mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali, aidha amekuwa akibainisha ubadhilifu mkubwa wa fedha za umma kama; malipo hewa, kutumia fedha zaidi ya zile zilizoidhinishwa kwenye bajeti, upotevu wa vitabu vya mapato, malipo bila vielelezo n.k lakini inasikitisha taarifa zake hazipewi nafasi ya kutosha kujadiliwa ndani ya Bunge na kwamba hoja za ukaguzi zimekuwa hazijibiwi na kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwaka huu Serikali imeleta marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi (*Public Audit Act, 2008*) vifungu namba 37, 38, 39 na 40 vya sheria ya Ukaguzi wa Umma kukataza taarifa ya CAG kujadiliwa Bungeni hadi Serikali ijibu hoja hizo, upo ushahidi wa kutosha katika Bunge hili, tumeomba mara kwa mara taarifa ya majibu ya hoja za CAG toka Serikalini tangu waka 2009/2010, 2010/2011 lakini hadi sasa majibu hayajaletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya hayajawahusisha Maafisa Masuuli ambao hawajibu hoja za ukaguzi kwa wakati hadi CAG anapokuwa amekamilisha ripoti yake, badala yake sheria inatetea uzembe huo kwa kuhalalisha mianya ya ufujaji wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa Bunge katika mchakato wa bajeti. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa kusimamia na kukubali mabadiliko ya mzunguko wa bajeti (*Budget Cycle*) kuanza mapema na kumalizika kabla ya mwezi Julai sambamba na kuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Kamati ya Bajeti na Bunge hili lipate fursa nzuri ya kuchambua mapendekezo ya bajeti lazima iende sambamba na uanzishwaji wa Ofisi ya Bajeti (*Parliamentary Budget Office*). Kwani hivi sasa licha ya kuwapo kwa Kamati ya Bajeti haina nyaraka muhimu (*Budget Analysis*) zitakazo wawezesha Waheshimiwa Wabunge kuwa na taarifa za kutosha kuhusu bajeti. Taarifa zilizopo ni kwamba suala hili linapingwa na Serikali pasipo sababu zinazoeleweka na zipo taarifa kwamba hata uanzishwaji wa Kamati ya Bajeti ulipigwa vita na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni masikini sana na hivyo ni lazima kila fedha na rasilimali tulizonazo zitumike kwa uangalifu na kikamilifu. Taifa limeshindwa kufikia Malengo ya Milenia ya kupunguza umasikini na kufikia 19.5% ifikapo mwaka 2015 ikiwa kabla ya miaka miwili tu na umasikini Tanzania bado ni 33.4%, pia kwa mujibu wa ripoti ya nchi maskini sana duniani ya mwaka 2012 iliyotolewa na Shirika

la Biashara na Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNCTAD*) Jiji Geneva-Uswiss imebainisha nchi 48 zinazolingia katika kundi la nchi maskini sana (*LDC*), na Tanzania ni moja wapo kati ya nchi 33 za Afrika, katika orodha hiyo wenzetu Wakenya hawapo katika kundi hili, hii ni aibu kubwa na haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo:-

(1) Serikali ipunguze zaidi na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima katika posho, gharama za safari (ndani na nje), mafunzo (ndani na nje ya nchi), mafuta na vilainisho, viburudisho, ununuzi wa magari, ununuzi samani, ununuzi wa vifaa (sare, *stationary* na kadhalika), upangaji holela (Dodoma na Dar es salaam), gharama kubwa za matengenezo na ukarabati (barabara, majengo na magari), uhamisho holela, pia Serikali ikomeshe mishahara hewa na kuepuka malimbikizo ya riba na matumizi mengine ya mfano huu. Kabla ya kuwasilishwa kwa bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali iwasilishe Bungeni taarifa ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ikiainisha kiasi kilichookolewa na matumizi yake mapya. (*Makofi*)

(2) Kabla ya kuwasilishwa kwa bajeti ya mwaka 2013/2014, taarifa ya Kamati Maalum iliyoundwa na Mheshimiwa Spika kwa ajili ya kuishauri Serikali katika namna bora ya kuongeza mapato iwasilishwe Bungeni ili kutoa wigo mpana zaidi kwa Wabunge kuishauri Serikali kuhusu mapato na matumizi.

(3) Serikali izibe mianya yote ya upotevu wa mapato, ifuatilie na kutoza kodi na maduhuli yote yaliyokwepwa kulipwa miaka ya nyuma na ilete Mpango Mkakati wa kuongeza mapato ya ndani kabla ya kuwasilisha bajeti ya mwaka 2013/2014.

(4) Kabla ya kuwasilishwa kwa bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali iwasilishe taarifa ya mchanganuo (*detailed*) wa Deni la Taifa lililofikia trilioni 21 sasa, sambamba na madeni ya wazabuni na wakandarasi.

(5) Kwa kuwa Serikali imeahidi mara kwa mara kupunguza misamaha ya kodi na kwa kuwa tulikubaliana katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, hivyo katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2013/2014, Serikali ilieleze Bunge na Watanzania imepunguza misamaha ya kodi kwa kiasi gani? Punguzo hilo lazima liashirie kufikia 1% ya pato la Taifa ifikapo mwaka 2015/2016.

(6) Kwa kuwa suala la ugawaji wa fedha (*Disbursement*) linamkanganyiko mkubwa kati ya Hazina na watumiaji yaani Wizara, Taasisi na Halmashauri, Serikali iwasilishe taarifa ya ugawaji fedha katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 na 2012/2013 na sababu za kwa nini fedha hazipelekwi kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

(7) Ofisi ya Bajeti ya Bunge (*Parliamentary Budget Office-PBO*) inayohusisha wadau zaidi ya Wabunge ianzishwe sasa ili kuwasaidia Wabunge kuichambua bajeti kwa kina na kwa sekta ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa Bunge na Serikali. Bila uchambuzi ni vigumu kuifahamu bajeti kwa kina.

(8) Sheria ya Ukaguzi wa Fedha za Umma (*Public Audit Act, 2008*) pamoja na sheria zingine za usimamizi wa fedha yaani *Public Finance Act, 2001 na Local Government Finance Act, 1982* ziletwe Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho ili kuzipa uwezo zaidi wa kulinda, kusimamia na kudhibiti matumizi (*utilization*) ya rasimali za Taifa.

(9) Wizara ya fedha iweke rasimu za bajeti kwenye tovuti yake wakati ikiendelea kujadiliwa Bungeni. Rasimu hiyo iwe na mchanganuo wa kila Wizara (*MTEF*). Hii itawezesha wananchi wengi kufuatilia na kutoa maoni wakati bajeti ikijadiliwa, pia itarahisisha uchambuzi wa bajeti wa kitaalam (*Budget Analysis*) na pia Bajeti iliyopitishwa na Bunge iwekwe kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha ili wananchi waweze kufananisha iliyopendekezwa pamoja na ile iliyopitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naomba maelezo yangu yote haya nimeyasoma kwa

1 JUNI, 2013

summary lakini niombe sana yaingizwe kwenye *Hansard* kama ambavyo nilivyowasilisha kwako. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, huu ni utaratibu mzuri ambao unawaruhusu Wabunge wetu kuzitumia Kanuni ili kuweza kuleta ndani ya Bunge hoja mbalimbali ambazo wanaona kwamba zinastahili kuletwa Bungeni. Kwa hoja hii ya leo Mheshimiwa Mpina wewe ulijikita tu na Kanuni 28(8) lakini Kanuni namba 50 ndiyo ilikuwa inakupua mwongozo mzuri wa kujipanga sawasawa kwenye hoja hii. Kanuni hiyo ilikuwa inasema kwamba na nitaisema kwa manufaa ya Wabunge na Watanzania wote wasije wakafikiri kwamba Mheshimiwa Mpina hajapewa dakika 30 kwa makusudi ama kwa agenda nyingine.

Kanuni namba 50(2) inasema:-

“Mbunge anayekusudia kutoa Maelezo Binafsi anapaswa kuwasilisha maelezo hayo mapema kwa Spika na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi kumi na tano na maelezo hayo hayatakuwa na mjadala kuhusu jambo hilo”.

Kwa hiyo dakika zako hapa leo zilikuwa hazizidi kumi na tano. Hivyo basi ilikupasa kujipanga kwa namna ya kwamba mambo yako hayo yote yasizidi dakika 15 na hiyo imekufanya upate shida sasa na nilipokuwa naongoza kikao hiki ilinipasa kutumia Kanuni ili kukifanya kikao kiendane na yale unayotaka kuyasema bila kukiuka muda wa kusema hoja yako hiyo.

Kwa hiyo, hoja hii imewasilishwa kwa mujibu wa Kanuni na imeshasomwa kwa mujibu wa Kanuni ndani ya Bunge na Serikali imeisikia. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ikaitafakari hoja hii na itakapokuwa imetafakari iwasiliane na Ofisi ya Spika kusudi iweze kutoa Kauli, maelezo haya yatajibiwa na Kauli ndani ya Bunge. Kwa hiyo, Serikali mtakapokuwa mko tayari, mtaiarifu Ofisi ya Spika itapanga tarehe, Kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili iweze kutolewa hapa ndani ya Bunge.

1 JUNI, 2013

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa maelezo haya na baada ya kuwa na muda mrefu sana wa shughuli hapa ndani na kama nilivyosema hapo awali kwa kweli nawashukuruni sana kwa ushirikiano na uvumilivu wenu mkubwa na kwa kweli tumeonyesha kwamba tuko hapa kwa maslahi ya Watanzania. Kwa hiyo, nawashukuruni sana na sasa naomba niaihirishwe shughuli hizi za Bunge, tutakutana tena hapa ndani ya ukumbi wa Bunge siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. Ahsanteni sana.

*(Saa 7.45 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya
Jumatatu, Tarehe 3 Juni, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*